Kikao cha Pili – Tarehe 28 Septemba, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba Kuwasilisha wa Mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti naomba kuweka hati mezani Hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Kuhusu Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 85

Mpango wa Serikali Kukabiliana na Maafa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Katika miaka ya hivi karibuni, majira ya mvua yanakuwa na athari kubwa kwa wananchi na kupelekea kila msimu wa mvua Serikali kukabiliana na maafa ya mvua na maradhi ya milipuko. Katika hotuba yake ya Baraza la Eid el Fitr, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alieleza kuwa Serikali yake imeandaa mpango wa kukabiliana na maafa.

Je, ni mpango gani huo ulioandaliwa wa kukabiliana na maafa kabla hayajaleta athari kwa wananchi hasa katika vipindi vya mvua.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje swali lake Nam. 85 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, katika hatua za kukabiliana na maafa hapa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huwa inaandaa Miongozo mbalimbali ambayo itasaidia wahusika wote wa masuala ya maafa kuchukua hatua zinazostahiki kukabiliana na maafa pale yanapojitokeza. Mwaka 2011 Serikali iliandaa Sera ya Kukabiliana na Maafa, Mwaka 2011 Serikali iliandaa Mpango wa Kitaifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa yaani *(Emergency Preparedness and Response Plan)* ya mwaka 2015 Serikali Kupitia Baraza hili Tukufu ilitunga Sheria ya Kukabiliana na Maafa.

Mhe. Naibu Spika, miongozo yote hii ina lengo la kurahisisha hatua za kukabiliana na maafa ya aina yote ambayo yanaweza kuyakumba nchi yetu katika maeneo tofauti. Mpango wa kujiandaa na kukabiliana na maafa pia upo katika hatua za ngazi za Wilaya ambayo iwapo itafanyika kazi jamii yetu inaweza kuchukua hatua muafaka kabla, wakati na baada ya kujitokeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa, Serikali inaweza kuweka taratibu ambazo zinaweza kusaidia utekelezaji wa Mpango huo. Kwa mantiki hiyo, kutokana na haya yaliyojitokeza ya athari za mvua za masika kila mwaka, Serikali imeunda Kamati ya Kitaalamu ya Kubaini sababu zinazopelekea Zanzibar kuathiriwa na mvua za masika ambayo kimsingi imetekeleza wa majukumu iliyopewa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango huo wa Taifa wa Kukabiliana na Maafa. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza nichukuwe fursa hii kwanza kumshukuru Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa jitihada alizochukuwa kwa waathirika waliopata matatizo haya kuwatembelea Mkoa hadi Mkoa nimshukuru sana kwa kuwajali wananchi wake Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema.

a) Baada ya maelezo hayo jee ni lini kutakuwa na kituo cha maafa ya uokozi badala ya majanga na watu kuanza kutafutana na siyo ofisi, ofisi najua ipo ni lini Serikali itaanza kujenga kituo na maana yake kituo vifaa vyote viwepo *stand-by* tulishuhudua jimboni kwa Mhe. Ali Suleiman Shihata hata viatu buti *rain boot* vimeshindikana.

b) La pili utaratibu wa majanga na mafuruko unapotokeza tumeona hupelekwa watu maskuli jee ni lini Serikali itajenga eneo mbadala la kituo hicho baada ya taratibu za masomo huharibika na wakati mwengine skuli hufungwa ili kuwastiri ndugu zetu wanaopata maafa. Ni lini Serikali inajenga kituo muafaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje maswali yake mawili yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi lakini Mhe. Jaku ana dhamira ya kutaka kujua jee lini tutakuwa na kituo maalum cha uokozi.

Kwanza tumwambie tuu tuchukuwe na tupokee mawazo yake na ombi lake lakini kwa sasa Kamisheni ya Maafa inachokifanya yanapotokea madhara na majanga ya namna hii,

tunachokifanya ni ku-*assembly* Taasisi zote ambazo zinakuwa ni visaidizi katika jambo hili la maafa.

a) Kwa mfano, kuna wenzetu wa kikosi cha KMKM lakini tunawatumia wenzetu wa Mafunzo lakini tunawatumia wenzetu waliokuwepo Wizara ya Afya lakini pia kuna wenzetu wa Ardhi na Majenzi. Watu wote hawa tunapoungana tunaweza kujaribu kutatua kile ambacho kitakuwa kimetokea, lakini hofu ya Mhe. Mjumbe kwamba tunahitaji kuwa na vifaa vya uokozi kweli wazo lake ni jema dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba Kamisheni hii ya maafa inaweza kujitegemea kama ambavyo baadhi ya nchi kama vile Dubai na nyenginezo ambazo zimekuwa na kitengo cha namna hii kwa maana hiyo. Kwa maana hiyo wazo la Mhe. Mjumbe ni zuri tutaenda nalo kidogo kidogo kadri ambavyo Serikali itakuwa inaruhusu ipo siku na sisi tutafikia katika hatua namna hiyo.

b) Lakini kweli tukubali kwamba wakati mwengine tunapopata matatizo ya namna hii huwa tunahamisha watu wetu na kuwapeleka katika *centre* za aina moja na mara nyinyi huwa tunatumia katika majengo ya maeneo ya skuli, hili tukubaliane nalo. Lakini kwa sasa kupitia Kamati hii ya Kitalaamu ambayo tayari imeshahakuja hasa kushirikiana na wenzetu na taasisi ambazo si za kiserikali ambazo zimekuwa na ushawishi wa kutaka kuisaidia Serikali katika kuhakikisha tunaweza kuwa na *centre* ya pamoja, sasa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi kwamba tayari ipo katika hatua za mwisho za kuhakikisha sasa katika maeneo yetu yote mawili Unguja na Pemba tunaweza kuwa na nyumba ambazo litapotokea tatizo tunaweza kuwachukuwa watu wetu na kuwapeleka katika sehemu ile lakini kwa sasa tunatengeneza mazingira ili litakapotokea kwa haraka watu tuweze kuwachukua.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hili lazima tuelewe kwa sababu bado hatujakamilisha mpango wa pamoja wa kwamba likitokea tutapeleka kuwahamisha, kwa hatua za dharura inapotokea hatua nzuri sehemu pekee ambayo tunakuwa tunakuwa tunakwenda kuweka watu wetu ni katika maeneo ya skuli, likikamilika hilo tutaacha kutumia majengo ya skuli ili vijana wetu wapate elimu zao za skuli nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea jibu la ziada la nyongeza la Mhe. Jaku kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, Serikali ilishaamua kujenga vituo vya uokozi katika maeneo yaliyokubalika ikiwemo katika eneo la Malindi Unguja, Mkoani kule Pemba, Wete na Nungwi Unguja, utaratibu huo utafanywa chini ya uongozi wa kikosi chetu cha KMKM lakini pamoja na kushirikiana na wenzetu wa Kikosi cha Uokozi .Kwa hivyo utaratibu huo ulishapitishwa kwa sasa tunaimarisha kituo chetu cha mawasiliano pale Maruhubi ili kuweza kutoa taarifa kwa haraka kwa vyombo vinavyohusika pale tunapozipata taarifa hizo.

Lakini pia ikumbukwe kwamba wenzetu KMKM na kikosi cha uwokozi tunafatilia kwa karibu sana suala la majanga mbali mbali ambayo yanatokea nchini, hivyo napenda

kumuhakikishia Mhe. Jaku kwamba Serikali inalielewa hilo na itaendelea kulifanyia kazi kwa maslahi ya watu wetu.

Lakini aidha nataka niseme pia kwamba Serikali ina mpango kama alivyokwisha kusema Mhe. Naibu Waziri kwa kuhakikisha kwamba tunajenga nyumba kwa kushirikiana na wenzetu waliojitokeza kusaidiana na sisi katika suala zima la kuhakikisha wale ambao wamekuwa wakipata madhara mara kwa mara, waliojenga katika maeneo ambayo yanaathirika kila mwaka ili baada ya kupata nyumba hizo tuongeze utaratibu wa kuwahamishia huko ili waondoke katika maeneo hayo na tunaamini baada ya kufanya hivyo itapunguza kwa kiasi kikubwa sana athari zile za kutumia majengo ya skuli pale inapotokea athari za kimaafa.

Hata hivyo suala hili Mhe. Naibu Spika, huwezi kuliondoa moja kwa moja tusitumie skuli na majengo mengine ya umma pale inapotokezea dharura hiyo kwa sababu ni utaratibu ulimwengu mzima wanafanya hivyo na hakuna njia ya mkato Mwenyezi Mungu atuepushe mbali yasitokee majanga makubwa ambayo yanasababisha maafa makubwa yakahitaji maeneo zaidi kuliko matarajio yetu. Kwa hivyo tuendelee kuomba Mungu nchi yetu ikae salama, lakini pale inapotokea hatuna budi kutumia maskuli na nyumba nyengine za umma pale dharura inapohitajika, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ufafanuzi wa ziada. Mhe. Ali Suleiman Ali swali la pili la nyongeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini pia pamoja na maelezo mazuri ya nyongeza aliyoeleza naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza namuomba Mwenyezi Mungu atuepushie majanga ya maafa yasitokee katika nchi yetu na Tanzania kwa jumla hata kwa majirani zetu yasitutokee, lakini yanapotokezea majanga huwa hayachagui maeneo fulani huwa maeneo yote ya nchi yanaweza kutokea bila kutegemea jee Wizara kwa kuwa imeamua baadhi ya maeneo kwa mfano Wete, Chakechake, Nungwi na mjini haoni pana haja sasa hivi kwa kuwa Kitengo cha Maafa kipo na kinafanya kazi katika Wilaya zote pakaanzishwa makaazi maalum ya uokozi katika maeneo yote za Wilaya zetu za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Mwalikishi wa Jimbo la Kijito Upele swali lake moja na nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo tumejibu katika langu la msingi na lile jibu la nyongeza la Mhe. Waziri kwamba suala la kuwa na makaazi maalum tulichosema kwa sasa Serikali tayari imeshapitisha na ipo katika hatua za mwisho ya Serikali kushirikiana na Taasisi zisizokuwa za Kiserikali katika kuhakikisha tunakuwa na makaazi, lakini tunapozungumzia jambo la dharura linapotokea jambo la dharura kwa sasa lazima tutaenda katika majengo ya umma huo ndio mtazamo wa Serikali.

Lakini kwa muelekeo wetu tunahitahitaji kuwa na sehemu maalum itakapotokea tatizo lile watu wetu tuweze kuwatoa sehemu moja kuwapeleka sehemu nyengine zitakazokuwa salama zaidi nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nampongeza kwa majibu mazuri aliyoeleza katika suala zima la kukabiliana na maafa, lakini Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba taarifa za upatikanaji wa utabiri wa hali ya hewa ni nyenzo mojawapo muhimu sana katika kukinga athari zile kuwa kubwa maana kuna kukinga alau unawaondosha watu unajitayarisha nafikiri ni *element* moja muhimu sana na wataalamu wanaita *Early Warning System.* Kama Marekani kule umeona vimbunga vile mfululizo sasa taarifa zile ukizitoa watu unawaondoa unawatayarisha ni muhimu sana tuliwahi kulizungumza suala hili la taarifa za hali ya hewa katika vyombo vyetu vya habari, redio, *television* jee kama wewe mratibu wa shughuli za Serikali bado taarifa hizi haziendelei kutolewa unalihakikishia nini Baraza hili katika suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini Mwakilishi wa Jimbo la Dimani swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa inafanya kazi kwa karibu sana na vyombo vya Utabiri wa Hali ya Hewa, ndio maana hata tukitizama miaka miwili iliyopita mwaka jana na mwaka wa juzi Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa ukiathirika sana na mvua za masika. Lakini kwa kutumia taarifa zile kwa mwaka huu Mkoa baada ya kuzipokea taarifa kutoka katika vyombo vya hali ya hewa imetahadharisha sana wakaazi wote wa Mkoa wa Mjini Magharibi katika Wilaya zake za Mjini, Wilaya ya Magharibi A na Magharibi B na kuwatahadharisha wananchi wake wote wanaokaa katika maeneo hatarishi waweze kuondoka mapema na wengi katika maeneo yale wamefanya hivyo, ndio maana hata tukaona katika athari za mvua za mwaka huu athari iliyotokeza katika Mkoa wa Mjini Magharibi haikuwa sawa na ile athari iliyotokea katika miaka ya nyuma. Yaani hali mara hii kidogo ilikuwa na unafuu tofauti na mwaka jana, hii yote ni kutokana na taarifa tuliyokuwa tukipewa na vyombo hivi vya utabiri.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, Serikali imekuwa ikijitahaidi sana kutoa taarifa hizi na uelewa kwa watu tatizo linalotukuta ni zile hali zetu za unyonge mtu anafikiria sehemu aliyokuwepo na taarifa iliyokuwepo na vitu hivi au athari hizi ni *natural disaster* si kitu kana kwamba tutatabiri halafu kita-*predict* kitatokea, lakini pale inapotokea tunahitaji kulikabili lakini bado uelewa umekuwa ukitolewa bado, elimu imekuwa ikitolewa kupitia kamati za maafa ya kitaifa zile zilizokuwepo katika ngazi ya Wilaya na hata zilizokuwepo katika ngazi za Shehia.

Na hili Mhe. Naibu Spika, hata jana katika jibu langu la msingi nimelirudia na napenda sana niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe sisi Wawakilishi wote kupitia Wilaya zetu ni wajumbe wa Kamati za Maafa katika Wilaya zetu kwa maana hiyo tupende kuhudhuria kule kushauriana na Mwenyekiti ili kutokana na hali ya maeneo yetu,

kutokana na hali zilizokuwepo ndani ya Wilaya zetu tupate kutoa mwelekeo uliokuwa mzuri katika Wilaya ili sasa Wilaya kama Wilaya ianze kuwa na maandalizi ya kutosha mazuri ya kukabiliana na maafa na sio kusubiri tatizo hili limetokea halafu ndio tunaanza kuchangia.

Kwa hivyo tuwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe ambao wanatokana katika maeneo haya tupende kwenda, tutowe mawazo yetu, tutowe michango yetu ili kuweza kujikinga kwa pamoja tukisaidiana, kwa pamoja tukitowa elimu hii tutaweza kuwakinga wananchi wetu wengi katika maeneo yetu nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Nam. 70

Kesi za Serikali Kushindwa Mahakamani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kwa mujibu wa maelezo ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyoyatoa 14/4/2017 ni kuwa katika kesi kadhaa zinazohusu ardhi na mikataba ya barabara, huwa Serikali inashindwa Mahakamani.

a) Je, kwa nini Serikali inashindwa kesi mahakamani wakati ina wataalamu wa kushughulikia mikataba mbali mbali inayoingia na watu au kampuni nyengine.
b) Je, ni hatua gani zinachukuliwa ili kuwezesha Serikali kuepuka hasara ya kushindwa kesi Mahakamani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 70 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali lake Nam. 70 lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kesi za madai dhidi ya serikali zinafunguliwa kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Sheria Nam.3 ya 2010 inayojulikana kama "*The Government Proceedings Act*". Baada ya kutimizwa kwa masharti ya sheria hiyo, mdai na mdaiwa hutakiwa kuwasilisha madai na majibu ya madai kwa kuzingatia masharti ya sheria ya madai, sura ya nane (*Civil Procedure Decree Cap 8*) na Mahakama husikiliza na kutoa hukumu kwenye kesi za madai kwa kuzingatia masharti ya sheria hiyo ya sura ya 8.

(a) Mhe. Naibu Spika, kushinda au kushindwa kesi Mahakamani hakutegemei kuwa na wataalamu wa kushughulikia mikataba mbali mbali, bali hutegemea msingi wa kesi yenyewe. Kwa mfano, katika kipindi cha Machi, 2015 hadi Septemba 2017 jumla ya kesi 29 zinazohusu ardhi dhidi ya serikali zilizofunguliwa. Kati ya kesi hizo ni kesi nane (8) tu zilizomalizika ambapo kesi 4 serikali ilipoteza na 4 ilishinda. Aidha, kwa upande wa mikataba ya barabara,

jumla ya kesi 5 zimefunguliwa kuanzia 2015 hadi 2017 na hakuna kesi hata moja iliyotolewa uamuzi.

(b) Mhe. Naibu Spika**,** serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuepuka hasara zinazoweza kutokea kutokana na mikataba. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuipitia mikataba yote ya serikali na kutoa ushauri wa kisheria kabla taasisi husika hazija-*sign* mikataba hiyo.

Mhe. Naibu Spika**,** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeanzisha Kitengo cha Mikataba ambacho majukumu yake ni pamoja na kushiriki katika hatua zote muhimu za mikataba zikiwemo mazungumzo, ufungaji na usimamizi wa mikataba hiyo. Ofisi pia inaendelea kutoa mafunzo kwa wataalamu wake juu ya usimamizi wa mikataba katika maeneo mbali mbali nchini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimwambie Mhe. Naibu Waziri anipelekee salamu kwa Mwanasheria Mkuu tunapomfata pale asifikirie kama tunakwenda kumpiga virungu, tuna *issue* muhimu za wananchi ndio yale aliyosema Dkt. Ali Mohamed Shein anashangaa mawaziri wanaganda ofisini na kuwa na kesi sio chuki na ofisi ile, hata Simba ya Yanga ukimaliza mpira hupeana mikono.

Mhe. Naibu Spika, nilichomfata pale kuna sheria tumepitisha ya makampuni ambayo imetiwa *sign* tarehe 3, siku hiyo hiyo ikaanza kazi, mimi nilikwenda kumuuliza yeye akanambia niende kwa Naibu Mwanasheria, Naibu Mwanasheria namfahamu, kwa *AG* sifikirii kama nakwenda kupiga kirungu. Nimemfuata kutaka ushauri, lakini majibu ya Naibu Waziri ni ya kusikitisha sana, Waheshimiwa Wajumbe nisaidieni alivyokuwa anajibu.

Mhe. Naibu Spika, kushindwa kwa kesi Mahakamani hakutegemei kuwa na wataalamu kushughulikia, hiki ni kitu cha kusikitisha ndio pale tunapokuulizeni jibuni maswali, kama hakutegemei wanasheria hata mimi ningekuwa Mwanasheria Mkuu kama si mtaalamu, hiki kitu ni cha uongo. Hiyo mikataba basi hata kule Mahakamani ningempeleka mchukuzi na mvuvi tu akenda akatetea. Mhe. Naibu Spika, swali halijajibiwa anajibu hakutegemei kuwa na wataalamu wa kushughulikia.

Mhe. Naibu Spika, kitu cha kusikitisha hao wanaokutoleeni majawabu hebu waulizeni na pitieni wasikupelekeni tu, wewe utakwenda Mahakamani bila ya kuwa mtaalamu. Kitu cha kusikitisha hata golini basi utaweka boriti tu likae golini pale kama hapana utaalamu, mnatutia aibu Mhe. Naibu Waziri, utendaji huu ndio mnapoambiwa na bwana mkubwa huko tokeni mumsaidie, mikataba inaandaliwa kwa pesa hakutaki utaalamu, madai yanayoshughulikiwa Mahakamani kuna mengine yanataka suluhu ya Mwanasheria Mkuu, kuna *technique …*

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa uliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kuna *technique* na *court room techniquel* Mahakamani sasa utampeleka mtu akawa na wasiwasi pale ataweza kutetea hoja, hili swali halikujibiwa mheshimiwa mimi nataka utangulizi swali lirudiwe

tena. Haiwezekani kuja kudanganywa ndani humu hakutegemewi kuna wataalamu, itakuwaje bila ya mtaalamu hili swali Mhe. Naibu Spika nataka nitumie kanuni yako kwamba hili lirudi tena ili wananchi wapate kufahamu.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya *AG* kuna hili balaa jengine sasa hivi la makampuni juzi kuna tarehe nyengine ime-*back* tarehe ya Kamisheni huwa tunafanya nini *AG*. Mimi sitoweza kumuuliza swali…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa uliza swali…

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa nataka kutumia kanuni ya 37.

Mhe. Naibu Spika: Aah! Hapa nimekunyanyua kwa sababu ya swali la nyongeza ndio nilichokunyanyulia, kanuni itakuja baadae nataka uulize swali kama umeshauliza basi mheshimiwa akujibu, lakini nimekunyanyua kwa sababu ya swali la nyongeza tu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

a) Je, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hebu itwambie kesi ngapi ilizozichambua kutafuta *analysis* baada ya kwenda Mahakamani na kukaa na wateja kuepusha serikali kupata hasara, ni kesi ngapi tuelezwe na nyengine zinasemezeka.

b) La kusikitisha huwezi kwenda Mahakamani kama huna mtaalamu hata hapa ofisini kwetu wanasheria tumeekewa hiki kitu kinasikitisha, ni kitu cha aibu tulichotiwa. Ni lini serikali itajipanga kutumia lugha ambayo muafaka kuwa na wataalamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kwamba narejea tena kusititiza jawabu langu ambalo jibu ni sahihi kabisa, kwa sababu unapokuwa na wataalamu wa kutengeneza mikataba inawezekana ukatengeneza mikataba mizuri tu sawa, hilo ni suala moja. Lakini suala la kwenda Mahakamani kushinda na kushindwa ni suala jengine masuala haya hayawezi kwenda sambamba moja kwa moja. Inawezekana ukawa na mkataba mzuri lakini Mahakamani kuna mbinu zake mbali mbali. Kwa hivyo, inawezekana pamoja na mkataba wako mzuri lakini Mahakamani ukaweza kupoteza kesi hiyo, kwa hivyo si kuwa na mikataba mizuri tu moja kwa moja kwa maana ya kwamba unakuwa na *confidence* moja kwa moja kushinda Mahakamani. Lakini ukiwa na mikataba mizuri inapelekea Mahakamani kushinda kesi hizo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea hapo ni kwamba tunao watalaamu na wewe Mhe. Jaku shahidi wa hayo, wataalamu ambao wanaisimamia mikataba yetu hatua mbali mbali nimezieleza kwamba wataalamu tunao wa mikataba na sasa hivi tumeshafanyia *review* mikataba mbali mbali kuhakikisha kwamba mikataba ambayo serikali inaingia inakuwa mikataba bora zaidi. Kwa hivyo, wataalamu tunao Mhe. Jakuna na kutoshinda kesi si

suala la kwamba kama nilivyosema awali kwamba hatuna wataalamu wazuri. Wataalamu wazuri tunao ambao wanatengeneza mikataba lakini Mahakamani kushinda na kutoshindwa sio sababu ya kwamba pengine huku hatuna wataalamu wazuri hapana.

Mhe. Naibu Spika, katika swali jengine Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama nitakuwa nimeenda nae sambamba alitaka pengine kujua kesi ambazo tumeshinda.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, alisema swali la pili hakulisikia ninamwambia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeshughulikia kesi ngapi kuchagua ambazo zinaweza kuzungumzika kuliko serikali kupata hasara yaani kufanya *analysis* kuzichagua hizi zinazozungumzika na mteja kuliko kwenda Mahakamani kupoteza mafuta na baadae serikali kuja kudaiwa pesa nyingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Kama nilivyoeleza katika jawabu yangu mama kwamba kuna kesi mbali mbali ambazo nyengine tumeshinda na nyengine tumeshindwa. Sasa labda kama unahitaji zile nikutajie zile ambazo tulizoshindwa sawa.

Mhe. Naibu Spika, kwa faida yake kwamba tuna kesi nne tulizoshindwa na naomba niziseme hapa. Kuna kesi ya Jaku Hashim Ayoub na wenzake, *versals* Mwanasheria Mkuu hii ya Mahakama Kuu Nam.3 ya 2016, lakini hii *notice* ya kuomba rufaa ishatolewa kinachosubiriwa ni kupatiwa mwenendo wa kesi tu.

Lakini sambamba na hilo kuna kesi nyengine ambayo pia tulishindwa ni ya *Al-Hubra Marine Service Limited versals* Mwanasheria Mkuu hii kesi ya Mahakama Kuu Nam.6 ya 2016, hii imeombewa rufaa Mahakama ya Rufaa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, kesi nyengine ambayo pia tulishindwa miongoni mwa hizi kesi nne ni ya Richard Antony *versals* Mwanasheria Mkuu ya Mahakama Kuu hii ni kesi yenye Nam.8 ya 2016. Lakini sambamba na hilo tunayo kesi pia ya Amina Juma Shamuhuna *versals* Mwanasheria Mkuu ya Mahakama Kuu hii ni kesi yenye Nam.36 ya 2016.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri katika kujibu swali lake kama utachukua muda wa kusoma hizo kesi zote sasa hivi hapo ina maana muda wetu wa maswali hautotosha. Ningeshauri hiyo *list* ya kesi ambazo zimepelekwa Mahakamani na kama zimepata hukumu mpelekee Mhe. Jaku Hashim Ayoub azione.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Nashukuru Mhe. Naibu Spika.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nilichomuuliza Mhe. Naibu Waziri kesi zilizokuwa kwa Mwanasheria Mkuu sio Jaku wala nani zile za kuzungumzika ni ngapi kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zimefanyia *analysis* hizi tatu, saba wameitwa

wateja wakazungumzika mengine serikali ni kula hasara. Sikutaka mgogoro wote ule nilichomwambia kesi zilizokuwepo Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika: Anataka idadi ya jumla ya hizo kesi ni ngapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nashukuru Mhe. Jaku kwa kuleta maelezo zaidi juu ya ufafanuzi ambao anauhitaji. Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba kesi za aina hizo ambazo zinaweza kuzungumzika hatuna.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba kuna kesi nne ambazo serikali imeshindwa. Je, ni kiasi gani serikali imepata hasara kwa kushindwa kesi hizo na mikakati ipi ya wizara kuhakikisha kwamba jambo hilo halitokezei tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa hivi siwezi kumwambia Mhe. Mwakilishi moja kwa moja ni hasara ya kiasi gani ambayo serikali imeipata kwa ajili ya kushindwa kesi hizi nne nilizozitaja.

b) Ni kwamba tuna mikakati gani ambayo tumeiweka ili hizo kesi nyengine zisiweze kushindwa. Ni kwamba mikakati ipo mbali mbali kama nilivyosema kwamba tuna wataalamu wetu tunaendelea kuwafundisha, tuna vitengo mbali mbali pale Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuhakikisha kwamba tunawakomaza kielimu ya kisheria kuhakikisha kwamba kesi zetu zote tunazokwenda huko tuweze kushinda kama nyingi ziweze kushinda zaidi ya hivyo ambavyo tunavyoshinda. Nashukuru sana.

Nam. 11

Uhaba wa Wafanyakazi katika Wilaya ya Kojani

Mhe. Makame Said Juma – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kuona haja ya kuiweka Wilaya ndogo ya Kojani, lakini hadi leo kuna wafanyakazi watano (5) tu miongoni mwao wawili (2) ni walinzi.

Je, lini wafanyakazi wa wilaya hii wataongezwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ) - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Wilaya Ndogo Kojani imeanzishwa chini ya kifungu Nam.4(1) cha Sheria Nam. 8 ya 2014 ya Tawala za Mikoa ili kurahisisha shughuli za utawala na kusogeza huduma kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Ikama ya Ofisi ya Wilaya Ndogo Kojani, mahitaji ya watumishi katika ofisi hiyo ni watumishi saba (7). Kwa kuzingatia idadi ya watumishi waliopo hivi sasa Ofisi ya Wilaya Ndogo Kojani ina upungufu wa watumishi wawili, ambao ni Ofisa Mipango na Mlinzi. Katika kukabiliana na hali hiyo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tayari imewasilisha maombi ya kuruhusiwa kufanya uajiri ili kujaza nafasi tupu za wafanyakazi hao waliostaafu. Nakushukuru mheshimiwa.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nishukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwamba nakumbuka mimi Kojani si mgeni na ofisi hii iko karibu na mimi sana, kwa sababu karibu nyumba ya tatu tu au ya nne lakini sijawahi kuona wafanyakazi hawa saba hata kusikia majina yao au orodha yao katika ofisi hii. Lakini pamoja na hivyo Mhe. Naibu Spika kama ilivyo serikali inahimiza sana kuboresha katika shughuli mbali mbali kwa jamii. Nauliza ni lini wafanyakazi hawa ambao kuwa wamebakia na wameshachukua muda mrefu karibu ofisi itakufa sijui lini watapatiwa ajira ili kufanya katika ofisi hiyo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ): Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la swali mama ni kwamba ofisi hii hivi sasa ina wafanyakazi watano, lakini wafanyakazi wanaohitajika hivi sasa ni wafanyakazi saba, wafanyakazi wawili wapo katika mchakato wa kuajiriwa na wizara itachukua juhudi ya kuhakikisha kwamba wafanyakazi hao wawili wanaohitajika wanaajiriwa kwa haraka iwezekanavyo.

Lakini pamoja na hayo pamoja na kutambua kwamba ofisi ndogo ya Kojani ni ofisi ambayo inatekeleza shughuli za serikali kuu, lakini bado ziko kamati ambazo zimeundwa ndani ya suala zima la ugatuzi wa madaraka kuangalia mahitaji halisi ya watendaji katika ofisi mbali mbali zilizoko katika serikali kuu kwa maana ya Serikali za Wilaya, Ofisi za Masheha lakini vile vile na Serikali za Tawala za Mikoa. Kwa hiyo, suala hilo linafanyiwa kazi mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a).

Mhe. Waziri Kojani ni kisiwa na kisiwa ni bahari kwa sababu pana bahari pale mpaka ufike kwenye kisiwa kile na wafanyakazi wale baadhi yao wanatoka Wete. Je, kuna usafiri gani maalumu uliowekwa kwa ajili ya wafanyakazi wale wanapokwenda kule ili kuwahi kazini mapema.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kweli Kojani ni kisiwa kama vilivyo visiwa vyengine na visiwa hivi baadhi ya wakati vinakuwa na mahitaji makubwa ya usafiri, lakini pia tunatambua kwamba usafiri unakuwa mgumu katika baadhi ya visiwa hivi. Serikali kwa kulitambua hilo imo katika utaratibu wa kutayarisha *raft* ambazo ni zile boti ndogo ndogo ambazo zitakuwa zinawachukua wafanyakazi na wananchi wengine wanaokwenda katika visiwa hivyo. Suala hili litatekelezwa kwa awamu na kama tulivyoeleza hapa wakati tukiwasilisha Bajeti ya Serikali kwamba ndani ya bajeti ya mwaka 2017/2018 utaratibu wa kununua boti kwa ajili ya usafiri wa visiwa limezingatiwa.

Nam. 12

Uwezeshaji wa Wanawake na Vijana

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma – Aliuliza:

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) imezitaka kila Halmshauri za Wilaya zake kutenga asilimia 5% ya mapato yake kwa ajili ya mikopo ya vijana na asilimia 5% mikopo ya wanawake ambapo mikopo hiyo hutolewa kwa vikundi vya wajasiriamali ili kusaidia kutekeleza majukumu yao yanayowakabili.

Je, serikali yetu ya Zanzibar inafikira gani ya kuwa na mpango kama huu Zanzibar ili kuwapunguzia kadhia ya kuombaomba, wanawake na vijana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Bismillah Rahmani Rahiim. Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza naomba nianze kumshukuru *Allah (S.W.*) ambaye anaendelea kutupa pumzi zake na asubuhi hii tukakutana hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa na afya njema. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye kifungu (a) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuandaa Mpango huu mzuri wa kuwasaidia wanawake na vijana kupitia Halmashauri za Wilaya. Pia nampongeza sana Mhe. Mwakilishi kwa kuona kwamba mpango huu unahitaji kuigwa hapa kwetu kwa maendeleo ya wanawake na vijana.

Mhe. Naibu Spika, wizara inalichukua wazo hili na itakaa na wizara inayosimamia masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuona ni namna gani Zanzibar itaweza kutekeleza mpango huo kwa maendeleo ya wananchi wake.

Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2013 imeanzisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao uko chini ya wizara yangu na unaendelea kutoa mikopo kwa wananchi wote wakiwemo wanawake na vijana.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Naibu Spika, ahsante, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, ya utulivu na ya umakini zaidi. Lakini naomba nimuulize Mheshimiwa katika majibu yake ametwambia katika sheria ya mwaka 2013 wamepitisha na kusema kwamba kuna sheria maalumu ya kuweza kuwapa vijana mikopo na wanawake. Mimi nilikuwa nataka kujua ni akina nani au vijana wangapi na wako wapi ambao wamepewa mikopo kupitia Mfuko huu wa uwezeshaji. Nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohamed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Vijana ambao wamepewa mikopo ni vijana wa Pemba na Unguja, ambapo vijana kutoka Pemba waliopata mikopo hiyo ni 376 na Unguja ni vijana 140,199.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: Mhe. Waziri kama tunavyofahamu kwamba lengo la serikali ni kuwa Mfuko huu ni kuwakwamua wananchi kiuchumi, tukizingatia sana suala zito lililotukabili mbele yetu la ajira kwa vijana wetu. Lakini kumbukumbu zinaonesha kwamba kuna baadhi ya wananchi wanapopata Mfuko huu hawarejeshi.

(a) Je, wizara yake ni kiasi gani cha fedha ambacho kinawadai wananchi hawa na

(b) Ni hukumu gani ambayo imechukuliwa kupewa wananchi hao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chambani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Pesa ambazo zinadaiwa na wizara yangu ambazo wamekopeshwa wananchi na mpaka hivi sasa bado hazijatolewa ni shilingi milioni mia mbili. Adhabu inayochukuliwa dhidi ya watu hawa ambao hawarudishi pesa hizi kwanza tunawaita na kuwakusanya na masheha na kuwaelekeza taratibu zetu na tukiona maelezo yale hayakufuatwa basi hatua inayofuata ni kuwapeleka Mahakamani. Lakini napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba, mpaka hivi sasa wananchi hao wanaodaiwa fedha hizi wanarudisha fedha kwa utaratibu ambao tumewapangia na hakuna kesi hata moja iliyofika mahakamani kuhusiana na suala hili. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kuniona naomba niulize swali dogo tu la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini kwa sababu swali hili lililenga katika Halmashauri za Wilaya ambazo wilaya zote za Zanzibar zipo kwanza nataka kufahamu je, wizara hii suala hili wameshalikalia pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambao wao ndio wenye hizo Halmashauri za Wilaya? Kama wamefanya hivyo ni kwa nini wasizianzie kwenye Halmashauri za wilaya zote na wakati wilaya zote zipo na ile ni michango ya wananchi ambayo wao pia wanastahiki kupata hiyo huduma wananchi hao. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo: Kama nilivyosema kwenye jibu langu mama kwamba wizara yangu ya kazi itakaa na Wizara ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuweza kulijadili suala hili ili na wananchi wetu nao waweze kufaidika na mikpo hii kwa kupitia wizara hii. Niendelee kumwambia kwamba wizara yangu sasa hivi itakaa na wizara husika ili tuweze kutekeleza agizo hili kama alivyouliza Mhe. Mwakilishi. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Machano Othman Said maswali ya nyongeza yamekwisha au unajaribu, tunaendelea.

Nam. 5

Ukaguzi wa Bidhaa ziingiazo Nchini

Mhe. Abdalla Maulid Diwani – Aliuliza:

Serikali inastahiki pongezi kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa bidhaa ziingiazo nchini.

(a) Je, ni lini serikali itatangaza *tender* ya kumpata wakala wa ukaguzi wa bidhaa.

(b) Serikali inafaidika kwa asilimia ngapi ya makusanyo ya kodi za uchunguzi wa bidhaa kutoka kwa wakala huyo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi Nam. 5 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali inaendelea na taratibu za kutangaza *tender* kwa ajili ya ukaguzi wa magari katika nchi nne, ambazo ni Japan, Hongkong, Singapore na Uingereza. Tayari nyaraka za *tender* hizo zimeshatayarishwa na tunategemea kutangaza ndani ya robo ya kwanza ya mwaka huu.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa serikali inafaidika na asilimia 30 ya makusanyo ya kodi kutoka kwa wakala wa kuchunguza bidhaa zinazoingia nchini mpaka pale *ZBS* itakuwa na uwezo wa maabara zake wenyewe, zitakazoweza kupima bidhaa zinazoingia hapa Zanzibar pamoja na wataalamu mahiri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri swali langu la nyongeza lina (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri asilimia 30 ni pato dogo sana kwa nchi yetu ukilinganisha na wafanyabiashara ambao wanakwenda nchini. Je, kuna hitilafu gani kwamba

tuweze kuongeza kutoka asilimia 30 angalau basi twende kwenye asilimia 45 mpaka 50, *fifty fifty* baina ya yule mfanyaji na sisi ili pato liingie katika serikali yetu.

(b) Nafahamu kwamba Amani *ZBS* wana kitengo kizima cha ukaguzi na tayari vifaa vipo na kazi ile inafanywa. Je, kwa nini wizara yake bado inaendelea na mpango wa kupiga adhabu kwa wale wafanyabiashara ambao waliokuwa hajakagua bidhaa zao nje. Hii inaonesha wazi kwamba analazimisha watu wakague nje tupate asilimia 30 kuliko kuja kukagua hapa ndani tukapata asilimia mia moja zile pesa ambazo zinatakiwa kulipwa kule.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo. Tatizo kubwa ambalo limesababisha hata makubaliano kwamba sisi tuchukue asilimia 30 wao wachukue zilizobaka asilimia 70, ni kwamba kwa sababu kazi hii inatakiwa watu wanunue vifaa kwa ajili ya ukaguzi wa magari. Hivi hivi tutakuwa tunazungumza kwamba ukaguzi wa magari sio tu kwenda kuangalia magari na kuondoka lakini inatakiwa vifaa kupima kila aina ya kifaa kilichomo ndani ya gari au katika vitu vyengine kwa uhakika. Kwa sababu sisi kama serikali bado maabara yetu na hata kule bandarini hatujakuwa na vifaa vinavyotakiwa, na kwa kuwa tunaelewa kwamba gharama za kununua vifaa zinawafanya wale ambao tumewapa kazi hii wapewe pesa nyingi zaidi kwa ajili ya gharama hizo za vifaa na kazi wanazofanya. Lakini bado tunatizama tena kipindi cha miaka mitatu kuona kwa kiasi gani tunaweza kuja ku-*review* tena pindipo tutakuwa na vifaa vya kutosha katika bandari yetu.

Swali lake la pili kwamba tunafanya makusudi ili kuwapa wale ambao wanatumia pesa nyingi kushinda sisi ili waweze kupata fedha nyingi sio la kweli na mimi sikubaliani nalo Mhe. Nabu Spika. Ahsante.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wakala wetu wa Dubai amekuwa akiwanyanyasa na kuwabughudhi wafanyabiashara wanaopeleka gari kudhaminiwa pale na kuwarudisha mara kwa mara bila ya sababu za msingi, hata likiwa *tire* tu limebomoka.

Je, serikali inatoa tamko gani kuweza kuwasaidia wafanyabiashara wadogo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, mimi sina hakika kama huyu wakala wetu wa Dubai anawanyanyasa wafanyabiashara. Nasema hivyo kwa sababu tulipewa malalamiko hapo nyuma kwamba kuna matatizo kule Dubai, lakini Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, lilipeleka timu Kamati yetu ya Fedha na Uchumi pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko; walikwenda Dubai wakafanya uchunguzi na wakakaa nao. Taarifa iliyorudi kwangu mimi haikusema kwamba haya makosa yamethibiti na nikaambiwa kwamba wanafanya kazi yao kwa mujibu wa tulivyokubaliana.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo mimi sina ushahidi na hayo anayosema Mhe. Mohammed Said Mohammed. Kwa kweli timu ilikwenda ikaangalia na imerudi na maoni tofauti na

mapendekezo mengine kwamba hii kampuni inafanya vizuri. Kwa hivyo, mimi sikubaliani nayo na anayosema Mhe. Mohamed Said Mohamed sasa hivi kwa ushahidi wa hii kamati yetu yenyewe ya fedha iliyokwenda kule kuonana na hawa wanaohusika.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Lakini kabla nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya swali mama na swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la ukaguzi wa bidhaa zinazohusiana na ujenzi ikiwemo mabati, *tiles*, vigae, lakini vile vile bidha au vifaa vinavyohusiana na mambo ya maji kama mipira, mabomba na kadhalika; hivi sasa kumekuwa na wimbi la bidhaa *fake* kutoka nje na maabara yetu ya *ZBS* haina kitengo kinachohusikana na ukaguzi au uchunguzi wa bidhaa hizi.

Je, hivi sasa bidhaa hizi zinafanyiwa uchunguzi wapi, lakini ni lini shirika letu au taasisi yetu hii ya *ZBS* itakuwa na maabara ambayo inachunguza vifaa hivi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mhe. Mwakilishi kuhusu ukaguzi wa bidhaa nyingi zaidi za ujenzi. Ni kweli sisi pale katika kituo chetu hatujakuwa na maabara ya kuangalia vifaa hivi vya ujenzi, lakini bado tunafanya kazi na tunavikagua na wakati mwengine ikibidi tunapeleka *TBS* vile vifaa ambavyo tunakuwa na wasiwasi navyo kwa ajili ya kwenda kukaguliwa kwa uhakika na ukamilifu zaidi. Lakini niseme pamoja na kwamba hatuna maabara lakini baada ya kupokea taarifa inategemea na *TBS* inavyosema na wakati mwengine huwa tunatumia vile vile kama kitu ambacho kinagusa pia maslahi ya chakula tunatumia vile vile bodi yetu ya vyakula hapa Zanzibar. Tumeshachukua hatua mbali mbali za kuweza kufelisha na kuviharibu baadhi ya vifaa, nadhani mnakumbuka kwamba tulifelisha mafuta yaliyokuwa ya gari ambayo yalikuja hapa yakawa hayajafikia viwango, tukayafelisha na kontena nzima hiyo iliyokuja tukaitoa.

Kuhusu lingi tutakuwa na maabara hii ni kwamba tunakwenda kwa awamu. Nafikiri katika kipindi cha mwaka huu mwaka 2017/2018 itakuwa tumepata bajeti ambayo tutaiongezea baadhi ya maabara nategemea na hii nayo itakuwemo katika mkumbo huu. Ahsante Mhe. Nabu Spika.

Mhe. Nabu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kidogo nitaomba radhi kwa kubadilisha mtiririko wa *order paper* ya kwamba sasa hivi swali linalofuata ni la 47, lakini kutokana na dharura ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ningeomba niridhie swali lake lije sasa hivi halafu baada ya hapo litakuja swali ambalo lilikuwa linafuata. Sawa? Naona nimekubaliwa kwa hiyo katibu.

Nam. 96

Mbegu Bora za Zao la Muhogo

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa zao la muhogo ni chakula muhimu kwa sasa duniani kinachohitajika nchi mbali mbali ikiwemo China, ambao wanahitaji idadi kubwa ya muhogo mkavu. Na kwa kuwa mbegu za muhogo uliopo kwa sasa zinaonekana kupungua sana uzalishaji kutokana na sababu mbali mbali.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kutafuta mbegu mbadala za muhogo na kuwapa wakulima mbegu ambazo ni bora zinazozalisha muhogo zaidi ili kuongeza kipato cha wakulima wetu.

(b) Je, wizara imefanya utafiti gani ili kuweza kugundua mbegu bora ya muhogo ambayo inakubaliana na ardhi yetu.

(c) Kama wameshaigundua je, mbegu hiyo inaitwaje na inapatikana wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 96 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa kuwa muhogo ni zao lenye umuhimu sana, vile vile zao hili linalimwa na wakulima wengi hapa Zanzibar. Ukweli usiopingika kwamba zao hili la muhogo limekuwa likikumbwa na maradhi mengi sana.

Mhe. Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wakulima na wadau wengine wamekuwa wakifanya jitihada kubwa ya kufanya utafiti katika kuliendeleza zao hili, ni pamoja na utafiti wa kupata mbegu bora zinazotoa mazao mengi na kustahamili maradhi hayo. Baada ya kutoa maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali yake namba 96 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu tayari imeshatoa mbegu bora za muhogo ambazo zina uwezo mkubwa wa kustahamili maradhi ya virusi na zenye kutoa mavuno makubwa kwa wastani wa tani 25 kwa hekta. Mbegu hizo ambazo zinapandwa katika maeneo mengi ya visiwa vya Unguja na Pemba ni pamoja na aina ya Kizimbani, Machui na Mahonda.

(b) Mhe. Naibu Spika, katika kufanya tafiti hizo, wizara pia inaangalia mbegu ambazo zinafanya vizuri katika ardhi yetu, na mbegu hizo zinazopendekezwa na kuendelezwa pia zina sifa ya kustahamili hali ya udogo na mazingira ya hapa visiwani. Aidha, wizara yangu inaendeleza tafiti nyengine katika vituo vyetu vya utafiti Unguja na Pemba na katika mashamba ya wakulima ili kutafuta mbegu nyengine zitakazokuwa na sifa kama hizi au zaidi ya hizi ili kuwasaidia wakulima wetu na wananchi kwa jumla kupata mavuno mazuri na kuongeza kipato chao.

(c) Mhe. Naibu Spika, mbegu hizo ni pamoja na mbegu aina ya Kizimbani, Machui, Kama na Mahonda. Mbegu zinapandwa katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja na Pemba yakiwemo Kinyikani, Junguni, Madinani, Makombeni, Kengeja, Machui, Bumbwini, Matangatuani, Kizimbani, Dunga, Selem na mengineyo. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kuna aina za mbegu ambazo amezitaja hapo juu mbegu zilizotolewa kwa wakulima, sasa kwanza mimi nilitaka nijue hizi mbegu zilitolewa mbegu hizi kwa ajili ya majaribio wakapewa wakulima maalum au zilitolewa kwa wakulima wote.

(b) Kama zilitolewa kwa wakulima wote ni sababu gani inayowafanya wakulima waendelee kuzitumia mbegu zile za zamani ambazo hazitoi mazao bora wakaacha mbegu nzuri zinazotoa mazao mazuri. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi Omar Seif Abeid kama ifuatavyo:-

- Mbegu hizi zilitolewa kwa wakulima wote ili waweze kupata mazao bora na mazuri sasa kwa nini hawatumii wakulima hili inabidi ni suala la kukaa tukafanya ufatiliaji mimi na wewe ili tuwashajihishe watumie mbegu zile ambazo tumezitoa sisi Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi. Ahsante.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini pia nimpongeze kwa utafiti ambao umeshafanyika katika wizara kwa kuona hizi mbegu ingawa hajatutajia majina yake, lakini tunavyojua mbegu ambayo sasa hivi inasambazwa haswa katika hivyo vijiji ambavyo alivitaja na mbegu hii inapandwa sana ni mbegu ya Kalolo ambayo muhogo wake ni mchungu ajabu ya Mungu na muhogo huu sana unatumika kwa chipsi na makwaru.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna mbegu nyingi ambazo zipo na mbegu hizi ni nzuri hata kama utapata ile mbegu yake moja tu unaweza ukapanda matuta matatu. Lakini bado mbegu hizi zinaonekana kama hazifatiliwi na hazifanyiwi kazi.

Je, Mhe. Naibu Waziri kuna utafiti gani ambao utafanyika tena kwa hizi mbegu ambazo tunazijua sisi wananchi na muhogo wake ni mzuri akina mwari, sepide, hameni mjini na nyenginezo ambazo zinapandwa na zinapendwa na muhogo wake *mashaallah*. Kuna utaratibu gani ambao tutamika ili mbegu gizi zienee na wananchi wazitumie na soko liongezeke zaidi ili nchi yetu izidi kupata mapato kupitia Wizara ya Kilimo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu swala lake la nyongeza Mhe. Hidaya Ali Makame wa viti maalum swali lake kama ifuatavyo.

Kwanza ningemuomba Mheshimiwa Mwakilishi aniletee hilo jina alilosema kwamba muhogo mchungu nitashukuru sana.

Halafu jengine hizi mbegu ambazo anasema ni nzuri pia tushirikiane na sisi Wizara ya Kilimo kutuletea kuwashajihisha wananchi hawa. Lakini kwa nilivyowauliza watu watu katika utafiti wao walioufanya mbegu kama hizi mwari na mbegu nyengine ambazo zinaitwa kipusa, matemwe hizi zinaenea maradhi kwa wingi sana kwa sasa hivi kipindi hichi na ndio maana tumeacha kuzitumia.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuniona kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali na mimi niendelee kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kuweza kusimamia wizara hii ijapokuwa waziri wake hayupo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza swali Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni nchi ya China ilitangaza kununua muhogo Tanzania jambo ambalo ni zuri na itaifanya nchi yetu kuweza kupata kipato kikubwa na kutangaza soko.

Je, nchi yetu ya Zanzibar imejitayarisha vipi na soko hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ni kweli China imetangaza hivi karibuni kununua muhogo Tanzania. Lakini niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wote tuwashajihishe wakulima wetu kulima muhogo kwa wingi ili tuweze kukamilisha ile idadi ambayo nchi ya China inataka na yule ambaye hana mbegu basi anakaribishwa katika Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kupata mbegu na vile vile kupata utaalamu zaidi ili waweze kupata mazao mengi zaidi. Ahsante.

Nam. 44

Umuhimu wa Kusoma lugha ya Kiswahili na Kiarabu

Mhe. Shehe Hamad Matar – Aliuliza**:**

Kwa kuwa kumekuwa na msukumo mkubwa katika vyuo vikuu kufundisha lugha za kigeni, kama vile kiingereza, kifaransa, na sasa kichina na kutotilia nguvu lugha yetu ya Kiswahili ambayo haitambuliki vyema na pia lugha ya kiarabu ambayo ni lugha kuu ya Kitabu Kitukufu cha Waislamu.

(a) Je, ni lini Serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu itaanza kutilia mkazo kufundisha lugha yetu ya Taifa ya Kiswahili kwa lengo la kuitambua vyema na pia kuwatengenezea vijana soko la ajira nje ya nchi.

(b) Je, ni lini Wizara ya Elimu itaweza kutilia mkazo kufundisha lugha ya kiarabu nchini ili kuweza kukabiliana na ukosefu wa wataalamu wa lugha hiyo

hasa pale tunapoweka mikataba na nchi za kiarabu lakini pia kwa Utalii wetu ambao umekuwa utaongezeka kwa kupokea watalii kutoka nchi mbali mbali zikiwemo nchi za kiarabu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:**

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatilia mkazo mkubwa katika ufundishaji wa masomo yote yaliyopendekezwa na Mitaala katika ngazi zote za elimu. Lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha yetu ya Taifa ndio inayotumika kwa kufundishia madarasa ya elimu ya maandalizi na msingi ambapo kila mtoto hujifunza vyema kupitia lugha yake ya asili "Lugha mama". Katika madarasa ya msingi ya juu Darasa la 5 na 6 ambapo kipindi hiki tunamuandaa mwanafunzi kwa ajili ya kumudu masomo yake ya Sekondari, lugha ya Kiswahili inaendelea kutumika katika kufundishia masomo ya Kiswahili, Uraia, Michezo, Historia, Dini na Elimu Amali. Somo la Kiarabu linasomeshwa kwa wanafunzi wote kuanzia maandalizi hadi Kidato cha Pili kwa lugha ya Kiarabu.

Kwa hivyo, Lugha za Kiswahili na Kiarabu zinasomeshwa kikamilifu katika skuli zetu za msingi juu, sekondari, vyuo vya ualimu na hata vyuo vikuu vya hapa nchini.

Katika Chuo cha Ualimu cha Kiislamu Unguja na cha Pemba vinatoa Stashahada ya masomo ya Lugha ikiwemo Lugha ya Kiswahili na Kiarabu.

Mhe. Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kinatoa Shahada ya kwanza, shahada ya pili na shahada ya tatu katika somo la Kiswahili. *SUZA* pia inaendesha mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni kutoka nchi mbalimbali ambao wanakuja aidha kwa kujifunza Lugha ya Kiswahili au kwa kufanya kazi nchini Tanzania. *SUZA* imeanzisha mashirikiano na vyuo vikuu vya Marekani ambapo hubadilishana uzoefu wa namna ya kukifundisha na kukitumia Kiswahili kwa usahihi katika kuwasiliana. Walimu wa Kiswahili kwa wageni walipata nafasi ya kwenda nchini Marekani kufundisha Lugha hiyo. Aidha, wanafunzi kutoka Marekani wamekuwa wakifika visiwani mwetu kupitia programu hiyo. Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumeit vijana wa Kizanzibari na wageni wanasomea Shahada ya kwanza ya Kiswahili na somo jengine kwa mujibu wa ufaulu wao.

Mhe. Spika, kwa upande wa Lugha ya Kiarabu Wizara inajitahidi sana kuimarisha ufundishaji wa somo hilo katika ngazi ya elimu ya Maandalizi hadi Chuo Kikuu. Vile vile, walimu nao hupatiwa taaluma ya somo hili ili waweze kufundisha vizuri katika Vyuo vya Ualimu vya Zanzibar kwa ngazi ya Stashahada ya Dini na Kiarabu inayotolewa katika vyuo vya Ualimu vya Kiislamu Unguja na Pemba. Aidha, kwa ngazi ya Shahada ya kwanza ya Kiarabu hutolewa katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) na Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumeit Chukwani. Vile vile Chuo Kikuu cha Zanzibar (*ZU*) Tunguu hufundisha somo la Kiarabu kwa wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza.

Mhe. Spika, Jitihada zote hizo zinachukuliwa kwa lengo la kuzijengea hadhi Lugha zetu hizi mbili ambazo ni muhimu kwa kudumisha maadili na maendeleo ya Taifa letu. Ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Matar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa niulize swali nyongeza:-

Kwanza sina budi nimpongeze kwa majibu mazuri na marefu ya kina kabisa ya Mhe. Waziri. Lakini nina maswali mawili (a) na (b) ya nyongeza:-

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea kutopewa kipaumbele wanafunzi ambao wanamaliza darasa la kumi na mbili na kufaulu kiswahili na kiarabu wakati wa ajira humu nchini.

(b) Je, ni lini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaanza kutoa motisha kwa wanafunzi ambao wanafaulu vyema katika masomo ya kiswahili na kiarabu ili waweze kutengeneza ajira za nje katika masomo haya kwa nchi ambazo zinahitaji lugha ya kiswahili hasa kiswahili.

Ni lini Wizara ya Elimu itaweza kutoa kipaumbele au motisha kwa wanafunzi wanaofaulu vyema katika masomo ya kiswahili na kiarabu ili waweze kujitengenezea mfumo mzuri wa ajira za nje hasa somo la kiswahili. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba arejee suala la (a) sikulisikia.

Mhe. Shehe Hamad Matar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu. Ni sababu zipi zinazopelekea kutopewa kipaumbele kwa wasomi ambao wanamaliza darasa wa kumi na mbili na kufaulu vyema kiswahili na kiarabu kudharauliwa wakati wa ajira. Mara nyingi sana huwa wanatajwa waliofaulu kiingereza na hesabu katika ajiara hawatajwi wenye kiswahili na kiarabu. Hilo ndilo swali langu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa napenda kumjibu Mhe. Shehe Hamad Matar swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Tunapozungumzia suala la ajira na masomo ni mambo mawili ambayo kila moja lina lengo lake. Mara nyingi katika sera za kimataifa tunajiuliza nini madhumuni ya kusomesha kupata ajira au kupata elimu. Ikiwa ni kupata ajira kama soko la ajira litakuwa limejaa tufunge vyuo na skuli hapana na kwa maana hiyo tunasomesha kwa ajili ya kupata elimu ambayo mtu ataitumia elimu hiyo kwa ajili ya kujiajiri au kuajiriwa na serikali.

Kwa hivyo, sisi kama Wizara ya Elimu tutaendelea kusomesha masomo yote bila ya kujali kuna ajira ya serikali au laa. Katika mtizamo wa sasa tunahimiza sana kwamba watu wajitayarishie ajira zao kwa lugha nyengine tunasomesha ujasiri amali mtu ambaye

amesoma kiarabu au kiswahili anaweza akatayarisha ajira yake na wako watu ambao wamefanikiwa katika kujiajiri wenyewe kwa kutumia kiswahili na kiarabu. Kwa hivyo hatudharau somo lolote.

(b) Kwa mtizamo huo huo tutaendelea kutoa kipaumbe kwa masomo ambayo yametajwa kwamba ni kipaumbele cha taifa yametolewa na Tume ya Mipango Zanzibar. Lakini pia na haya ambayo hayatajwa kama vipaumbele Wizara ya Elimu itaendelea kuyasomesha ikiwemo masomo haya ya kiarabu na kiswahili. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nashukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini niongeze kwa swali lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa tunaendana na kasi ya kushidana kielimu pengine katika shule za *Private* na shule za serikali. Ni sababu zipi zinazofanya shule la serikali zisianze kusomesha kiengereza kutoka darasa la kwanza.

(b) Kama ni kipaumbele ambacho tunakiona katika elimu baina ya elimu inayotolewa na *Private* na elimu inayotolewa na shule za serikali kama yeye mfano ni Waziri wa Elimu ni sababu zipi zinazofanya watu wengi ambao wana uwezo na hawana uwezo lakini wanapendelea sana kwenda kwenye shule za *Private* wakaziacha shule za serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Said Sarahan swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Ni kwamba katika kusomesha lugha na kwa upande wetu lugha ya kiswahili na kiingereza kwamba tunaangalia mitaala inasemaje na mitaala ndiyo inayoamua somo gani lisimeshwe katika ngazi gani au lugha gani isomeshwe katika ngazi gani na kwa sasa Tanzania tuna lugha mbili ambazo tunazitumia kama ni njia ya kusomeshea lugha ya kiswahili na lugha ya kiingereza. Sasa ni mitaala yenyewe ndiyo inayoamua kama lugha ipi itumike katika ngazi ipi na mitaala hiyo inaamua hivyo kutokana na mahojiano, kutokana na mijadala mbali mbali na maoni ambayo tunapata kwa wadau mbali mbali wa elimu wakiwemo wazazi na wataalamu wengine.

(b) Kuhusu kusoma katika skuli ya binafsi na za serikali hili ni suala wakati mwengine ni suala la maamuzi ya mzazi. Wakati mwengine wazazi wanadhani kama labda katika Skuli za Serikali pengine ufanisi wao katika kusomesha ni mdogo, lakini ni dhana sio sahihi. Ukaguzi tunaufanya kupitia wataalamu wetu wakaguzi kwa kweli viwango vya usomeshaji vinafana kwa sababu wote wa skuli binafsi na skuli za *Private* wanalazimika kufuata mitaala yetu kwa mujibu wa sheria.

Kwa hivyo, wakati mwengine kuwapeleka vijana wetu katika skuli za binafsi tunapeleka kama ni *fashion* tu lakini si hasa katika kuamua upi ubora upi ubaya katika elimu. Ahsante.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante na mimi Mhe. Naibu Spika, kunipa na mimi nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja kama ifuatavyo:-

Lugha ya kiarabu ni lugha ya lazima kwa waisilamu wanaume na wanawake na hususan kwa nchi yetu ya Zanzibar kuliko lugha ya kiingereza. Lakini la kusikitisha ni kwamba lugha ya kiingereza imepewa vipindi vingi skuli kuliko lugha ya kiarabu. Ikiwa lugha ya kiingereza inafundishwa vipindi sita kwa wiki lugha ya kiarabu imepewa vipindi viwili tu kwa wiki.

Je, Mhe. Waziri lini wizara yako itaamua kuongeza vipindi vya kiarabu badala ya viwili alau vikawa vipindi vinne kwa wiki ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Said Omar Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kwamba suala la mitaala ni suala ambalo kwa namna fulani ni la kitaalamu sio suala la kukurupuka, ni kwamba kutokana na mitaala inavyotayarishwa mpaka sasa wizara imejiridhisha kwamba vipindi viwili vinatosheleza kusomesha somo hilo. Tunasema hivyo kwa sababu kila somo limegaiwa vipindi vyake kwa mujibu wa uzito wake,na kwa mada zake na kwa mujibu wa vipaumbele vilivyopo.

Kwa hivyo, tunaamini kwamba mpaka sasa vipindi vilivyowekewa lugha za Kiarabu vinatosheleza na vinakidhi haja ambayo inatakiwa. Endapo vitasomeshwa vizuri kabisa, walimu wakasomesha vizuri kabisa na wanafunzi wakasikiliza vizuri kabisa, basi vipindi hivyo vinatosheleza wanafunzi kupata umilisi wa lugha ya Kiarabu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 47

Upimaji wa Maeneo Yaliotangazwa na Serikali

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Kisiwa cha Fundo Serikali imekitangaza kwamba ni moja kati ya maeneo ya uwekezaji na tayari Serikali ipo mbioni kukamilisha mradi wa kupeleka umeme kisiwani humo.

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kuyapima maeneo yaliyopo Magharibi ya Kisiwa cha Fundo ili kujitayarisha kwa ajili ya uwekezaji.

(b) Je, kwa sasa kuna hati yoyote ambayo imetolewa kwa wawekezaji waliowekeza katika kisiwa cha Fundo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 47 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, kuhusu uwekezaji katika Kisiwa cha Fundo, serikali kupitia wizara yangu bado haijapima maeneo ya Magharibi ya Kisiwa cha Fundo

kwa ajili ya uwekezaji, bali inategemea kuandaa mpango wa matumizi wa eneo hilo.

(b) Mhe. Naibu Spika, hadi sasa katika Kisiwa cha Fundo kumetolewa mkataba wa ukodishaji wa ardhi. Moja ni *Land Lease* kwa *Fundo Lodge Limited.* Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba hamna hati kwa ajili ya uwekezaji iliyotolewa katika Kisiwa cha Fundo, na kwa sababu mimi Fundo nakufahamu vizuri sana na nina watu kule Fundo ambao tunawasiliana, iwe kwa wiki au kwa mwezi. Lakini hatupitishi mwezi bila ya kuwasiliana, na kwa sababu najua kwamba kuna wawekezaji na mmoja kaanza tokea mwaka 2014, lakini nashangaa wewe kuniambia kwamba hakuna mwekezaji.

Swali langu liko hapa. Je, imekuwaje yule mwekezaji kampuni yake siijui inaitwaje, lakini mimi namjua msimamizi anayeitwa Hassan, akaweza kuwekeza na akaenda serikalini akapewa vibali vya ujenzi wa hoteli ambayo iko Kaskazini mwa Kisiwa cha Fundo, akaweza kuendeleza hoteli yake, tokea mwishoni mwa mwaka 2014 hadi leo yupo. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, je mmejipanga vipi kwa sababu yale maeneo sasa yameshakuwa mali Kaskazini mwa Fundo upande wa Magharibi. Upande wa Mashariki ni makaazi, lakini upande wa Magharibi ni maeneo ambayo ni mazuri kwa uwekezaji. Je, mmejipanga vipi kuyapima, badala kusubiri watu kupata vibali kutoka *ZIPA* ndio mkayapime. Nyinyi wizara mna mpango gani wa kuyapima mkayaweka na kuyatayarisha kwa ajili ya uwekezaji. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa rubusa yako naomba kulijibu swali la nyongeza la Mhe. Omar Seif Abeid wa Jimbo la Konde kama ifuatavyo. Ni kweli katika Kisiwa cha Fundo kuna mwekezaji, lakini labda niseme nikiri kwamba swali lilivyoulizwa mwanzo, swali la hati watu wakizungumza hati wanafikiri ni *Right of Occupancy*, na ndio kama vile alivyojibu Mhe. Naibu Waziri wangu kalijibu vizuri na kwa ufasaha.

Lakini Mhe. Naibu Spika, tunazungumzia mkataba wa wawekezaji, ndio alichokuwa akizungumzia *issue* ya *land lease.* Kwa hivyo, kama ni *land lease* kweli imetolewa ya katika Kisiwa cha Fundo ya Fundo *Lodge Limited* ambayo uliyemtaja ndugu yangu Hassan Jojoba ndio mmiliki wa hiyo *land lease*, kwa hivyo hapa swali lilivyokuja halikuja kwa maelezo yale ya hati, kwa hivyo hati ile ilichukuliwa ni hati ya *Right of Occupancy,* ndio maana jibu sahihi alikupa Mhe. Naibu Waziri wangu. Kwa hivyo, naomba nikiri kwamba *Land Lease* mkataba wa ukodishwaji wa uwekezaji umetoka kwa *Fundo Lodge Limited* ya ndugu Hassan.

Lakini la pili swali ambalo ameliuliza la kuyapima. Kama swali la awali lilivyojibiwa kwamba wizara yangu itapima eneo hilo pale itakapojitokeza haja, kwa sababu sasa hivi kweli eneo lipo, lakini kama mwekezaji hajatokea wala hajaomba wala *ZIPA* haijatoa

chochote, kuyapima tu maeneo ambayo wananchi sasa hivi wanayatumia kwa shughuli zao, kwa hivyo ni kama tunataka kufanya kitu ambacho hakiko sahihi, kwa sababu maeneo yale yanajulikana na katika *master plan* yetu yote yameonekena kama haya ni ya kilimo, haya ni ya uwekezaji na haya ni ya hivi, lakini *by the time* hatujaya-*specify* moja kwa moja. Lakini kwa mawazo uliyoyatoa mimi naomba niyachukuwe kwamba sisi tuendelee kuyapima tukae nayo, pale mwekezaji atakapotokea, basi iwe kazi rahisi ili ile kazi isije ikajirejea. Naomba kuwasilisha Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa utalii ni sehemu ya uwekezaji na Kisiwa cha Fundo inategemewa kuwekeza sehemu ya utalii. Je, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira imeshawahi kushirikiana na *ZIPA* katika kutoa elimu kwa wananchi wa Kisiwa cha Fundo juu ya namna gani utalii utaweza kuleta faida na namna gani utalii unaleta hasara katika Kisiwa cha Fundo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mattar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, tayari elimu imetolewa na ndio maana tayari mwekezaji mmoja yuko kule na ndio huyo anayeitwa Hassan. Lakini pili tutazidi kuendelea kutoa hii elimu na tunashirikiana vizuri na *ZIPA.* Ahsante.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katiba yetu ya Zanzibar sehemu ya kwanza inatambua kwamba Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la visiwa vya Unguja na Pemba, pamoja na visiwa vidogo vilivyozunguka na bahari yake, ambapo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

(a) Mhe. Naibu Spika, nilitaka kufahamu kwamba Fungu la Mbaraka au Latham Island lipo katika upande upi wa Jamhuri ya Muungano.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tuna mafungu mengi ya mchanga ambayo yanatumika sasa katika masuala ya uwekezaji na wageni kutembelea pande zote kwa upande wa Unguja na Pemba. Sasa nilitaka kujua je, ni utaratibu gani ambao serikali imejipanga ili kuyadhibiti haya mafungu ili kupunguza uharibifu wa mazingira na kuweka utaratibu rasmi, ili mapato na kutokana na mafungu haya kutumika kwa ajili ya matembezi ya wageni wetu, yawe katika mtiririko na kufanyika katika mtazamo ambao utakuwa ni rasmi na ambao unatambulika kisheria, pamoja na kuongeza pato la serikali. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Simai Mohamme hili swali lako umeuliza kisiwa gani? Kisiwa ulichokiuliza katika swali lako la (a) ni kisiwa kipi?.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, nimeinukuu katiba ya Zanzibar

Mhe. Naibu Spika: Hapana, nimekufahamu uliponukuu. Umeuliza swali, nataka kujua katika kisiwa ambacho umekusudia ujibiwe kutokana na hiyo nukuu yako ni kisiwa kipi?

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, nimezungumza kwa kunukuu katiba ya Zanzibar ambayo pia imetambua visiwa pamoja na eneo la bahari pamoja na haya mafungu. Sasa hapa najua serikali inashirikiana, wote wanafanyakazi kwa kushirikiana kwa pamoja, mafungu yote yanayotumika ni sehemu pia ya mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hivyo, kama ni mafungu na visiwa ni maeneo tofauti, basi ningemuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atusaidie hapa, ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Nina wasiwasi swali lako sio swali la msingi Mhe. Mjumbe. Kwa hivyo, ningekuomba sana swali lako litengeneze vizuri halafu lije lijibiwe kama swali la msingi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, lakini naona Mhe. Naibu Waziri keshaondoka bado kuna swali jengine.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umeondoka hata sijakuruhusu. *(Makofi)*

Tunaendelea, tunaendelea.

Nam. 124

Ziara ya Viongozi Katika Vituo Vya Afya Jimbo la Mfenesini

Mhe. Machano Othman Said – Aliuliza:-

Tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwezi wa Machi, 2016. Uongozi wa Jimbo la Mfenesini umekuwa ukifanya jitihada kubwa ili Waziri na Naibu Waziri wa Afya watembelee vituo vya Afya vya jimbo hilo. Hata hivyo juhudi hizo zimegonga mwamba kwani hadi leo viongozi hao hawajafanya ziara hiyo, jambo ambalo linawakatisha tamaa wananchi wa Jimbo la Mfenesini.

(a) Kwa kuwa huduma za afya bora ni moja ya malengo maalum ya Mapinduzi Matukufu ya 1964, Je, ni lini viongozi wa Wizara hiyo watakuwa tayari kuacha viti vyao Ofisini na kutembelea jimbo hilo.

(b) Je, ni lini Wizara itaanzisha utaratibu wa kuyapatia majimbo idadi ya mgao wa dawa zinazopelekwa katika vituo vyao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 124 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida Mhe. Waziri wa Afya na Mhe. Naibu Waziri wa Afya wamekuwa na utaratibu maalum wa kutembelea vituo vya afya Unguja na Pemba, yaani ziara kwa kadri hali inavyoruhusu. Sote tunafahamu kwamba vituo vya afya ni vingi na nakiri kwamba baadhi ya vituo hivyo bado hatujapata fursa ya kuvitembelea, lakini sio kwamba hatutovitembelea, vituo hivyo vimo katika ratiba ya ziara zitakazoendelea *Inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwezi wa Machi, 2016 na kupitishwa kwa bajeti ya mwaka 2016/2017, uongozi wa Wizara ya Afya, maafisa mbali mbali wa afya Mkoa na Wilaya tulitembelea vituo mbali mbali vya afya, vikiwemo vituo vifuatavyo:

(a) Kituo cha Afya Chuini, Kituo cha Afya Selemu, Kituo cha Afya Bumbwisudi, Kituo cha Afya Mfenesini, na jengo la Kituo cha Afya Mbuzini. Ziara hizi zilifuatiwa na kutolewa kwa zawadi kwa mama na mtoto kwa baadhi ya vituo vinavyozalisha.

Mhe. Naibu Spika, katika kufuatilia jibu la swali hili, watendaji wangu wamegundua kwamba baadhi ya vituo nilivyovitaja Kijografia vimo katika Jimbo la Mfenesini.Tunashukuru katika ziara za vituo hivi tulipata mashirikiano makubwa kutoka kwa baadhi ya Masheha na Maafisa wa serikali wa Wilaya.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa bado wizara haijafikia utaratibu wa kuyapatia majimbo taarifa za idadi ya mgao wa dawa zinazopelekwa katika vituo vyao. Utaratibu uliopo katika ugawaji wa dawa katika Vituo vya Afya ni kwamba, Bohari Kuu ya Dawa inakabidhi dawa na vifaa tiba katika vituo hivyo na wakati huo huo hukabidhi hati inayoonesha idadi na thamani halisi ya dawa na vifaa vilivyopelekwa katika kila kituo husika. Aidha, Mfamasia wa Wilaya nae huwa anapewa hati kama hizo zinazoonesha idadi na thamani halisi ya vituo vyote vilivyosambaziwa dawa na vifaa vya Wilaya yake.

Mhe. Naibu Spika, *structure* ya utendaji wa Wizara ya Afya ipo hadi ngazi ya Wilaya na kwa kuingia kwa ugatuzi imefikia hadi ngazi ya Halmashauri. Ahsante.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba majibu yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri na haya majibu niliyopewa mimi yanatofautiana sana. Sasa sijui nichukulie majibu yale au haya, naona kama kuna tatizo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe naomba ukae. Mhe. Machano Othman ni kweli na hata mimi nilikuwa tayari naanza kumuandikia Mhe. Waziri hapa, mbona yanatofauti majibu ambayo anayatoa Mhe. Naibu Waziri na majibu ambayo yameandikwa. Kwa utaratibu ambao tunaufuata ni kwamba majibu ambayo yatakuja kwenye meza ya Spika na ambayo atapewa Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali, lazima yaendane na majibu ambayo anayatoa Mhe. Waziri.

Sasa hilo nalikubali Mhe. Machano Othman ni kosa ambalo limefanyika na mimi nafikiria wizara itambuwe hivyo, kwamba kama kulikuwa kuna nyongeza yoyote basi ilikuwa ifike mapema hapa mezani pamoja na ambayo ameyajibu.

Mhe. Waziri sijui una maelezo kuhusu hilo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mimi ningeomba kidogo muongozo wako tu, kwa sababu nilivyozipitia mimi kanuni, sasa hivi siwezi kukinukuu kifungu. Kwamba kinachosemwa hapo ndicho kinachoingia katika Hansard *official record* hata katika kauli za serikali, serikali inaweza kuwasilisha kauli, lakini kauli itakayotamkwa pale na kuchukuliwa katika Ofisi ya *Hansard* ndio itakayoingia kwenye *record*.

Sasa utaratibu huu inawezekana wa kuwasilisha jibu mezani, jibu lile likaja mapema, lakini serikali ikafanya maamuzi kuwasilisha jibu ambalo Waziri au Naibu Waziri wake atatamka pale, ndio litakuwa jibu halisi ambalo litaingia katika *record* za *Hansard*. Sasa naomba Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taathima muongozo wa kiti chako *which prevail is it the Hansard* ndio ina *prevail* au maandishi yanawasilishwa. ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri utaratibu uliopo ni kwamba pale ambapo panatokea marekebisho au mabadiliko yoyote yanaletwa Barazani kabla ya siku ile au hata siku ile asubuhi. Lakini mimi ningeomba tu kwamba kwa sababu swali limeshajibiwa, Mhe. Mjumbe nilimpa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Sasa swali ni la Mhe. Machano Othman Said, kwa hivyo nampa fursa yeye mwenyewe atake majibu kama kuna majibu ya ziada kutokana na hayo ambayo yameulizwa hajatosheka, basi ayapate majibu hayo, nafikiri hiyo ndio fatwa yangu.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa maelezo yako, na ni vizuri Waheshimiwa Mawaziri wafuate taratibu, kwa sababu yale ya kuchomekea yote yanakuwa sio sahihi. Haya aliyoniletea ningeridhika nayo sana kwamba ndio hali halisi ilivyo. Pamoja na hayo naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara imekiri katika haya yangu kwamba hawajatembelea kutokana na wingi wa vituo, na kwa kuwa Mhe. Waziri ameshaniahidi mara mbili na kuwaarifu watu kwamba atakuja na akaahirisha.

(a) Je, ni lini tunatarajia kwenda kuvitembelea vituo vyetu hivi.

(b) Jimbo la Mfenesini lina kituo cha Chuini, Mfenesini, Bubwisudi na Mwachealale, lakini hiki kituo cha Mwachealale bado hakijakuwa na uhakika kama kipo au hakipo. Nilitaka kujua serikali inasemaje kuhusu Kituo cha Mwachealale kipo au hakipo. Lakini pia malipo ya umeme na walinzi wa vituo hivi nani anawajibika kulipa?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ziara kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba zitaendelea katika vile vituao ambavyo hatujawahi kuvifikia. Lakini Waheshimiwa Wajumbe naomba mkumbuke kwamba sasa hivi tumo katika ugatuzi, kwa hivyo kuna wizara maalum ambayo itakuwa inazunguka zaidi katika vituo vya afya tofauti na

mlivyozowea. Kwa kushauriana na kukubaliana na wizara hizo na hasa kwa sababu Wizara ya Afya bado tupo katika kushughulikia vituo vile kwa baadhi ya sehemu, basi tunakuahidi kwamba Mhe. Waziri atapanga ziara maalum ya kutembelea vituo vya afya kwa mashirikiano na wizara inayohusika.

Mhe. Naibu Spika, kituo cha Mwachealale vile vile napenda nimueleze Mheshimiwa kwamba kutokana na kuingia katika ugatuzi vituo vyote vya afya vimekabidhiwa kwa Wizara inayohusika ya Tawala za Mikoa, kwa hivyo shughuli zote ambazo zinahusu vituo hivi na nyote ni mashahidi kwamba hata bajeti ya vituo hivi imekwenda katika Wizara ya Tawala za Mikoa. Tutashauriana tutakaa tutapanga pamoja na Wizara hii husika ili tuone tutashirikiana vipi lakini Waheshimiwa pamoja na wananchi waliomo katika vituo hivyo waweze kuridhika na huduma zinazotolewa katika vituo hivyo.

Mhe. Machano Othman Said: Hakumalizia jibu nilizungumzia malipo ya walinzi na umeme nani anawajibika kulipa Serikali au wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kuhusu bili za umeme kwa sasa anayehusika kulipa na bili hizo ni Ofisi ya Tawala za Mikoa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuniona nimesimama muda mrefu lakini bahati yangu ikawa nzuri kwako.

a) Naibu Waziri safari ya kwenda Mfenesini ni mbali sana je, yeye Mhe. Naibu Waziri katika hospitali hii ya Mnazimmoja Hospitali tegemezi mmefanya ziara siku ngapi na mmebaini nini katika hospitali ile mtueleze matatizo yaliyokuwepo pale kama ziara, kwenda Mfenesini ni safari kubwa lakini Hospitali ya Mnazi Mmoja ofisi ipo pale mnatembelea kwa muda gani na matatizo gani mliyoyaona.

b) Kuna dawa ya *tetanus* imekuwa kitandawili kikubwa katika Hospitali ya rufaa ulitaja suala la madawa, mmejipangaje hasa kwa mnyonge akishindwa kudhibiti shilingi elfu tano au saba kwenda kununua dawa ya *tetanus* anakwenda kufukuzia hospitali ya rufaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Namuomba sana Mhe. Jaku arudie suali la pili.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku rudia lakini kwa ufupi sana uliulize upya kwa sababu suala lake lina (a) na (b) sasa naomba uyafupishe sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa muongozo wako Mhe. Naibu Waziri kwenda kutembea Jimbo la Mfenesini kwa Mhe. Machano ni mbali kutokana na Wizara yako ilipo, nilikuwa nataka kujua kama wewe Naibu Waziri na Waziri Ofisi zenu haziko mbali na hospitali ya Mnazi Mmoja ziara hizi mnafanya nini, au mmetembea gani na mumeona matatizo gani katika hospitali ile kama mmefanya ziara kweli mtueleze matatizo mliyoyaona, maana yake nashuhudia wakati mwengine hata balbu mle njiani hamna.

Mhe. Naibu Spika: Nimekwambia kwa ufupi ameshafahamu na hilo la (b).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, la pili kuna dawa ya *tetanus* imekuwa usumbufu katika hospitali ya Mnazi Mmoja alitaja mambo ya madawa na kimbilio lile mtu anatoka shamba ameshapanda gari….

Mhe. Naibu Spika: Suala unaulizia *tetanus* kwa nini haipatikani Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mheshimiwa Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, mimi na Mheshimiwa Waziri hospitali ya Mnazi Mmoja ni nyumbani kwetu kwa hivyo hatumalizi siku kama hatujapita mara moja au mara mbili katika hospitali ya hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini kama hilo halitoshi hata usiku tunatega muda wetu kwa kuzunguka katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuona utendaji wa kazi wa wafanyakazi pamoja na huduma wanazozipata wagonjwa wetu.

Mhe. Naibu Spika, changamoto ambazo tunazibaini wakati tukitembea katika Hospitali ile ambayo ni sawa na nyumba yetu kwa maisha yetu tulivyoyaweka, kwanza ni changamoto ya uhaba wa wafanyakazi ambalo hili ni tatizo hata nyote mnalijua na tunawashukuru mnatusaidia kulitatua na linatatuka taratibu.

Lakini pia changamoto ya wagonjwa na *relative* kuingia bila ya utaratibu au kugombana gombana na walinzi jambo ambalo tulishaliweka sawa na hivi sasa liko vizuri halikai. Mhe. Naibu Spika, Mnazi Mmoja nyote ni mashahidi kuna changamoto nyingi naomba nizitaje hizo chache ili mridhike.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ukosefu au upungufu wa dawa ya *tetanus* katika Hospitali ya Mnazimmoja dawa hii siwezi kukujibu kikamilifu kwamba haipo au iko, kwa sababu dawa zinakuwepo zinapoingizwa baadae zinapungua zinapotumiwa na zinakwisha kabisa zinapotumiwa zaidi na baadae zinaingizwa tena kwa hivyo siwezi kukupa jibu moja kwa moja kwamba sasa hivi au wakati huo ulipokwenda zilikuwa hazipo kabisa. Lakini mpango weu wa dawa zinaingizwa zinatumiwa kama kawaida zinapungua hadi zinaisha na kuongezwa hadi kukamilika. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wa Maswali na Majibu umemalizika na mimi nimeongeza dakika nyengine 15 kwa hivyo tumebakiza masuala matatu ambayo yapo kwenye *Order Paper* yetu na yalitakiwa leo yajibiwe, lakini kwa bahati mbaya na sisi kwa kuwa kuna masuala mengi na tuna miongozo mingi na Waheshimiwa Mawaziri wanajitahidi kujibu vizuri kwa hivyo muda wetu unakuwa haututoshi.

Kwa hivyo ningewaomba wale ambao walikuwa masuala yao yapo katika *Order Paper* watuombe radhi kwa leo tuendelee na shughuli nyengine na masuala yao yataingia katika *Order Paper* za siku nyengine.

Utaratibu

Mhe. Machano Othman Said: Nimesimama hapa kanuni 63 lakini nalenga kanuni 37 naomba ninukuu kanuni namba 37.

Mhe. Naibu Spika, kanuni namba 37 inasema Waziri au Mjumbe yoyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi. Sasa wakati wa masuala na majibu swali No. 12 ambalo liko ukurasa wa tatu katika *Order Paper* ya leo la Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Aliulizwa swali kuhusu vijana waliopewa mikopo katika majibu yake alisema kwa Unaguja vijana 140,000/= kwa mwaka 2016/17 kidogo nina hofu sana na *Hansard* hii na uhalisia wa hii idadi ya vijana 140,000/=.

Sasa nilikuwa naomba pengine kwa kupitia kiti chako Mhe. Waziri atuletee majibu yenye mchanganuo Mkoa kwa Mkoa na fedha zilizotumika ili kujua idadi halisi ni hayo tu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Machano nadhani Mheshimiwa amepokea ni swali ambalo kwa sababu umelileta kwangu mimi namtaka Mhe. Waziri alete mchanganuo ambao vijana hawa ambao wamekopa katika kipindi hicho ambacho kimetajwa.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na kuweka Mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Taifa la Biashara la Zanzibar liliundwa mwaka 2005 chini ya hati ya Kisheria No. 45 ya mwaka 2005 na kufanyiwa marekebisho hati ya Kisheria No. 35 na Na. 44 ya mwaka 2007 na 2009. Muundo wa Baraza hilo ilikuwa inajumuisha Mwenyekiti ambae ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na wajumbe 24. Kwa upande wa uendeshaji Baraza lilikuwa linasimamiwa na Kamati Tendaji chini ya Mwenyekiti wake ambae ni Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Katibu Mtendaji wa Baraza.

Mhe. Naibu Spika, Serikali imefikia maamuzi ya kufanya mabadiliko ya hati ya kisheria ya Baraza la Taifa la Biashara kwa kuanzisha sheria kamili ya Baraza la Taifa la Biashara ili kuendeleza na kutanua wigo wa shughuli za Baraza la Taifa la Biashara pamoja na kurahisisha utendaji kazi na utekelezaji wa maazimio ya Baraza. Sheria hii itasaidia kuweka mfumo wa kulifanya Baraza la Biashara kuweza kufanya kazi zote kuanzia taifa hadi kwenye Mikoa. Mbali na hilo Sheria itampa mamlaka Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuweza kuteua Katibu Mtendaji wa Baraza ambae atakuwa anafanya kazi za kila siku za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, kazi ya Sheria ya Baraza hili kutokana na mfumo mpya itakuwa kwanza kuwepo kwa mfumo wa kisheria unaoanzisha Baraza la Taifa la Biashara. Pili kuwepo kwa kamati za Baraza la Biashara na kupewa majukumu ya kusimamia utekelezaji wa maagizo ya Baraza pamoja na mambo mbali mbali yanayoibuka katika sekta husika. Tatu kuanzishwa kwa Mabaraza ya Mikoa ambayo yatasaidia kujadili na kutatua kero zinazoikabili Sekta ya Biashara katika ngazi ya mikoa. Nne kuanzishwa kwa Mabaraza ya Mikoa kutapelekea kutekeleza sera ya Serikali ya ugatuzi kwa madaraka.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kutungwa kwa sheria inayoanzisha Baraza la Taifa la Biashara la Zanzibar *ZNBC* kutawezesha kuwepo jukwaa la majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ambayo itapelekea wafanyabiashara kuelezea na kuwasilisha maendeleo, matatizo, changamoto inayoikabili sekta ya biashara, kilimo Utalii na uchumi kwa ujumla. Jukwaa hilo la majadiliano litasaidia kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kukuza uchumi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wachangie Mswada huu na baadae wapitishe kwa ajili ya kuwa sheria kamilifu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Kny. Menyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, muumba wa viumbe vyote mbinguni na ardhini kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima wa afya ili tuweze kutekeleza majukumu yetu katika Baraza letu tukufu. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako kwa niaba ya Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo, ili niwasilishe maoni ya Kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mheshimiwa, Balozi Amina Salum Ali pamoja na timu yake ya watalaamu kwa mashirikiano yao ya dhati waliyotupatia Kamati yangu katika kipindi chote cha majadiliano yanayohudu Mswada huu. Aidha, napenda pia kuwashukuru Wanasheria wa Ofisi ya Baraza letu hili la Wawakilishi pamoja na wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa uchambuzi na ufafanuzi wa kina wa hoja mbali mbali zilizokuwa zimejitokeza.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa umakini na ushirikiano wao waliouonesha katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua kwa majina yao:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi — Mwenyekiti

2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Mohammed Mgaza Jecha	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
5.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	Mjumbe
6.	Mhe. Ussi Yahya Haji	Mjumbe
7.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Mjumbe.

Mhe. Naibu Spika, Katika upitiaji na uchambuaji wa Mswada huu, Kamati yangu pia imeendelea kufanyakazi na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kutekeleza majukumu yetu ipasavyo, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina:

1.	Ndugu Asma Ali Kassim	Katibu
2.	Ndugu Said Khamis Ramadhan	Katibu

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, Kamati yangu imefanya kazi kwa kuzingatia Kanuni ya 83(6) ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016 ambayo imetoa uwezo kwa Kamati yangu kuwa na fursa ya kuwaalika Wadau kutoka sekta mbali mbali zikiwemo Jumuiya ya Wafanyabiashara, Viwanda na Wakulima Zanzibar *(Zanzibar National Chamber of Commerce, Industries and Agriculture)*, Chuo Kikuu cha Zanzibar *Tunguu (Zanzibar University)* na Asasi za Kiraia (Angoza) kwa lengo la kuwasilisha maoni yao kuhusiana na mswada huu. Hivyo, kwa kutambua michango yao waliyoitoa mbele ya Kamati, napenda kuwashukuru wadau hao kwa maoni na ushauri mzuri ulioiwezesha Kamati kuwa na muono mpana wa ufahamu wa Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaunga mkono kwa asilimia mia uamuzi wa Serikali yetu wa kuleta Mswada huu pamoja na kwamba umechelewa kidogo kuletwa Barazani kutokana na umuhimu wake lakini haujachelewa sana. Ni matumaini ya Kamati, Serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Wafanyabiashara watatetekeleza vyema masharti yote ya vifungu vilivyomo ndani ya Sheria itakayopitishwa ili Wafanyabiashara wetu waweze kupata fursa kisheria ya kukutana na Serikali yao kubadilishana mawazo na kuibua maazimio yatakayorahisisha uendeshaji wa biashara Visiwani mwetu kwa maslahi ya pande zote mbili.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu umekusudia kulifuta Tangazo la Kisheria Namba 106 ya mwaka 2011 ambayo ndio iliyokuwa ikitoa uhalali wa kufanyika kwa Jukwaa la Kibiashara Zanzibar na kuanzisha Sheria mpya itakayotoa uwezo wa kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Biashara - Zanzibar *(ZNBC)* ambalo pamoja na mambo mengine litakuwa na wajibu wa kuratibu Jukwaa la mazungumzo ya kibiashara baina ya sekta za umma na sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, wakati wa kupitia na kujadili Mswada huu. Kiujumla, Kamati yangu iliafikiana na baadhi ya vifungu vilivyomo katika Mswada huo kwa vile ilikuwa na uelewa mmoja na mtazamo wa Wizara lakini kuna baadhi ya vifungu Kamati imeshauri vifanyiwe marekebisho ili kuimarisha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Miongoni mwa vifungu ambavyo Kamati yangu imeshauri Wataalamu wetu waifanyie marekebisho ni pamoja na kifungu cha 20(3) cha Mswada kinachoeleza Katibu Mtendaji atakuwa ni Katibu wa Kamati zote zilizoanzishwa katika Mswada huo. Kamati inasisitiza Kifungu hichi kifanyiwe marekebisho kuepusha kukwama kwa baadhi ya vikao iwapo kutatokea vikao viwili au zaidi kufanyika kwa wakati mmoja. Kutofanyiwa marekebisho kifungu hicho kutasababisha kuzorotesha ufanisi wa kazi za Kamati au Baraza. Kamati inapendekeza kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo:

“Katibu wa Kamati atakuwa ni Katibu Mtendaji au Mtu yeyote atakaeteuliwa na Katibu Mtendaji.”

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu pia imeshauri kuongezwe kifungu chengine cha 20(6) kitakachoelezea muda wa kutumikia nafasi kwa Wajumbe wanaotoka katika Sekta binafsi kwani Kamati imeona si busara wajumbe hao waingie katika Kamati Tendaji bila ya kuwepo ukomo wa muda wa miaka mitano kwani kunaweza kupunguza ufanisi wa Kamati hiyo. Hivyo, Kamati imependekeza kifungu kidogo hicho kisomeke kama ifuatavyo:

> “Ukitoa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Wajumbe kutoka sekta binafsi watashikilia nafasi kwa kipindi cha miaka mitano (5) na watakuwa na sifa ya kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja”.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu pia imependekeza kufanyiwa marekebisho Jadweli la Tatu, Aya ya 1(a), 1(b) na 1(d) kwa kuwaingiza Wajumbe wataalamu kutoka katika Taasisi za elimu ziliopo Zanzibar. Kwa upande wa aya ya 1(a) ya Jadweli la Tatu, Kamati imependekeza kuongezwe Mjumbe mmoja kutoka sekta ya kitaalamu ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar *(SUZA)* kupitia Taasisi inayohusika na Utawala wa Fedha - Chwaka *(ZIFA)* atakaeisaidia Kamati ya Uchumi, Biashara, Uwekezaji na Kodi kwa kuipatia ushauri wa kitaalamu na sio kuacha nafasi kwamba mjumbe huyo awe anaalikwa na Kamati ikitokea haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, katika aya ya 1(d) ya Jadweli la Tatu, Kamati imependekeza awepo mtaalamu kutoka sekta ya kitaalamu ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kupitia Taasisi inayohusika na Utalii - Maruhubi ambaye ataisaidia Kamati ya Utalii kitaalamu. Kadhalika, kifungu cha 1(d) kimependekezwa kifanyiwe marekebisho kwa kumuingiza mjumbe kutoka sekta ya kitaalamu ya Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) atakaeisaidia kitaalamu Kamati inayohusiana na masuala ya ajira kwa mambo ya ajira za wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu pia, imependekeza kufutwa kwa baadhi ya vifungu vidogo vya Mswada huo kwa kuwa vifungu hivyo vimeonekana kujirejea. Baadhi ya vifungu vyenyewe ni kifungu cha 12(3) cha Mswada ambacho kimejirejea na kuwa sawa

sawa na kifungu cha 11(3). Aidha, Kifungu cha 25(2) nacho kimependekezwa kifutwe kwani maelezo yake tayari yameshaelezwa na sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati yangu ni kuweka usawa wa tafsiri ya maneno yaliyomo katika Mswada wa Kiswahili na ule wa Mswada wa Kiingereza ili Miswada hiyo iweze kwenda sambaba kimaana na kuepusha kuwepo utofauti hasa baada ya kupitishwa Mswada huu na Baraza lako Tukufu. Miongoni mwa vifungu vilivyobainika kuwa na marekebisho hayo ni kifungu cha 15(1)(a) cha Mswada ambapo maneno "wa Kamati Tendaji" yaongezwe mwishoni mwa kifungu hicho. Aidha, katika cha 27(1) cha Mswada maneno ya pembeni ya kifungu hicho, yanapendekezwa yasomeke "Hesabu na Ukaguzi."

Mhe. Naibu Spika, mbali na hayo, kamati yangu imelijadili jina la Mswada huu na kupendekeza lifanyiwe marekebisho kwa kuingiza neno "Zanzibar" ili liweze kuendana na jina ambalo limo katika Mswada wa Kiingereza kwani katika kifungu cha 1 cha Mswada wa Kiingereza, jina la Mswada huo linasomeka "…… *Zanzibar National Business Council Act* ….." wakati katika Mswada wa Kiswahili jina hilo linasomeka "… Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara..." pasi na kuwemo neno "Zanzibar".

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Kamati yangu imependekeza kuandikwa upya baadhi ya vifungu kwa kuwa havileti tafsiri iliyo sahihi kulingana na maana halisi iliyokusudiwa. Mfano wa vifungu hivyo ni kifungu cha 1(2) cha Jadweli la Kwanza la Mswada ambacho kimependekezwa kifanyiwe marekebisho kwa kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo:

"Akidi ya vikao vya Baraza itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wa Baraza na miongoni mwa wajumbe waliohudhuria, kila upande baina ya sekta ya umma na sekta binafsi utapaswa kuwakilishwa na angalau asilimia arubaini (40%) ya wajumbe waliohudhuria."

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu pia imependekeza kanuni itakayotungwa kutokana na sheria hii ieleze wazi wajibu wa Sekta Binafsi wa kuchangia Jukwaa la Biashara kwani kwa kutegemea serikali peke yake ndio ichangie, kuna uwezekano wa kushindwa kufanyika kwa Jukwaa hilo kila mwaka. Zaidi ya hayo, Kamati imeshauri kufanyiwe marekebisho makosa ya kiuchapaji na kisarufi kwa lengo la kuweka bayana maneno yaliyokosewa ambayo yametumika katika Mswada huo.

Mhe. Naibu Spika, haya ni baadhi tu ya marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati yangu, Marekebisho ya ziada yapo kwenye Waraka wa Kamati unaohusu Mapendekezo ya marekebisho ya Mswada huo *(Bill Digest)* ambao natumai Waheshimiwa Wajumbe wote mmepatiwa.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inawasisitiza Wafanyabiashara wetu kuandaa utaratibu mzuri wa kuchangia gharama za kufanyika kwa Jukwaa la Biashara kwa maslahi ya

Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. Hili likiwezekana litawasaidia Wafanyabiashara kupata fursa ya kuwasilisha maoni na mapendekezo yao kwa kufanyiwa kazi. Aidha, Serikali nayo itaweza kutafuta njia muafaka kuzishughulikia changamoto zinazokwaza maendeleo ya biashara nchini.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu basi kwa umakini mkubwa waujadili, Mswada uliopo mbele yetu na hatimaye waupitishe kwa kauli moja Mswada huu kutokana na umuhimu wake ili Sekta binafsi ya wafanyabiashara wetu iweze kupata fursa ya kukutana na Sekta ya Umma kisheria na kuweza kuibua maazimio yatakayokuwa na maslahi kwa pande zote mbili.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha,

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati. Waheshimiwa Wajumbe tunaanza na wachangiaji, nina wachangiaji saba na matarajio yangu kwamba kama watamaliza wote kwa wakati Sheria hii tunaweza tukaipitisha leo hivi asubuhi. Sasa nilikuwa naomba sana nikiangalia idadi ya Wajumbe waliokuwepo hapa haitoshi kabisa kuja kupitisha vifungu vya sheria hii.

Ningeomba sana kwa sababu tunalizungumza suala hili mara nyingi sana kwenye vikao vyetu. Suala la kuwacha shughuli za Baraza tukaenda sehemu nyengine ni wachache ambao wameniletea hapa barua za kusema kwamba wanaondoka wana dharura, wengine sijapata dharura zao. Ningeomba sana Waheshimiwa mliokuwepo mbakie ili tuweze kuendelea na shughuli zetu. Ahsante sana. Sasa nitamwita Mhe. Ali Suleiman Ali, baada ya hapo atakuja Mhe. Simai Mohammed Said, anafuata Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama katika Baraza hili na kuchangia Mswada wa Sheria kwa Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na kuweka mambo mengine yanayostahiki.

Pili Mheshimiwa nakupongeza kwa dhati kwa kunipa nafasi hii na nampongeza Mhe. Waziri na nampongeza Katibu Mkuu mpya ndugu Juma Ali Juma na Naibu wake ndugu Ali Khamis na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa sababu tunaamini kwamba wizara hii ndiyo Wizara mama ambayo tunaitegemea kwa hali na mali.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika mchango wangu nitakuwa na mambo machache ambayo lakini nategemea kwamba yatazaa mambo mengi kwa kuendeleza Mswada huu na kuanzisha hili Baraza la Taifa la Biashara. Tunaamini kwamba chombo chochote kikiundiwa Sheria huwa kinafaida na mara nyingi na faida ile inaleta manufaa kwa wananchi wake. Kwa hivyo niipongeze Wizara kwa kuliona hili na kuna haja na wakati umefika kwa kulianzisha shirika hili.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar lina umuhimu wake kwa aina mbali mbali na hasa tukizingatia kwamba biashara za Zanzibar zipo sehemu mbali mbali, kuna biashara za kilimo, biashara za uvuvi, biashara za ufugaji, biashara ya utalii,

chakula na mambo mengine mengi ambayo yote yanaleta faida katika nchi yetu na wananchi wanafaidika. Kwa hivyo mimi nitakuwa na ushauri tu au kuuliza maswali baadhi ya maeneo nitamuomba sana Mhe. Waziri aje anipe majibu.

Mhe. Naibu Spika, katika Sehemu ya Pili ya Uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar kifungu cha 7(1). Baraza litajumuisha Wajumbe wafuatao, Rais ambaye atakuwa ni Mwenyekiti, Mawaziri kutoka Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama wajumbe, na wajumbe 10 ama zaidi ya 10 vyovyote itakavyokuwa katika marekebisho. Katika marekebisho nafikiri wasiopungua watakuwa ni wajumbe na wengine ambao wataingia. Mimi nataka kuuliza hapa tu kidogo Mheshimiwa akija anipe jibu.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi ndio Mwenyekiti wa Baraza hili la Taifa lakini je, kama patatokea matatizo au masuala mengine ya kitaifa au ya kikazi panaendeshwa mkutano Mhe. Rais hayupo nani atakuwa msaidizi wake. Kwa sababu hili jambo ni muhimu kufikiriwa, Rais ni binaadamu Rais anaweza kupata shughuli yoyote ya kitaifa au nyengine atakuwa hayupo na huku Baraza limeitishwa nani atakaeshika wadhifa huo wakati Mhe. Rais hayupo.

Lakini jengine Mheshimiwa ambalo nimeliona zuri ingawa yote mazuri lakini kuna kuzidiana katika uzuri. Katika muundo wa Wajumbe wa Kamati ya Baraza kuna makundi mbali mbali, hiyo ni 121, Muundo wa Wajumbe wa Kamati itakuwa kama ifuatavyo. Kamati ya Uchumi Biashara, Uwekezaji na Kodi, Waziri Mwenye dhamana na Biashara ambaye ni Mwenyekiti, Mawaziri wengine wanaofuatia sina matatizo nalo.

Ukurasa wa 122(c) kuna Kamati ya Kilimo na Ufugaji na Uvuvi, Waziri wa Kilimo ambaye ni Mwenyekiti, Waziri wa Biashara, Waziri wa Ardhi, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Mjumbe kutoka Jumuia ya Wakulima wa Karafuu, Mjumbe kutoka Jumuia ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima, Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Mjumbe kutoka Chama cha Wakulima, Mjumbe kutoka Chama cha Wakulima wa matunda na mboga mboga Zanzibar na kadhalika. Mjumbe kutoka Chama cha Wafugaji Zanzibar naomba kiongezwe kifungu kifuatacho.

Zanzibar tumezunguukwa na bahari kwa asilimia kubwa asili yetu ni wavuvi. Ningemuomba sana Mhe. Waziri kama kuna jina lingetumika Mjumbe kutoka chama au jumuia ya wavuvi, hiki namuomba sana kiwekwe ili kuweka usawa. Ukiangalia ufugaji Zanzibar hatuna wafugaji wengi kuliko wavuvi. Wavuvi wanatuletea tija kubwa, kwa sababu kila mwananchi wa Zanzibar anategemea mvuvi kupata mahitaji yake ya kitoweo hata katika mahoteli yetu. Sipingi wafugaji, wafugaji wapo wengine lakini wavuvi wametuzidi zaidi na ndio waliotuzunguka katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri hilo alione.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika makundi haya yote kuna kundi kidogo limenishughulisha hapa katika huu muundo yaani 121 kifungu 5(viii), kinasema kwamba Kamati ya Uchumi, Biashara, Uwekezaji na kodi, namba (1) Waziri mwenye dhamana na biashara ambaye ni Mwenyekiti Waziri wa Fedha, Waziri wa Ardhi, Waziri kutoka Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Katibu Mkuu kutoka Wizara ya Biashara, Katibu

Mkuu kutoka Wizara ya Fedha, Rais kutoka Jumuia ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima, Mwenyekiti wa Makampuni ya Bakharesa.

Mhe. Naibu Spika, hapa nataka kuuliza, hapa anaingia Mwenyekiti au inaingia Kampuni ya Bakharesa, kwa sababu Mwenyekiti ni Mwenyekiti, lakini Kampuni ina watu wengi siku nyengine yeye anaweza akawa hayupo. Hapa nataka nipewe maelekezo yaani kifungu cha nane ya kirumi. Mwenyekiti wa Makampuni ya Bakharesa na yeye ni Mjumbe, Mwenyekiti anaweza akawa hayupo siku nyengine anatakiwa muhimu lakini ana wajumbe wake hapa itakuwaje.

Mhe. Naibu Spika, Katibu Mtendaji kutoka Tume ya Mipango sina tatizo, Mkurugenzi Mtendaji kutoka Mamlaka ya Uwekezaji sina tatizo, Kamishna wa Mamlaka ya Kodi sina matatizo, Kamishna wa Bodi ya Mapato ya Zanzibar, Mjumbe kutoka Jumuiya ya Usafirishaji na Utoaji Mizigo sina matatizo. Naomba sana Mheshimiwa hapa tunaweka sheria na sheria ni mzunguuko, unapomuweka mtu yaani Mwenyekiti ni mwenye mali lakini ile ni Kampuni anaweza kuwa hayupo. Je, wakati huo Mwenyekiti wa Kampuni ya Bakharesa atakuwa nani. Naomba sana hili tuliangalie kwa faida ya Kamati yetu hii ili ifanye kazi zake vizuri. Naona bora iwekwe kampuni kwa sababu anaweza akateuliwa yeyote ikiwa fulani, fulani kwa utaratibu unaofaa.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa ujumla niseme tu kwamba sheria hii nimeiyona nzuri na inafaa na kufaa kwake ni kuleta maendeleo katika nchi yetu. Chombo chochote kinachoundwa narudia tena kina faida katika nchi na nimefurahi zaidi Mhe. Rais ndiyo Mwenyekiti, wa Kamati yetu hii atakuwa na uwezo wa kukutana na wafanyabiashara mbali mbali, atapata faida kubwa ya kuzungumza na wafanyabiashara yaani Baraza letu hili. Lakini niwaombe sana wasaidizi wake wote waliokuwemo tumpe msaada wa kila hali Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais ana mambo mengi lakini anayeteuliwa ni msaidizi wake, kwa hivyo niwaombe wote waliokuwemo katika Mswada huu tushirikiane na yeye mwenzetu Mwenyekiti wetu huyu ili aweze kufanya kazi zake vizuri ili kuweza kuleta faida katika maendeleo ya nchi yetu.

Jambo zuri sana kuwa karibu na wafanyabiashara, kuwa karibu na wafanyabiashara ni suluhisho la kuondoa matatizo katika maendeleo ya nchi. Wafanyabiashara wana malalamiko au maelekezo yao, lakini malalamiko nafikiri kama yanakwenda vizuri hakuna malalamiko watakuwa na ushauri mzuri kuishauri serikali na Wizara. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara kwa uzoefu wake na umakini wake. Tunashuhudia na nampongeza kwa dhati kabisa kwa sababu Mhe. Waziri hatakiwi kuwepo ofisini kila wakati, Mhe. Waziri atoke katika mahitaji ya wananchi wanataka nini na na faida gani inapatikana.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano tumeshuhudia zao la karafuu nchini ni uti wa mgongo katika nchi yetu. Hivi sasa Mhe. Waziri akikaa siku mbili Unguja siku ya tatu yupo Pemba. Mimi nampongeza kwa dhati kwa hili na kuhakikisha kwamba uchumi wetu huu unapatikana kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Aidha kuhakikisha hili tukiri kwamba penye uchumi pana matatizo yanajitokeza, baadhi ya matatizo ambayo hatua anazozichukua kufika haraka na kulitanzua pia linatusaidia. Navipongeza vikosi vyetu vyote, vyombo vya dola vyote kwa kushirikiana na serikali katika kuhakikisha kwamba zao letu hili la uchumi wa karafuu haupotei. Ukisikiliza mawio, utasikia leo KMKM wamekamata makundi fulani.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri kwa pongezi hizo azidishe bidii yeye na watendaji wake na nikiri kwamba haya nitakayosema sisemi kwa ubaya nasema kwa wema kabisa, hata ndugu Juma Ali Juma Katibu Mkuu ni mtu mzuri sana, ni mtendaji mzuri anayejituma bila ya kujali mvua na jua, kwa hivyo tumtumie sana ndugu yetu huyu kuhakikisha Wizara ya Biashara inakuwa vizuri na inaendelea vizuri. Mimi nimpe faida hiyo, yeye anamjua na sisi sote tunamjue ni mzuri na nampongeza na namtakia heri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kwa heshima kabisa niseme tu kwamba mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu walionileta hapa Mswada huu naukubali kwa asilimia 100 na naomba wenzangu wauchangie tuuweke vizuri ili ulete faida katika nchi yetu. Ahsante.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwneyezi Mungu na kuipongeza Kamati pia kwa kazi nzuri waliyoifanya lakini pia nimpongeze Waziri mwenye dhamana kwa kuleta Mswada huu ambao ni muhimu kwa nchi kwa wafanyabiashara. Pia kuleta umoja na mahusiano ya karibu sana baina ya Sekta ya Umma na Sekba binafsi kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu na biashara katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na taifa letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa jimbo la Tunguu kwa kuniteuwa wao kuwepo hapa leo ili kuwa msemaji wao, mtetezi wao na niweze kutoa fikra na mawazo kwa kadri ninavyoamini na kuweza kuishauri serikali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo pia nichukue nafasi pia ya kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ziara yake aliyoifanya katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba hivi karibuni ambayo naamini pia inaleta muamko na itaweza kuleta tija na ufanisi katika kazi zetu za kila siku.

Sasa nianze kwenda moja kwa moja katika mchango wangu. Mhe. Naibu Spika, ukenda katika kifungu Nam. 3 kwenye sehemu ya kwanza ukiangalia neno maana ya Jumuia na ukenda kwenye tafsiri ya kiingereza huku inasema *Chamber means the National Chamber of Commerce, Industry and Agriculture* na ukienda katika Jumuiya tafsiri yake ni Jumuiya ya Wafanyabishara, Wenyeviwanda na Wakulima ni sahihi hili ndio jina uloliita lakini ndani ya sheria hii imetambua kutakuwepo na Jumuiya nyingi sasa, sasa mimi ningeshauri hapa Jumuiya ipate tafsiri yake na *Chamber* pia ipate tafsiri ambayo kama inaonekana kama ni *parent* ya Jumuiya ya hiyo *parent* inayotambulika ni kama Taasisi ambayo ni mama kwa niaba ya hawa wafanyabiashara.

Baada ya hapo nianze kwenye kifungu namba 7 kinaendelea Baraza litajumuisha na wajumbe wafuatao wametajwa wote A, B, C na D ambapo kuna Mhe. Rais, kuna

Mawaziri na Wajumbe kumi lakini pia *spirit* ya nchi yetu sasa hivi tunakwenda kwa kuwatambua Wazanzibari ambao wanaishi katika nje ya nchi. Lakini pia sasa hivi tumeunda Taasisi pia inayotambulika ambayo iko chini Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambao hawa kwa sasa wana jina la umaarufu wao wanaitwa *Diaspora* hasa mimi ningeashauri D iongezeke iwe kuna mjumbe mmoja wa *Diaspora* ambaye atakae chaguliwa na Waziri au Wizara mwenye dhamana inayosimimia kitengo hicho cha *Diaspora* kwa sababu hawa Jumuiya zao ziko nyingi kuna Jumuiya ziko ambazo katika nchi za Ulaya wengine wako Marekani na maeneo tofauti pamoja na Falme za Kiarabu.

Lakini pia imetambua kuweko Mweyekiti pale ambapo Mhe. Rais atapata dhamana basi na tunashauri aidha Waziri mwenye dhamana ya hii sheria au Wizara husika au Makamu wa Pili basi ataweza kukalia kile kiti ili kuendesha kikao, kwa sababu kwa mujibu wa sheria hapa naona kama imemtambua Rais ndiye atakuwa Mwenyekiti.

Lakini pia nashauri pia wanachama na Mkurugenzi huyo Mtendaji wa *ZNBC* au *Zanzibar National Business Council* ili kuleta umoja kwasababu kule kwetu Tanzania Bara wana *TNBC* halafu inatoka pia kuna *East African Business Council* halafu kuna *TPSF* ambayo ni *Tanzania Private Sector Foundation* hasa hawa wote kwa ujumla itakuwa ni vizuri pia kwamba wale ambao ni Wenyeviti na Wakurugenzi ambao wanatambulika katika zile Taasisi kulingana na Jamuhuri ya Muungano Tanzania, waingie katika zile Kamati ambazo wametambulika katika jadweli la pili, kama ilivyozungumza katika hii sheria ili tuweze kuleta umoja na yale ambayo sisi kwa upande wa *ZNBC* au kwa upande wa Zanzibar tumeazimia tunakuwa tunajenga umoja na wao pia kuyatambua hasa kwa upande wa Tanzania Bara.

Lakini ikiwezekana pia Mkurugenzi ambaye atasimamia *ZNBC* ambaye pia kwa hivi sasa Mwenyekiti wa *Zanzibar National Chamber of Commerce Industry and Agriculture* anakuwa ni Mjumbe katika *Tanzania National Business Council*, basi Mhe. Waziri apiganie na apeleke maombi yake kwa upande wa Zanzibar huyu Mkurugenzi Mtendaji kutoka *ZNBC* basi na yeye pia apate ujumbe asiingie katika *Steering Committee* aende katika ujumbe moja kwa moja wa *TNBC* pamoja na *East African Business Council*, ili *representation* ya Zanzibar iwe ni ya upana zaidi na ushiriki wake pia utambulike kisheria.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hili Baraza mimi mwenyewe niliwahi kuwa mjumbe wakati lilipoanzishwa na nitambue pia Waziri ambao wakati ule wakati Rais alikuwa Mhe. Rais Karume na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alikuwa pia Mhe. Haroun, Mhe. Dkt. Mwinyihaji, Mhe. Machano, Mhe. Hamza hawa wote walikuwa ni wajumbe wa lile Baraza na walipambana sana katika kushauri na kusaidia sisi ambao tunatoka katika jumuiya zile na moja ambalo tulikuja kulitambua kulikuwa na unageuka ni uwanja wa kupiga makelele na malalamiko na ukiangalia katika maazimio mengi yaliyotoka katika Baraza la Biashara mengi ambayo yalikuwa yakizungumzwa hadi leo hayajapatiwa ufumbuzi. Kwa mfano kero ya Wazanzibari kutaka kutambulika kuweza kusafiri na magari yao kwenda Tanzania Bara limeshazungumzwa miaka mingi, limeshazungumzwa Barazani bado linaendelea kuwa kero naamini kwa mujibu sasa katika sheria hii tunapoipitisha hapa na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu leo tutaipitisha, Waziri ahakikishe

katika yale yote ambayo yaliyokuwa nyuma yaliyoazimiwa pale waweze kuitwa wale Mawaziri husika ndani ya Jamhuri wahusike na wao katika siku mada zitapopangwa ili tuende kwa kazi pia na kuondoa hii kero ambayo imekuwa ya miaka mingi au zile zote ambazo zimezungumzwa kwa pamoja.

Lakini Mhe. Naibu Spika, ndani ya Baraza hili pia tunakuwa na malengo pia katika kuimarisha uchumi wetu na pia kuhakikisha kwamba tunapokea kodi. Nashauri pia wajumbe wote watakaotoka katika Sekta Binafsi wapatiwe mafunzo na kutambua Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu isiwe wanakuja na mawazo yao wanayoyataka wao peke wao lakini wasimamie pia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, waitambue inawezeka wao pia wana mrengo au mawazo na fikra wa vyama vyengine au pengine hawana chama cha siasa.

Lakini madhali Chama cha Mapinduzi ndio chama kilichopo madarakani ndiyo chama kinachooongoza sasa hivi ndiyo chama ambacho pia kitakuja kuongeza Serikali *Inshaallah* Mungu akijaalia 2020 - 2025, kwa hivyo tuwapatie mafunzo waitambue ilani yetu na wazidi kuielewa na hapa nataka niseme kitu muhimu.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi katika malazi ya mahoteli kuna tatizo moja limejitokeza na ningeshauri Waziri wa Biashara, Waziri wa Utalii na Waziri wa Fedha wasimamie kwa pamoja kuta kitu kinaitwa *Air B & B* vyumba ambavyo sasa vinakodishwa katika maeneo tofauti ndani ya Unguja na Pemba kupitia mtandao. Wageni wana *booking* katika mtandao wanalipa huko huko mtu anaingia ndani nyumbani kwa mtu anakodi chumba kimoja viwili analala na familia yake kimoja anaingia mtu ndani, sipingi Mzanzibari kuongeza kipato chake.

Lakini hapa tatizo kwa mfumo mzima wa Serikali kupoteza mapato yake ukiingia kwenye mtandao sasa hivi kwa upande wa Kaskazini na pamoja na Mkoa wa Mjini vitanda zaidi ya 2,000 vinakodisha majumbani na ukichukuwa kwa vitanda 2,000 ni sawa sawa na hoteli kubwa zaidi ya tatu, usalama pia wa wageni tunaweka njia juzi nimemkuta mgeni mtalii usiku anatembea peke yake saa sita amepotea, kalala katika *flat* za *BOT somewhere* maeneo ya Kiembesamaki, hajui wapi anapokwenda hasa usalama wake.

Mimi nashauri Waziri wa Biashara, pamoja na Waziri wa Utalii na Waziri wa Fedha walete mabadiliko ya sheria haraka sana katika kikao hichi ili tupige marufuku watu kutumia mtandao wa *Air B & B* na kutumia majumba yao kiraia kulaza wageni bila ya kupitia mfumo rasmi waliokuwa hawana leseni watu wanakuwa hawalipi kodi. Baada ya hapo nashauri pia katika mapendekezo yote yatakayotoka katika Baraza la Biashara basi yapelekwe pia katika Baraza Mapinduzi yafanyiwe kazi kutoka *Steering Committee* anayotoka pamoja na kwenye Baraza la *Council* lenyewe na mrejesho pia uletwe katika vikao vitakavyoeenda, lakini ukiangalia katika ukurasa jadweli namba la pili ambalo limetajwa juu ya hizi kamati.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia samahani jadweli la tatu kwenye namba 5 hapa inasema muundo wa kamati utakuwa ifuatavyo, kuna Kamati ya Uchumi, Biashara na Wawekezaji wa Kodi lakini ukuangalia humu ndani muundo tunaokwenda nao *speed* tunayokwenda nayo tukitambua kwamba utalii ni katika sehemu muhimu wana jumuiya

yao, mimi ningeshauri hapa pia Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii awe Mjumbe katika Kamati hii. Lakini pia ukienda kwenye B inasema wajumbe wa Kamati ya Utalii mimi nashauri hapa iwe Wajumbe wa Kamati ya Utalii na Mawasiliano kwa nini nasema hivyo.

Mhe. Naibu Spika, leo asubuhi nimeamka mimi nime-*sign* katika mfumo wa *google alerts* chochote kitanacho andikwa cha Zanzibar na duniani kokote nakikamata naangalia leo nakuta *Zanzibar Grapples to Protect Children from Sex Tourism*, yaani Wizara ya Kazi imeomba fedha inaelekea kutoka Umoja wa Mataifa kwa mpango wao juu ya udhalilishaji, lakini muandishi wa makala hii ambayo imetoka katika mtandao mkubwa sana wa masuala ya *Tourism* au Utalii na Usafiri inaitwa *interble* ameenda kuliungaunisha masuala ya udhalilishaji pamoja na biashara yetu na kama mtu hatakanusha hii linabaki katika mtandao na kila ukiandika inakuwepo inatutita jina baya. Sasa mimi nashauri hii kamati ambayo imetajwa hapa kisheria juu ya Kamati ya Utalii basi iongezwe Kamati ya Utalii na Mawasiliano ili tuweze sisi pia kufanya *Promotion* na *Marketing* na kunyanyua visiwa vyetu kiuchumi na kibiashara.

Lakini katika mambo kama haya tukiangalia yamekuwa yanatokea sana huko nyuma na tunachelewa kukanusha ikibakia, hizi taasisi za nje wanakuwa wanaamini. Sasa tuwe tunafanya mambo haya kwa haraka zaidi na katika Baraza la Biashara itakuwa ni sehemu moja kubwa sana ya kutusaidia, mimi nakumbuka huko nyuma tuliwahi kutoa taarifa katika mfumo mzima uliokuwepo katika kibanda ugali sehemu ya Kiwengwa.

Nampongeza sana aliyekuwa Rais mstaafu alikwenda alihakikisha kunasafishwa kote kule Kiwengwa palikuwa pamekaa vijumba uchafu mpaka maeneo ya maji yalikuwa yanaingiliwa na tungeweza hata kupata magonjwa haya ya *cholera* na mengineyo. Lakini namshukuru Mhe. Rais Karume aliweza kuhakikisha yale mambo yanaboreshwa na kero hizi zilipitia kutoka huko huko Baraza la Biashara.

Sasa nashauri pia katika hizi kamati wapatikane wataalamu wote kutoka Chuo cha SUZA walimu ambao ni *deans* katika Skuli zote kama mfano Skuli ya Biashara, Skuli ya Utalii, Skuli wanayotumia masuala ya fedha kutoka Chwaka basi watafutiwe njia hapa waingie waunganishwe kwa mfano *Vice Chancellor*.

Vice Chancellor angeweza kuingia katika Kamati ya masuala yanayohusiana na ajira na hapa katika hii D ningeshauri pia Jumuiya ya Uwekezaji Sekta ya Utalii pia wangeingia hapa tumeona karibuni jinsi suala la ajira baada aya Mhe. Waziri mwenye dhamana kutanganza tarehe 30 Juni juu ya kima cha chini cha mshahara na tumeona mtafaruku uliokuwepo hadi hivi sasa maeneo tofauti kwamba pia jinsi ya utekelezaji wake umekuwa ni mgumu. Sasa Baraza la Biashara ukisoma ile sehemu ya kazi zake ambazo imekusidia kwenye namba 4, Baraza la Taifa la Biashara lina malengo yafuatayo, kuandaa mikutano na majadiliano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi kwa dhamira aya kupata muwafaka na uwelewa juu ya mabo ya msingi yanayohusiana na usimamizi wa ukuaji wa uchumi.

Ukiangalia suala la *Minimum age* linavunja ile *spirit* baada aya Waziri kutangaza na jinsi utekelezaji wake ulivyokuja juu ya ile *Public Private Partnership* hata ukiangalia sasa

hivi kwa upande wa Sekta ya Umma kuna changamoto kubwa mimi nimekwenda uwanja wa Mao kuangalia jinsi vibarua wanavyolipwa mishahara wanapolipwa zile *daily workers pay* yao ya *skilled* na *unskilled.*

Uwanja wa Mao umejengwa kwa msaada wa Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa China juzi nimekwenda pale mtu ambaye anatakiwa alipwe Shs. 25,000/= analipwa shilingi 10,000, mtu ambaye anatakiwa alipwe Shs. 30,000/= analipwa Shs. 10,000/= yaani *daily worker unskilled* na *skilled* analipwa Shs. 10,000/=. Hii ni dhahiri kwamba changamoto iliyokuwepo katika Sekta Binafsi iko pia ndani ya Sekta ya Umma pia, kwa sababu Uwanja wa Mao unasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa msaada wa watu wa China, naamini pia sitaki kutaja maeneo mengine ambayo nayafatilia kuangalia na changamoto zilizokuwepo. Lakini hii tunajitia doa wenyewe kwa sababu tuna mahusiano mazuri na nchi kama hii lakini utekelezaji unakuta sasa bado. Mimi nashauri kwa *spirit* hiyo hiyo SMZ itafute njia mbadala kuhakikisha kwamba wao watafidia zile fedha ambazo wanazolipwa wale *daily workers* katika Uwanja wa Mao ili tusije tukapata malalamiko huko mbele.

Lakini ningemshauri Waziri pia kwamba tuna mpango wa kujenga *Terminal II* na tuna mawazo na ndoto kwamba tunamini hii itakuwa moja katika *Legals* ya Mhe. Rais fedha ambazo zilizotengwa za Uwanja wa *Airport Terminal II* ni US$ 58,000 kwa mkopo wa *Chinese Exim Bank* tuliopata. Sasa huu umepitishwa kabla hii kima cha chini hakijapitishwa, sasa tusije tukatoka sasa tukenda kuanza uwanja huu huku tukitambua utekelezaji wa hili suala la *daily pay* ya *skilled* na *unskilled* likawa changamoto *again* kwa kuwa sasa pana *delayed mechanism* tukachelewa mradi huu sasa kuchukuwa hatua nyengine.

Lakini pia barabara ambazo tumezitaja ndani ya ilani kwa mfano mimi jimboni kwangu barabara ya Tunguu kuja mpaka Fuoni ambazo pia zimetajwa lakini miradi hii yote ipo katika utekelezaji imeshapangwa na fedha yake tayari imeshatengwa. Lakini zinabidi *project* zote hizi zinagaliwe tena upya, barabara pia Malindi kwenda mpaka Kinazini kwenda zake mtoni mpaka Bububu ambazo ni kilimota 11.2 zimetajwa ndani ya ilani inabidi Waziri wa Fedha angalie utaratibu wa jinsi gani tutahakikisha kwamba hakuna malalamiko juu ya hivi vibarua katika ulipaji wa Shs. 25,000/= na Shs. 30,000/= tusije tukayachukua mambo yote kwenda kuyapeka katika Baraza la Biashara.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nataka nilizungumze pia juu ya nafasi ya Zanzibar na mwenendo tunavyotambulika katika nchi za kimataifa kwa jinsi gani tunavyoweza kufanya biashara katika Gazeti la Zanzibar Leo la Septemba tarehe 24.

Mhe. Naibu Spika kwenye ukurasa wa pili inamsema Waziri wa Fedha ambaye ni Mhe. Dkt. Khalid inasema mageuzi yanahitajika kwenye uwekezaji kwenye *paragraph* namba 3 nanukuu hili gazeti nasema:

> "Alibainisha kuwa suala la upatikanaji wa huduma za msingi kwa wawekezaji limekuwa likilalamikiwa sana na wawekezaji kutoka nje hali ambayo idadi ya Miradi inayoidhinishwa imeanza kupungua.

Hiki kima cha chini kilichotangazwa na Mhe. Waziri Mradi mmoja wa Fumba ambao Pemba umeshafutwa kwasababu Zanzibar itakuwa ghali sana kutumia vibarua katika ujenzi huwezi ukamlipa mtu kibarua Shs. 25,000/= na Shs. 30,000 tunakuwa katika visiwa ghali katika kujenga ndani ya bara la Afrika na chini katika pia na Bara Asia.

Kwa hiyo miradi yote midogo midogo na mikubwa sasa hivi kama utafanya *Feasibility Study* inabidi Mhe. Waziri uwangalie upya jinsi gani, ukienda katika nafasi katika gazeti hili ambalo ni la Serikali inatajwa Zanzibar alisema ripoti ya benki anamkariri hapa Mhe. Waziri wa Fedha:

> "Benki ya Dunia inasema *Doing Business* inaonesha Zanzibar inashika nafasi ya 155 katika nchi ya 189 zilizofanyiwa utafiti hali inaonesha kutofikiwa kasi ya ushindani hili ambalo la *Minimum Wage* kwa uwekezaji ambao ZIPA wanataka kujipanga *One Stock Centre* intakuwa ni mtihani".

Kwa hivyo Waziri wa Biashara angalie jambo dogo lakini linakuwa ni kubwa unaweza kuona kitu kidogo sasa hivi lakini athari zake ni mnyororo unakula kila pahala unakula kwenye wafanyakazi, unakula katika uwekezaji, unakula pia katika hadhi na sifa ambazo za kutangaza Zanzibar katika huo uchumi ambao tunaotaka kwenda nao. Ukiangalia huku inasema ZIPA imejipangia kusajili miradi ya wawekezaji ndani ya siku ishirini na moja ndani ya siku ishirini na moja lakini ukienda leo Rwanda ambao ni mfano katika nchi za Afrika Mashariki na Kati ndani ya masaa 24 ukitaka kuwapa leseni hapa Zanzibar unataka leseni hawa watu wa hoteli wana leseni ya watu wa utalii, wana leseni ukenda huku upande wa mila na sanaa, una leseni ya vileo, una leseni nyengine na Mhe. Waziri wa Kazi sasa anaanzisha leseni mpya. Kama wewe utakuwa na kiwango 300,000/= utakuwa leseni ya 300,000/= unatambulika au 180,000. *Duplication* ya leseni hata ukipeleka Baraka la Biashara tutakuwa tunapiga makelele mambo kama haya yanatakiwa yaondoke, yaondoke katika hadhi ambayo tumeyapanga si kuyatambua.

Kwa hivyo mimi nashauri haya makero ya lazima tuyaangalie sana huku tukijua kwamba hayatupeleki tunakwenda mbele tunarudi nyuma, tunakwenda mbele tunarudi nyuma, tunakwenda mbele tunakwenda nyuma. Wafanyabiashara kwa hali inavyojisikia huko nje wanajiona wao ni maadui hawapendwi kwa hivyo dhana ya wafanyabiashara ukienda mahala pengine wanaonekana wao ni wezi hawalipi kodi, lakini wao ndio wanao *create* ajira wao ndio wanaopanga mawazo na biashara zao kwenda kusaka na kuleta Zanzibar. Hili namkariri ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambaye alikuwa Mkurugenzi wa ZIPA alisema Wawekezaji wote wanapotaka kuja Zanzibar wanakuja kutokana na sifa zetu wenyewe wanapiga debe kuja huku.

Kwa sababu ukiangalia kwa Zanzibar fedha kutumia kwenda kutangaza Zanzibar ni kidogo hatutumii nyingi kwa hivyo sisi tujenge mazingira ya biashara na pawe na nia njema kabisa baina ya watendaji ndani ya Serikali na Sekta ya Umma ili ule umoja na dhamira hii sheria iwe tunakwenda nao sambamba.

Mheshimiwa mimi baada ya hapo nitakuwa sina mengi niseme tu nikazie tu suala la *Air B & B* nililolizungumza kwamba Serikali inakosa mapato nalitilia mkazo sana katika Kikao hiki kama kuna sheria ya mabadiliko yoyote walete haraka, tuna vyumba bubu

viko vingi Zanzibar Serikali inakosa fedha tujipange haraka sana ili kuhakikisha tunalinda wageni wetu na utalii wetu na uchumi wetu kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nikupongeze wewe pia lakini pia nikupe pole kwa jinsi unavyofanya kazi kwa vizuri sana juu ya kiti hicho na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atakulinda na atakusaidia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Amina inshaallah. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Shehe Hamad Mattar na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil na baadae ni Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa na mimi kuchangia machache katika mswada ulioko mbele yetu. Kwanza niwapongeze wale wote ambao kuwa wameuandaa mswada huu lakini pia vile vile na kamati ambayo imeupitia na kutoa mapendekezo yao ambayo wameona kuwa ni muhimu kuzingatiwa. Nami sitaacha kutoa chochote katika hili kwa muono wangu na nitakwenda moja kwa moja mimi kwenye vifungu kama inavyojionesha hapa ili kuchukua muda mfupi lakini kuweza kufanya mengi.

Mhe. Naibu Spika, mimi niko katika ukurasa wa 108, kifungu Nam.4(b) naomba marekebisho haya yafanyike, hapa awali inasema kuzidisha ukuaji wa uchumi kwa lengo la kupunguza umasikini. Mimi napendekeza kwamba neno la kwanza litumike kuharakisha ukuaji wa uchumi badala ya kuzidisha, hayo ni maoni yangu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba kifungu cha 4(c) inavyosomeka ni kutathmini muda baada ya muda maendeleo ya nje na mazingira ya kibiashara na kuendelea. Kwa hivyo, mimi napendekeza hivi kutathmini muda baada ya muda maendeleo ya ndani na nje ya mazingira ya kibiashara yaongezwe maneno baina ya maendeleo ya ndani na nje ya mazingira ya kibiashara na kwa kuishia pia vile vile kupata suluhisho la vitendo, suluhisho lenye tija. Hapo napendekeza katika kifungu hiki yasomeke hivyo.

Mhe. Naibu Spika, niende kifungu kidogo (d) kinachosema kubadilisha uzoefu juu ya utekelezaji uliokuwepo na kwa mazingira ya kurekebishwa. Mimi napendekeza kwamba kubadilisha neno uzoefu litoke iseme kwamba kubadilishana mawazo juu ya mazingira ya sasa ya uendeshaji na sheria kwa lengo la kuboresha utendaji na kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, naendelea katika kifungu hicho hicho kwa kifungu kidogo cha (e) kutathmini na kupendekeza uboreshaji wa sera za kimazingira ambazo zitawavutia wawekezaji na ushindani wa kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, maoni yangu mimi napendekeza ifuatavyo. Kutathmini kupendekeza uboreshaji wa mazingira mazuri ambayo yatawavutia wawekezaji moja kwa moja wa nje na ushindani wa kibiashara, hayo ni maoni yangu.

Pia vile vile niende katika kifungu hicho hicho, kifungu kidogo cha (f) kuzingatia jambo jengine lolote ambalo litapelekea hapa naomba yaongezwe maneno matatu yafuatayo:

Kuzingatia jambo jengine lolote ambalo ni muhimu ambalo litapelekea kwa Baraza la Taifa na kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, nihame hapo niendelee katika sura ya pili uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar kifungu Nam.7(1)(b). Hapa panasema mawaziri kutoka wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hapa naomba nimuulize waziri atakapokuja mawaziri kutoka wizara za serikali je, Mawaziri wasiokuwa na Wizara Maalum je hawa hatuwezi kuwaangalia, je hawamo kuweza kuteuliwa humu nauliza hapa.

Mhe. Naibu Spika, jengine kifungu cha 7(c) wajumbe kumi na mbili, nilipoangalia neno kumi na mbili haimo katika *version* ya Kiingereza kuonesha idadi hii kwa hivyo tuiangalie vizuri sehemu yetu ambayo ya upande wa pili ya Kiingereza.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu kidogo cha 7(b) bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo kama inavyoendelea. Mimi napendekeza Nam. 2 ianze bila ya kuathiri sio bila ya kujali, mimi napendekeza bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo halafu itaendelea kama ilivyo kawaida.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 110, kifungu cha 9(b) kazi za Baraza. Hapa kuna kazi za Baraza zitakuwa ni kuweka fursa kwa majadiliano ya kibiashara baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Hapa napendekeza kwamba iwe ni kuendeleza mshikamano wa sekta ya umma na sekta binafsi. Kifungu cha 9(c) hapa napendekeza kwamba hii lugha naona iliyotumika haiendani kabisa kidogo na hali yenyewe ilivyo. Kwa hivyo, naomba isomeke hivi kama zinakubaliwa kuzingatia mambo yatokanayo na jukwaa la biashara yanayohusu maendeleo ya uchumi na kupendekeza maazimio ya mkakati kwa sekta husika kwa utekelezaji. Kifungu cha (c) naomba kiondolewe na kiwekwe hivyo kama itakubalika.

Mhe. Naibu Spika, lakini tuende kifungu cha (d) kufanya au kusababisha kwa utafiti, ukaguzi au mafunzo juu ya sera za maendeleo ya kijamii. Mhe. Naibu Spika, mawazo yangu nasema hivi kufanya au kusababisha kufanya utafiti, ukaguzi au uchunguzi juu ya sera jambo lolote au makosa ya sera za maendeleo isomeke hivyo.

Mhe. Naibu Spika, naendelea kifungu kidogo cha (f) kupokea, kuyapitia na kutoa mapendekezo juu ya sera taarifa ya ushauri uliowasilishwa. Mimi napendekeza kwa maoni yangu kupokea, kuzingatia na kutoa maendeleo mapendekezo juu ya sera, utafiti, taarifa na mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye Baraza na uhusiano.

Lakini pia vile vile baada ya maneno maendeleo ya kiuchumi iendelezwe kutoka kwa sekta mbali mbali, yaongezwe maneno hayo hapo kutoka kwa sekta mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, hayo ni maoni yangu. Niende moja kwa moja katika kifungu cha (i) kupokea na kuipitia taarifa ya utekelezaji ya mwaka ya Baraza. Napendekeza kwamba kupokea na kuijadili na sio kuipitia na kuijadili iwe hivyo.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye kifungu cha (j) kuwa na uhusiano au ushirikiano na Mabaraza mengine ya biashara ya Zanzibar liongezwe neno ya Zanzibar kwa lengo la kutafuta ujuzi wa kubadilishanataarifa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu cha (k) kuanzisha kamati endapo itahitaji kwa utekeleazaji wa kazi, yaongezwe maneno baina ya itahitaji kwa utekelezaji neno kwa ajili ya utekelezaji, badala ya inahitaji kwa utekelezaji iwe inahitaji kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, bado naendelea kutoa mchango wangu katika ukurasa wa 111, kifungu Nam.12(c). Kutayarisha hoja zinazotakiwa kujadiliwa katika vikao vya Baraza, kamati tendaji na kamati mbali mbali za Baraza. Mimi nasema hivi kukusanya ajenda za mikutano ya Baraza, kamati tendaji na kamati nyenginezo. Hayo ni maoni yangu.

Mhe. Naibu Spika, tuende katika kifungu 12(f) inayosema kwamba kutayarisha bajeti ya kila mwaka ya kazi za Baraza na kuiwasilisha kwa kamati tendaji kwa ajili ya kuthibitisha. Hili neno kuthibitisha Mhe. Naibu Spika naomba litumike kuidhinishwa iwe ni kwa ajili ya kuidhinishwa sio kuthibitishwa hiyo bajeti ndio itakapokuwa na maana zaidi.

Mhe. Naibu Spika, tuende kwenye kifungu cha (h) kutayarisha ripoti ya utekelezaji ya kazi za Baraza hapa liongezwe neno baina ya neno ripoti ya utekelezaji itajwe kutayarisha ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa kazi za Baraza. Na baadae kifungu cha (i) kufanya kazi nyengine yoyote itakayoelekezwa na kamati tendaji isomeke, kamati nyengine yoyote atakazoagizwa na Baraza au kamati tendaji hayo ni majukumu ya Katibu mtendaji.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kutoa mchango wangu katika *paper* tulionayo hapa kwenye ukurasa wa 112, kifungu cha 15(1)(c), wajumbe kutoka sekta ya umma wateuliwe na Katibu Mkuu Kiongozi kama atakavyoona inafaa. Naomba hapa watajwe idadi sheria iweze kuonesha kwamba ni idadi gani watakaoteuliwa hapa.

Pia vile vile kifungu cha (d) nayo itajwe na napendekeza wawe watatu katika kifungu cha (c) na kifungu cha (d) napendekeza angalau wawe watano kwa kupitia sekta hizo mbali mbali *Chamber of Commerce* na nyenginezo jumuiya mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika kifungu hiki cha 15(2) inaposema kwamba katika kuteuwa wajumbe kutoka sekta binafsi jumuiya ya wafanyabiashara na jumuiya nyenginezo ambazo si mwanachama wa jumuiya ya wafanyabiashara watawasilisha majina wanayopendekeza kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa ajili ya uteuzi. Naomba isomeke hivi, wanayopendekeza kwa maandishi kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa ajili ya uteuzi, yaongezwe maneno hayo mawili badala ya wanaopendekezwa kwa Katibu ioneshwe kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, bado naendelea kuchangia mchango huu katika ukurasa wa 113, kifungu Nam.16, kifungu kidogo cha (j) kuanzishwa muundo wa taasisi na utaratibu wa kutekeleza kazi kama itakavyoonekana inafaa iendelee kwa utekelezaji wa kazi za Baraza, imalizie badala ya neno inafaa kwa utekelezaji wa kazi za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, mwisho mchango wangu nielekeze katika kifungu cha (l) kuthibitisha mpango wa kazi, malengo na mkakati wa biashara kwa kamati na kuratibu utekelezaji wake kwa ajili ya kuhakikisha unafikia malengo endelevu. Mimi naomba isomeke hivi kuidhinisha mpango kazi na malengo ya kamati na kufatilia utekelezaji wake, hayo ni maoni yangu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nitoe shukurani kwa kunipa muda huu na mimi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana mheshimiwa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia mswada huu wa Baraza la Biashara ulio mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni miongoni mwa wadau wa Baraza hili na niliwahi kuwa *observer* wa Baraza hili kwa kipindi cha mara mbili. Mswada umewasilishwa vizuri na una sifa zote na utendaji wote, napenda kujikita katika maoni yangu ya mswada huu kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, sisi Zanzibar kama dunia na Tanzania ndani ya miaka 13 au 14 wakati wa Rais *Obama Administration* uchumi uliyumba na likatoka neno linaitwa *recession*. Bajeti zote za dunia ziliharibika, mipango yote ile tuliyopanga iliharibika na nampongeza Rais wa wakati ule Jakaya Mrisho Kikwete namna alivyotumia taaluma yake kuokoa uchumi. Uchumi uliyumba nadhani alikwenda mpaka akaita wachumi na uchumi ukarejea katika hali ya kawaida. Alitumia fedha nyingi kutia katika mashirika ili aweze kuwa *sustainable* na yeye alikuwa *sustain* kweli. Kwa hivyo, mimi ningependekeza katika hali hii ya furaha tunaunda Baraza hili, lakini dunia na sisi tumo kama Zanzibar itakapotokezea hali yoyote ya kuyumba kwa uchumi na sisi tuwe tumejipanga sawa sawa. Kwa hivyo, kiwepo kitengo ambacho kitakuwa kinaangalia *day to day* kuangalia hali ya uchumi ikoje katika chumi za dunia ili itakapotokea *waves* ya aina yoyote na sisi tuweze kuokoa uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kitengo hicho kiwe na mawasiliano ya dunia nzima hata kikishirikiana na *WTO* ambayo ipo Marekani, *otherwise* panaweza pakatokea *spread* tukawa tumeyumba hatujui pa kwenda, hatujui pa kuanzia. Hatujui pa kuanzia, kuanzia mkulima atalima vizuri lakini atakuwa hajui auze wapi, na hali ile kila mmoja aliiona.

Mhe. Naibu Spika, nilisoma *news* moja wakati wa *recession* nchi ya Marekani ilikuwa ina-*loose* wafanyakazi *six hundred thousand* kwa siku moja ilifukuza watu. Lakini Rais Baraka Obama akaokoa uchumi na ukarejea katika hali ya kawaida pole pole na hiyo ni miongoni mwa sifa yake, aliweza kufanya *traditional of economy* ikaja katika hali ya kawaida. Kwa hivyo, na sisi kama Zanzibar Baraza hili ningeshauri sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na Wizara ya Fedha na Waziri wa Biashara kwamba aone hali hiyo na naamini kipindi kile Waziri wa Biashara Mhe. Madam alikuwa kipindi kile yuko Marekani aliiona hali ya *recession* hali ilikuwa ni mbaya na ilikuwa ni nzito. Kwa hivyo, kitengo hicho kiundwe kiweze ku-*monitor* uchumi siku kwa siku dunia inasemaje, mbali

ya hii hali iliyotokezea lakini kama tishio lolote litakalotokezea Mwenyezi Mungu asitujaalie iwe na sisi tumejiweka sawa sawa huo ndio mchango wangu kwanza.

Mhe. Naibu Spika, ya pili ni kwamba Baraza hili liwe-*fair* kwa wawekezaji wote ziko dalili na upo ushahidi kamili kwamba hawa *foreign investors* wanapokuja hapa wanatumia ujanja kutuibia kwa kiwango kikubwa. Hali hiyo inapunguza juhudi za wawekezaji wa ndani tena kubwa tu, wao wanapewa misamaha mingi ikiwemo saruji, nondo hata kijiko cha chai. Mwekezaji wa ndani anaanza kubanwa *from the beginning* anakuwa na mbavu, anadharauliwa kwamba si chochote si chochote. Kwa hivyo, Baraza hili kadhalika liwe lina *monitor* na kumsaidia mwekezaji wa ndani na wapo na wanaweza au *otherwise* itakuwa mgeni kaja kachukua kaondoka sisi bado tutakuwa tunafuga kilema.

Mhe. Naibu Spika, nishawahi kushuhudia kwa nafsi yangu kwamba miongoni mwa kampuni zimepewa msamaha, kazi imemalizika na wameingia katika soko la ndani. Kazi imemalizika kapewa msamaha wa baadhi ya bidhaa halafu kaingia soko la ndani. Kwa vyovyote mwekezaji wa ndani au mfanyabiashara wa ndani hawezi ku-*compite* kwa sababu yeye kapewa msamaha pengine una *difference ya two hundrend thousand per term.* Hilo lipo na limefanyika kampuni imeondoka kauza vifaa vyake kwa njia anazozijua mwenyewe baadae kaingia katika soko la ndani tena alivyokuwa hana akili anatujia sisi tunao-*deal* na *item* ile ile ili tumpe nafasi ya kuuza, wengine tuna uzalendo tukasema aah sisi hii hatuwezi kuingia. Kwa hivyo, Baraza hili liwe lina-*monitor* na kumfanya mwekezaji wa ndani aweze kuwa *sustain* ili achangie uchumi wa taifa na hasa ukiangalia kwamba yeye yule ana watu ambao wanamtegemea na analipa kodi na kwa vyovyote anaisaidia serikali katika mapato pamoja na *employment*. Hiyo *point* ya pili *is very important.*

Jengine ni kwmaba katika hali hii ya biashara huweko migogoro tena wala si mikubwa ya kudhulumiana auhata ya kukaa tu katika meza moja. Kwa hivyo, kingekuwepo kitengo kidogo cha usuluhishi pindi inapotokezea migogoro kitengo kile kiweze kukaa baina ya mlalamikaji na mlalamikiwa kusudi mambo yaende mbele. Si vizuri kidogo tu, mahakamani, kidogo tu, tunashitakiana, migogoro mwengine ni kukaa meza moja tu. Mimi naamini mgogoro wa Chabria usingeamuliwa katika mahakama, *at the end of the day* Chabria leo anataka kukaa na mawasiliano ili wamalize suala hili.

Kwa hivyo, kitengo hiki kitakuwa kimekaa katikati na Chabria mjuaji kwa sababu kazi nyingi kafanya mimi namjua tangu zamani, kwa hiyo alipoona ngoma imemkaa kakubali kukaa kwamba tayari wakae kitako wamalize suala lile. Sasa kwa hivyo Baraza la biashara nalo liwe lina fursa ya ku-*intervals* mambo madogo madogo haya kusudi nchi isiwe kitu kidogo mahakamani tunaitia sura mbaya.

Kwa jumla mimi Mhe. Naibu Spika, mchango wangu ni huo na mwisho Baraza liwe na kitengo katika hicho hicho kiwe kila baada ya muda kinashirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kujua hasa mwenendo wa biashara ya dunia ili kiweze kwenda na wakati. Kila siku kuna bidhaa zinashuka, zinapanda, zinakuwa *stable.* Kwa mfano, sasa hivi nilikuwa nasoma baadhi ya *news* na nikawauliza watu wa mafuta, mafuta katika soko la dunia yanapanda na kushuka. Mimi niliwauliza watu wa *ZURA* na walinijibu suala zuri

sana kwamba kuna kitengo chenye kushughulikia mwenendo wa biashara ya mafuta kiko Uingereza, ambapo makao makuu yake yako nchi moja ya Asia, wao ndio wanatoa leo hali iko hivi, leo iko hivi. Kwa hivyo na sisi kadhalika ili tuweze kwenda na dunia tuwe na utaratibu wa kujua dunia inasemaje katika biashara ili na sisi tuingie katika uchumi wa kati wafanyabiashara ndogo ndogo wakiwa na fursa katika nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache mswada mzuri na una manufaa kwa nchi yetu na kadiri tutapoanza kuutekeleza ziko *points* ndogo ndogo nitaishauri serikali kusudi twende *fair*. Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hamza Hassan Juma baadae atafuata Mhe. Suleiman Sarahan Said lakini namuona hayupo kwa hivyo nitampa nafasi Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mhe. Hamza Hassan Juma karibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nataka nikushukuru kuweza kunipa nafasi hii kuweza kuchangia mswada huu muhimu sana kwa uchumi wa taifa letu, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri aliyewasilisha mswada huu, kwa sababu Mhe. Waziri huyu pia ni muasisi wa uanzishwaji wa hili Baraza la Biashara hapa Zanzibar. Kama tulivyoelezwa Baraza hili sio jipya lilikuwepo, lakini nadhani imeonekana kuna mambo kidogo hayaendi sawa ndio maana ikabidi sasa itengenezwe sheria ambayo Baraza litafanya kazi zake kwa usimamizi endelevu. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri na namtakia kila la kheri katika kuanzisha Baraza hili, wafanyabiashara wetu na wawekezaji waweze kupata afuweni katika changamoto mbali mbali ambazo zinawakabili.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze mbele zaidi katika ukurasa wa 122 katika madhumuni na sababu. Najua madhumuni na sababu sio sehemu ya mswada lakini ni muongozo ambao unatoa taswira na picha nini ambacho serikali ilichokusudia.

Mhe. Naibu Spika, nataka nianze *paragraph* ya mwanzo kabisa iliyokuweko ukurasa wa 123 ambayo ndio msingi mkuu wa uidhinishwaji wa mswada huu au sheria hii, naomba ninukuu inasema kwamba:

"Mswada una malengo ya kuondosha vikwazo vya kibiashara ambavyo si lazima katika uendeshaji wa biashara. Kwa muktadha huo, inaanzisha utaratibu wa kisheria ambao utawajumuisha sekta za umma na sekta binafsi kwa ajili ya kujadili na kutafuta suluhisho la matatizo na vikwazo vya kibiashara na kuhakikisha uendeshaji ulio bora na kukuza usatwi wa jamii ya Zanzibari".

Mhe. Naibu Spika, lazima tukubali kwamba wenzetu au ndugu zetu ambao wameamua kwa makusudi kuanzisha biashara au kuanzisha uwekezaji kwa upande wa Zanzibar ni watu ambao wameamua kujitolea muhanga. Kwa sababu kwanza wao wenyewe ni sekta binafsi lakini wanafika kujitolea muhanga rasilimali zao, wanakopa fedha nyingi sana

kwa ajili ya uwekezaji na fedha zile hawapewi na serikali, fedha zile wanatafuta wao wenyewe, wanatafuta uwekezaji aidha kujenga mahoteli au kufanya biashara mbali mbali.

Vile vile kitu chengine cha ziada mfanyabiashara au mwekezaji hawezi kuendesha biashara yeye mwenyewe lazima atahitaji wasaidizi, wasaidizi ina maana ataajri kuanzia Wakurugenzi na watu mbali mbali mpaka wafagiaji.

Sasa Mheshimiwa tuone umuhimu wa wafanyabiashara na kuweza kuwapa hadhi na thamani inayostahiki kwao. Kwa sababu wanakuwa moja kwa moja wametekeleza ile ilani yetu ya uchaguzi ambayo inasema kukuza uchumi na kupunguza umasikini wa kipato lakini vile vile kuweza kutoa ajira. Kwa hivyo, hawa wafanyabiashara wanatekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya CCM, hivyo lazima serikali tuhakikishe tunatoa *support* kubwa sana ili kuhakikisha kwamba wanafanya kazi za vizuri ili kuleta ustawi wa wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, kitu ambacho nataka nikianze hapa na ninaanza katika ile ile madhumuni na sababu iliyoanzishwa Baraza hili la biashara.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wawekezaji hapa Zanzibar wageni walikuja wakaomba maeneo kwa ajili ya kuwekeza katika sekta ya mahoteli na sekta ya utalii. Kwa kweli walipata usumbufu mkubwa sana, walipata usumbufu na mpaka wengine wakafikia kukata tamaa wakaamua kuondoka. Sasa baya zaidi hapo wakishaondoka wanakwenda kutupa sifa mbaya sana nje ya nchi. Kuna wengine kutokana na udhaifu wa ubinafsi wa baadhi ya watendaji ilifika pahala walikwisha kupewa maeneo na serikali na wana vibali vyote. *ZIPA* wamewapa vibali, Ardhi wametoa hati, lakini matokezeo yake Mhe. Naibu Spika, walisumbuliwa, wakanyanyaswa na wengine wakanyang'anywa yale maeneo bila ya hata utaratibu.

Mhe. Naibu Spika, wamelalamika, wamehangaika, wamekuja mpaka kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilshi kuwatetea lakini kwa kweli utekelezaji au utatuaji wa matatizo yao unakuwa ni mtihani mkubwa. Sasa kama nilivyosema wawekezaji hawa ni wafanyabiashara wana-*sacrify* wanakopa, wanahangaika ku-*invest* lakini baadae matokeo yake wanakuwa wanapata usumbufu. Kwa hivyo, naamini kupitia kuanzishwa kwa sheria hii ya Baraza la Biashara itaweza kusaidia sana kuwa wamepata sasa pahala pa kupeleka malalamiko yao. Kwa sababu humu miongoni mwa vifungu ambavyo vimo katika mswada huu wa sheria kuna maeneo ambayo wao wanatakwa moja kwa moja wapeleke malalamiko yao naamini itaweza kuwa ni muarobaini wa kuweza kuondoa matatizo yao.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nitamuomba sana Mhe. Waziri anipe mashirikiano makubwa kwa sababu bado miongoni mwao wengine wageni ambao walisumbuliwa waliamua kuondoka, lakini wazalendo ambao mpaka sasa hivi wanaendelea kunyanyasika ndani ya nchi yao kwa kuwekeza mpaka leo wananyanyasika serikali inashindwa kuwapatia hati na vibali vya kuweza kufanyia kazi. Wameshagharimu pesa nyingi sana kwa mimi na wewe Mhe. Naibu Spika, nafikiri tungelikuwa tayari tuko *ICU* taabani. Lakini bado wazalendo hawa wanaendelea ku-*struggle* bado wanakusudia kuwekeza Zanzibar. Haiwezekani mwananchi mzalendo wa nchi hii amezaliwa Zanzibar anaomba *lease* zaidi ya miaka kumi hajaipata, kweli leo tunahamasisha wafanyabiashara wawekeze? Ukiuliza

makosa yake ubabaishaji hajulikani, inawezekana pengine labda anataka kupewa mtu fulani.

Mimi nadhani umefika wakati ubaguzi tumeuondoa mwaka 1964 sasa hivi wananchi watumie matunda yao ya mapinduzi ili kuhakikisha wanawekeza wanapata salama.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwa sababu hili suala tumeshahangaika nalo sana, hata Baraza lililopita lilizungumzwa humu ndani Waziri wa Fedha aliyepita akaahidi atalishughulikia, Waziri wa Biashara aliyepita aliahidi atalishughulikia, lakini mpaka leo Mheshimiwa kwa kweli imekuwa ni kitendawili. Sasa nitaomba sana kama nilivyosema kuwa hili nitaomba mashirikiano baina ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Waziri wa Fedha na Mipango kupitia *ZIPA* pamoja na waziri wangu wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuhakikisha kwamba tunalipatia ufumbuzi suala hili ili kuhakikisha wananchi wanawekeza ndani ya nchi yao bila ya kuwa na ubaguzi wa aina yoyote. Kwa sababu haiwezekani mtu useme unamzuia huyu kwa sababu kuna mwengine anasema anataka kufanya bora zaidi, si ungelimpa na yeye kwanza halafu ukaangalia atafanya bora zaidi au vipi, lakini unamzuwia eti kwa sababu kuna bwana fulani yeye ndiye anasema atafanya vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nchi hii haina bwana, nchi hii sasa hivi ina viongozi waliochaguliwa na wananchi na kwa kweli wanatakiwa wawatendee haki wananchi wote. Kwa hivyo, kama kuna bwana mimi nafikiri kupitia mswada huu wa sheria huyu bwana sasa atakaa upande wananchi wanyonge waweze kufanya shughuli zao ndani ya nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, nije moja kwa moja kuingia katika mswada huu. Nimeangalia katika mswada huu kutakuwa kuna Baraza la Taifa la Biashara halafu kutakuwa na Mabaraza ya Mikoa. Mimi nakubaliana nayo sana haya, kama alivyosema Mhe. Simai Mohamed Said hata mimi niliwahi kuwa Mjumbe wa Baraza la Biashara na kupitia Baraza lile la Biashara nilifaidika na nilijifunza mambo mengi sana ya namna gani wawekezaji wanavyo-*struggle* kutafuta uwekezaji mbali mbali. Mhe. Simai Mohamed kazungumza vizuri sana wafanyabiashara hawa hasa wawekezaji katika sekta ya mahoteli Mheshimiwa wanaisaidia sana bajeti ya Wizara ya Utalii. Kwa sababu sisi bajeti tunayopitisha hapa ya kutangaza utalii *is pinnate,* kama tungekuwa tunategemea wizara ya utalii kutangaza utalii kwa kuja Zanzibar. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, hao watalii waliokuweko sasa hivi wangekuwa hata robo hawafiki, lakini kupitia ma-*investors* wawekezaji katika sekta ya hoteli na utalii wao wenyewe wenye mahoteli ukiangalia katika maonesho ya biashara mbali mbali duniani wanatumia *resource* zao, wanakwenda wanatafuta makampuni, wanatafuta mawakala kwa ajili ya kuleta wageni hapa Zanzibar na ndio maana tunajisifu tunapofika wakati wa bajeti tunasema Zanzibar watalii wameongezeka kutoka laki moja mwaka uliopita mpaka laki moja na sitini, ukiangalia kazi kubwa inayofanywa ni wawekezaji katika sekta ya utalii katika maonesho mbali mbali huko duniani.

Mhe. Naibu Spika, leo kila mwekezaji katika sekta ya hoteli na utalii basi ujue kwamba kila yanapotokezea maonesho ya biashara wanapeleka watu wao wanakwenda wanatangaza pamoja na kwamba wale watalii watakuja kulala katika mahoteli yao, lakini watalii wale wanahesabika wamekuja Zanzibar na wakija hapa wanatumia ndio maana

uchumi wetu unakua siku hadi siku na ndio maana kupitia sekta hii Mhe. Naibu Spika, sekta ya utalii sasa hivi katika mahoteli imeajiri watu wengi sana. Kama ingekuwa tuna udhibiti mzuri wa *control* ya wafanyakazi katika mahoteli kama mfano tungelisema tunaweka asilimia mfano asilimia 70 ya wafanyakazi kwenye mahoteli watoke Zanzibar basi nadhani huko mitaani kungekuwa hakuna vijana ambao wanazururа. Kwa sababu sekta hii imechukua wageni wengi katika sekta ya utalii ingawa asilimia kubwa ya wafanyakazi wanatoka Tanzania Bara lakini bado sisi hatuna tatizo kwa sababu bado ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, kwa kweli wafanyabiashara hawa wanawasaidia sana kuongeza uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, katika hili Baraza la Biashara hawa wanakuwa wanatoa mawazo mengi sana na miongoni mwa mawazo wanayoyatoa ndio yale tunakuja kuyaona mengine yanachukuliwa na mawaziri husika katika utekelezaji au mipango yao ya muda mfupi na mrefu katika kuendeleza nchi yetu. Kwa hiyo, mabaraza haya kwa kweli ni muhimu sana iko haja ya kuweza kushirikiana nayo ili kuhakikisha kwamba tunainua uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika Sehemu ya Pili ya mswada huu kifungu cha 5 kinasema kunaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Taifa la Biashara kwa ufupi *ZNBC* na Baraza hili litakuwa ni jukwaa la majadiliano ya kibiashara baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Sasa Mheshimiwa mimi nadhani Baraza hili kama litafanya kazi yake hasa ipasavyo haya tunayoyazungumza malalamiko ya wafanyabiashara kwa kweli yatakuwa yanaondoka. Kwa sababu nakumbuka kipindi kile Dkt. Amani Abeid Karume ilikuwa wafanyabiashara wanapolalamika pale pale Mhe. Naibu Spika, kipindi kile aliyekuwa Rais wa Zanzibar anamsimamisha mtendaji wa sekta husika jibu suala hilo moja kwa moja.

Kwa kweli tulikuwa tunaona ni namna gani, kwa hivyo hata wale watendaji wazembe ambao wanaweka vikwazo visivyokuwa na sababu wanapata sitaki kusema kuumbuka lakini wanapata kuonekana udhaifu wao wa utendaji mbele ya Mhe. Rais ambapo mara nyingi yeye ndiye anakuwa anawateuwa. Lakini sio hivyo tu, kuna kipindi alialikwa na aliyekuwa Kamishna wa *TRA,* Mr. Harry *Kitilya*, alialikwa pale Bwawani kwenye Baraza la Biashara. Wafanyabiashara walitoa malalamiko yao akajaribu kubisha bisha pale, Mhe. Rais pale pale kipindi kile akawasimamisha wafanyabiashara, hebu toeni ushahidi. Leo ilikuwa inafika pahala mtu anachukua mivao 12 ya kanga akifika bandari ya Dar es Salaam anaambiwa alipe ushuru, mivao 12 ya kanga mtu anaambiwa alipe ushuru. Sasa lakini haya bado mpaka leo changamoto hii inaendelea kutokezea kwa sababu ukiangalia ukienda bandari ya Dar es Salaam pale unaikuta mizigo mingi sana tena mizigo yenyewe watu wanabangaiza wanaganga njaa mbayo mizigo ile tayari ilikwisha kulipia ushuru hapa Zanzibar watu wamenunua wanakwenda kutafuta riziki kwa upande wa pili wa Muungano. Lakini bado suala hili halijakaa sawa. Kwa hivyo, naomba wale Wajumbe watakaokuwepo katika kipindi hichi naomba maswala kama haya waweze kuyafanyia kazi.

Lakini vile vile Baraza hili linatakiwa liwe na mashirikiano makubwa baina ya sekta binafsi na serikali. Kwa hiyo, tumepitisha hapa sheria ya *PPP* lakini bado Mhe. Naibu Spika, naona bado utekelezaji wa ile *partnership* baina ya serikali na sekta binafsi bado haujakaa sawa. Kwa hivyo, kupitia Baraza hili baada ya sheria hii na kwa kuwa kutakuwa na *follow up* kwa sababu kutakuwa na Katibu ya Kamati tendaji kutakuwa na kamati ndogo ndogo naamini hili linaweza likaja kufanikiwa vizuri.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 8(ii) ukurasa wa 110 naona kidogo hapa imetumika lugha kali. Nilikuwa naomba kidogo Mhe. Naibu Spika, lugha hii hebu tujaribu kuangalia tuifanyie marekebisho. Kifungu kidogo cha (ii) kinasema:

"Katika kuteuwa Wajumbe chini ya kifungu kidogo cha 1b cha kifungu hiki Rais atalazimika kushauriana na Jumuiya ya Wafanyabiashara".

Sasa mimi nadhani hii lugha atalazimika kidogo kama ni amri ambayo ni kali. Mimi nadhani tungelisema kwamba Rais atashauriana na Jumuiya ya Wafanyabiashara ukisema atashauriana ndio tayari hiyo ni kitu ambacho kinamlazimisha. Kuliko kusema atalazimika hii lugha kidogo iko *very hash* mimi nafikiri kidogo tuifanye iwe nyepesi. Kwa hiyo, hii tu nilikuwa napendekeza tuipunguzie kidogo makali.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile nikiangalia katika uteuzi wa huyu Katibu Mtendaji kifungu cha 11 kinasema:

Kutakuwa na Katibu Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais na kifungu kidogo cha (ii) kinasema mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa Katibu Mtendaji ikiwa angalau ana shahada ya kwanza katika fani ya Utawala wa Umma wa Uongozi na Usimamizi wa Biashara, Sheria ya Uchumi na fani yengine zinazofanana na hizo katika chuo kinachotambulika. Sasa nilikuwa hapa kidogo nataka nipate ufafanuzi huyu Katibu Mtendaji Rais anaweza kumteua kutoka katika *Private sector* kwa sababu huyu atakuwa ni mtendaji wa shughuli za kila siku na tunajua hawa watu wa *Private Sector* kidogo wana mambo yao wana shughuli nyingi. Kwa hiyo, kwenda kuwabambika ofisini kule akapigwa na baridi nafikiri kidogo itakuwa shughuli.

Kwa hivyo, mimi nadhani huyu angelikuwa ni kutoka Maafisi Maandamizi wa serikali nafikiri kidogo ingekaa sawa. Lakini hii kidogo pia nilikuwa nataka nipate tu ufafanuzi kwamba je huyu Katibu Mtendaji kama sheria inamruhusu kwamba kutokana katika sekta binafsi.

Lakini vile vile nije katika ukurasa wa 112 kifungu cha 15 kifungu cha 15 ni sehemu ya tatu ya mswada uanzishwaji wa Muundo wa Kamati za Baraza. kifungu cha 15(1) kinasema:

Kamati Tendaji itajumuisha Wajumbe 10 ambao watakuwa na uwakilishi sawa katika sekta ya umma na sekta binafsi kama hivi ifuatavyo. Hapa ameelezwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mwenyekiti mwenza ambaye atateuliwa na kamati. Lakini ikija (ii) inasema:

"Katika kuteua Wajumbe kutoka sekta binafsi Jumuiya ya wafanyabiashara na jumuiya nyengine ambao si wanachama wa jumuiya ya wafanyabiashara watawasilisha majina yatakayopendekezwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa ajili ya uteuzi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hapa tu kidogo nilikuwa nataka nipate ufafanuzi kwa sababu hawa wajumbe kutakuwa na wajumbe wanatoka maeneo mawili, kuna wajumbe wanaotoka serikalini lakini kuna wajumbe wanatoka sekta binafsi. Sasa hao wanaotoka sekta binafsi pia anatakiwa Katibu Mkuu Kiongozi yeye ndie ende akawathibitishe au *chamber of commerce* wao ndio wapeleke yale majina wale wajumbe watakaoingia kule. Sasa hili kidogo nilikuwa nataka nipate ufafanuzi.

Lakini vile vile katika kifungu cha 18 sehemu ya (iv) inayozungumzia uazishwaji wa kamati za Baraza. Kifungu cha 18(1) kinasema:

Kutakuwa na kamati zitakazoanzishwa na Baraza kama itakavyoona inafaa, halafu kifungu kidogo cha pili kinasema:

Kamati zitaanzishwa chini ya kifungu kidogo cha i cha kifungu hiki zitakuwa na uwezo wa kutekeleza jambo lolote watakalopewa na Baraza na taasisi za kibiashara za kijamii wenye maslahi. Halafu hapa katika (iii) kinasema:

Baraza litakuwa na kamati zifuatazo:-

- Kamati ya Uchumi
- Kamati ya Utalii
- Kamati ya Kilimo na Mifugo na Uvuvi na
- Kamati ya Mambo ya Ajira.

Sasa hapa Mhe. Naibu Spika, kifungu kidogo cha (iv) kinasema bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (iii) kifungu hiki bodi inaweza kuanzisha kamati. Lakini huku katika tafsiri sikuona neno bodi na hii bodi imetajwa katika eneo moja tu. Kwa hivyo, katika huu muundo sikuona kwamba kutakuwa kuna bodi. Sasa hapa kidogo Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba tu niweze kupata ufafanuzi ili nijiridhishe kwa sababu kama bodi haikutajwa huku kwenye sheria sasa hapa hii bodi sijui itakuwa ikoje.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika kifungu cha 20 kifungu kidogo cha (ii) kinaelezea hapa inakuwa kazi za kamati kupokea kifundu kidogo cha pili kinasema:

Kupokea lolote au malalamiko yanayohusiana na jukwaa la biashara kutoka kwa mtu yoyote.

Sasa hapa kifungu hichi kwa kweli ndio kimezidi mimi kunipa matumaini makubwa kwamba zile changamoto ndogondogo ambazo zilikuwa zikijitokeza kwamba sasa hivi wafanyabiashara au mtu yoyote atakuwa na uwezo wa kupeleka malalamiko kwenye hii Kamati Tendaji ili kuweza kupatiwa ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, naomba univumilie kidogo namalizia malizia nakuja katika kifungu hichi cha 18(5) kinasema kwamba:-

Wajumbe wa kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (iii) cha kifungu hichi watakuwa kama ilivyoainishwa chini ya jadwweli la pili la sheria hii.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuangalia kwenye jaduweli la pili lakini mimi nilikwenda mbali zaidi nikaja kwenye hili jaduweli la tatu. Jadwweli la tatu nimejaribu kuangalia ule muundo wa wajumbe wa kamati utakuwa kama hivi ifuatavyo:-

Sina tatizo na muundo wa wajumbe wote lakini tatizo langu liko hapa katika hichi kifungu kidogo cha 5,6,7,8 hapa kidogo naona kidogo tumekwenda kinyume na taratibu zetu za kisheria kwamba hapa miongoni mwa wajumbe ameambiwa kutakuwa na waziri mwenye dhamana ya biashara, Waziri wa Fedha, Waziri wa Ardhi, hao mawaziri wote sina tatizo.

Halafu cha 7 kinasema Rais kutoka katika Jumuiya ya wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima.

Lakini cha 8 kinasema mwenyekiti wa makampuni ya Bakhresa hapa kidogo mtihani. Sasa unaposema mwenyekiti wa makampuni ya Bakhresa sasa hapa hii ndio ile *destimination*.

Mhe. Naibu Spika, hapa wakati tuna *chamber of commerce* basi bora tungelisema na mjumbe mwenyekiti wa jumuiya ya wafanyabiashara pamoja na mjumbe kutoka katika jumuiya ya wafanyabiashara. Lakini ukisema moja kwa moja mwenyekiti wa makampuni ya Bagharesa ina maana tayari umem-*target* mtu. Huu utakuwa ni ubaguzi na sheria zetu hapa sisi hatutungi sheria za kibaguzi.

Sasa leo utakaposema mwenyekiti wa makampuni ya Bakhresa je leo makampuni ya Bakhresa kampuni zimefilisika kampuni hazipo huyu mjumbe tutampata wapi na katika masuala ya biashara hakuna mfanyabiashara mkubwa, hakuna mfanyabiashara mdogo wote wanachangia pato la taifa wote wanachangia kodi.

Mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, sheria kama hizi labda zile nchi za kifalme, maana nchi za kifalme unaambiwa Waziri wa Fedha atakuwa mtoto wa nani Waziri wa nini atakuwa mjukuu wa nani. Lakini katika sheria zetu hizi za Demokarasia unapomuelekeza mtu *direct* hapa itaonesha kuna upendeleo maalum au upendeleo fulani.

Kwa hivyo, mimi sitokubali kuridhia katika jaduweli hili kwa sababu najua dajuweli ni sehemu ya mswada mimi nitakuja kuzuia fungu hili ili kuhakikisha kwamba hili jina la mwenyekiti wa makampuni ya Bakhresa linaondolewa isipokuwa ibadilishwe iwekwe mjumbe kutoka *chamber of commerce*. Sasa wenyewe *chamber of commerce* huku watajua nani wenyewe wanaweza wakampendekeza awe mjumbe katika hili Baraza la Biashara au kama kuna nafasi nyengine huko za uteuzi anaweza akateuliwa. Lakini kwa

kuweka ndani ya sheria kwa kweli tutakuwa tunakiuka ile misingi ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba tena kumshukuru tena Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu mswada ni mzuri hizo changamoto ndogo zilizojitokeza naamini yeye ni msikivu ataweza kuzifanyia kazi ili tuweze kuupitisha mswada wetu huu bila ya matatizo yoyote.

Naomba wafanyabiashara wengine ambao hawajajiunga na *chamber of commerce* wajiunge kwa sababu sasa hivi wamepata sehemu ya kutatua matatizo yao. Kama alivyosema Mhe. Simai Mohammed Said kuna masuala ya ajira, kuna masuala ya mishahara na mambo mengine. Baraza hili ndio nafasi yake pekee litakaloweza kujadili masuala mbali mbali ya biashara, masuala la ajira kama sasa hivi kuna wafanyakazi wengi ambao wanafanyakazi katika taasisi mbali mbali hawana hata ile mikataba hata ile ya muda watu wanafukuzwa ovyo wanafukuzwa kama kuku.

Kwa hyo, mimi nadhani kupitia hili Baraza la Biashara itakuwa ni sehemu pekee ya kuweza kutoa maoni na ushauri kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu na wafanyabiashara wanafanyakazi bila ya matatizo katika nchi yao.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii isipokuwa tu kwa asilimia 80 asilimia 20 naziweka katika kile kifungu ambacho nilichosema yale maneno yaondolewe. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassaan Juma. Waheshimiwa Wajumbe minong'ono kwanza imezidi mnazungumza sana hata hizi sauti sasa zinakuwa hata hao wanaoturikodi wanakuwa hawatupati vizuri hilo moja.

Lakini wakati mnafanya majadiliano mjue kwamba kuna *live* kamera hizi hapa ambazo watu wanaona na wengine mnatizamana hivi mnazungumza haioneshi vizuri.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe mjue kwamba hapa mnaonekana na wananchi wapiga kura wenu wanakutizameni. Sasa ina*judge how much serious you are* katika majadiliano hayo. Naomba tuliangalie kwa hilo. Ahsante nashukuru.

Baada ya hapo mchangiaji wetu mwengine atakuwa ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani kama muda utatosha samahani Mheshimiwa nimesema Mhe. Abdalla Maulid Diwani halafu baadae Mhe. Suleiman Said Sarahan Mheshimiwa ulikuwa hupo ndio maana nikamtaka Mhe. Abdalla Maulid Diwani na muda ukitosha utachangia wewe. Mhe. Abdalla Maulid Diwani karibu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika mswada huu uliopo mbele yetu.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu hizo, vile vile nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kutuletea mswada huu wakati muafaka japo kwamba kidogo umechelewa. Mswada huu ulikuwa uletwe

kipindi cha nyuma zaidi kwa sababu nyuma kulikuwa na sheria tu ya kuweka na kuangalia namna gani Baraza la Biashara linafanyakazi lakini hakukuwa na sheria kama ambavyo imeletwa hivi sasa. Nakushukuru sana kuona kwamba umeletwa japo kwamba umechelewa.

Kama ilivyo kwamba Baraza la Biashara ni *corridor* ambayo wafanyabiashara iwe kimbilio lao kwa ajili ya kupeleka changamoto zao mbali mbali zinazowakabili katika shughuli zao za kila siku. Sasa wakati umefika naomba Wajumbe wenzangu sote tuunge mkono huu mswada ili tumalize hapa tuangalie tuwape neno wenzetu wa kuweza kusimamia haya yaliokuwemo humu.

Lakini kuna changamoto zake ambazo toka kuanzishwa Baraza la Biashara na mpaka leo Baraza hili bado kuna changamoto ambazo zimekuwa sugu. Kwa hiyo, Mhe. Waziri nakuomba sana katika mswada huu kwamba yale ambayo yamekuwa changamoto ambazo ziko katika mikono yako basi zingetatuka.

Mjumbe mwenzangu aliepita alizungumza baada yake tu lakini zipo nyingi na kila siku tunaambiwa zinatatuka lakini bado tatizo kubwa sana kwa wafanyabiashara wenzetu wa Zanzibar kwa upande wa pili wa Muungano. Kwa hivyo, hili Baraza litakuwa kimbilio la kwenda kukaa pamoja na kubadilishana mawazo kuona namna gani hizi changamoto ambazo zilizokuwa si za kikodi na yenginezo zinaweza kutatuka ili watu wetu wakafaidika na biashara hii ambayo ipo ndani kwetu.

Sasa mimi naomba niende moja kwa moja katika mswada huu niende katika sehemu ya tatu uanzishwaji wa muundo wa Baraza. Hapa nakubaliana napo vizuri imewekwa vizuri kabisa hata mchanganuo wake naomba ninukuu kipengele cha 15(1);

Kamati tendaji itajumlisha wajumbe 10 ambao watakuwa na uwakilishi sawa kutoka katika sekta ya umma na sekta binafsi. Hapa iko vizuri sana nakushukuru sana Mhe. Waziri.

Lakini katika muundo huu huu kule katika kifungu cha 18 katika uundwaji wa kamati, pale ndipo panapo kilio changu mimi. Kilio changu mimi tuangalie katika muundo wa kamati ya Biashara, Uwekezaji na Kodi. Tukumbuke kwamba biashara au sekta binafsi ndio asilimia tisini naa ndio imekamata hii biashara serikali sasa hivi haifanyi biashara.

Sasa katika hichi ningependekeza tu angalau basi wale wajumbe kungekuwa na uwiano tafauti na wajumbe waliopangiwa hapa katika kamati hii kuna wajumbe karibuni 13 lakini ukiangalia wajumbe wa sekta binafsi ni wajumbe 3.

Kwa hiyo, tayari kunapunguza ile wigo wa changiaji katika hawa hapa kuna mawaziri, kuna makatibu wakuu lakini kwa wao wameka mwenyekiti wa makambuni ya Bakhresa kama mwezangu alivyozungumza si mahala pale hapa hapastahiki lakini naipongeza sana Kamati ya Sheria kwa kuweza kuliona hilo kwamba wamebalisha. Naipongeza sana kwa vile wametoa mapendekezo kwamba mfanyabiashara maarufu tu ni jambo zuri. Lakini mwanzo kidogo ilikuwa imesham-*point* mtu lazima awe yeye. Sasa nashukuru

kwa uledi wa kamati hii kutuletea marekebisho haya nafikiri marekebisho haya yatapita bila ya matatizo.

Lakini sasa bado kunahitajika watu wengine wa ziada kuongezwa *category* hii ambayo ina wajumbe 13 ili angalau uweko uwiano kama huku mlikounda kamati yenu ya Baraza ilivyosema kwamba watakuweko wajumbe 10 wenye uwiano sawa kama 5 sekta binafsi na 5 katika umma unaona kumekaa vizuri tu. Lakini kwenye kamati hizi ndogo ndogo mmerudi kule kule kujipendelea wenyewe serikali zaidi kuliko sekta binafsi wakati serikali haifanyi biashara tena isipokuwa inaratibu tu na kusimamia biashara ya nchi hii. Kwa hivyo, ningeomba sana marekebisho yanahitajika kidogo angalau kuongezwa watu kuweko na uwiano ule wa kulingana na si huko tu hata katika Wajumbe wa kamati ya Utalii. Mwenzangu alisema hapa katika hili kulikuwa vile vile kuna haja ya kuwatia wale wawekezaji wazalendo wa utalii katika kipengele hichi hapa mmeandika tu Mjumbe wa Jumuiya ya Utalii uwekezaji na Mjumbe kutoka katika jumuiya inayotembeza watalii. Kwa hivyo, wapo hata wamiliki wa mahoteli wana changamoto nyingi sana hawa katika suala zima la shughuli yao wanayoifanya kila siku. Kwa hivyo, ningependelea kuwepo wale wenye ma-*restaurant* wanaostahiki kuingia hapa.

Lakini vile vile nikienda katika kamati ya Kilimo na Uvuvi hapo mapendekezo yangu mimi wapo hapa wajumbe wanne kutoka sekta binafsi lakini wajumbe watano kwa hivyo inalingana kidogo. Lakini ikumbwe kwamba tukitoka kuna mjumbe kutoka jumuiya ya wakulima wa karafuu nafikiri hichi kipengele kingefutwa kidogo angalau ikasomeka kwamba Wajumbe kutoka Jumuiya ya wakulima wa viungo, ili wakaingia hapa kwa sababu hapa tusitegemee kwamba tutakuwa na karafuu tu sie tunataka tu-*stimulate* kilimo chetu cha biashara tutakuja kulima vanila hapa, tutalima hiliki, pilipili manga. Kwa hivyo, hapa angalau ingekuwa basi mjumbe kutoka jumuiya ya walima viungo ambayo wanaingia wote hawa. Lakini ukisema kama mjumbe wa karafuu tu peke yake ina maana hata baadae mbele tukisimama katika vilimo vya vanila, mfano hiliki atakuwa hana nguvu na hana mwakilishi, ningeomba hiyo kidogo ichukuliwe na iangaliwe kama inafaa iingizwe.

Lakini hata vile vile tukitoka kwenye ukulima huu tuna mwani, inaonaje basi katika jumuiya ya walima mwani wasiwepo kwa sababu wale watu wamekuwa na changamoto nyingi, siku hadi siku wanalalamika, kwa hivyo hii *corridor* ni sehemu yao pekee kupeleka malalamiko yao. Kwa hivyo, ningeomba basi watafutiwe sehemu yoyote wawekwe na wakulima wa mwani, mjumbe kutoka Jumuiya ya Wakulima wa Mwani, kwa sababu tunapiga kelele kwamba mwani sasa hivi unakwenda kuwa zao la tatu la biashara kwa Zanzibar. Kwa hivyo, wana kila sababu na wao kuingizwa katika wajumbe hao.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, alizungumza mwenzangu katika madhumuni na sababu kwa mswada huu, ni kweli kuondoa changamoto, lakini bado changamoto zimekuwa kero kubwa sana inasababisha hata baadhi ya wafanyabiashara wetu kushindwa kuwafanya biashara katika nchi hii sasa hivi, hususan sasa hivi jinsi yanavyotafutwa mapato katika nchi hii, imekuwa kero kubwa Mhe. Waziri wa Biashara kuna haja ya kukaa na Waziri wa Fedha na Mipango ili kuona mustakabali mzima kwa sababu malalamiko yamekuwa mengi sana kwa wafanyabiashara wetu kwa kupitia taasisi zetu hizi za serikali.

Kwa mfano, *ZRB* sasa hivi wanafanya mambo ambayo hayastahili kufanywa kutumia vikosi vya SMZ katika suala zima la kukusanya kodi. Wamewapa wale *temporary permanent* za kufanyia kazi, lakini mara wanapoachana na utawala ule wa *ZRB* wanakwenda *personal* vikosi kwenda kuwanyanyasa wafanyabiashara wetu. Kwa hivyo, hiyo inakera na inaleta kadhia kubwa sana kwa wafanyabiashara wanalalamika. Ndio tunahitaji kodi, lakini itafutwe *approach* itakayokuwa nzuri kwa wale wafanyabiashara kulipa kodi kwa furaha, tofauti na sasa hivi imekuwa vitisho na hawana furaha na biashara zao wanazozifanya.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa na mengi lakini wenzangu mengi wamenifilisi nimeamua niseme hayo machache, naunga mkono hoja hii angalau kwa asilimia 99 na hii asilimia moja iliyobakia nitasubiri mpaka maelezo ya Mhe. Waziri. Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Suleiman Sarahan, na kama muda utatosha basi tutamkaribisha Mhe. Dk. Makame Ussi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru sana kwa kuniona ili kuweza kuchangia hoja kidogo ambazo zitaboresha baadhi ya mambo ambayo tunapitia katika mswada wetu huu.

Mhe. Naibu Spika, mimi niangalie katika vifungu lakini nilikuwa nazungumza kwamba baadhi ya vifungu vinahitaji kuangalia na kutazama lengo na madhumuni halisi ya hili neno kwa visiwa vyetu viwili, maana yake tunaizungumzia Zanzibar katika Baraza letu, lakini Zanzibar ni visiwa viwili vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo ambayo zana nzima ya Baraza la Biashara ni kukuza uchumi, ambalo kwa wenzangu waliozungumza tunaangalia kama uchumi mkubwa ndio tunaoutizama zaidi, lakini tukitizama na uchumi mdogo ndio unaoweza kutupunguzia baadhi ya changamoto zikiwemo ajira ambazo kwa kweli ndio ni moja ya changamoto zinazotusukuma sana katika kupata changamoto nyingi za vijana.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kwanza naomba katika huu mswada ni kwamba katika ile sehemu ya uwakilishi, najua kuna watu wengi ambao wanaingia katika maelezo yale, lakini katika upande wa Pemba ningeomba kama itawezekana Afisa Mdhamini ambaye anakuwa kama ni kiongozi wa wizara kutoka kisiwa cha Pemba, basi na yeye labda kama itawezekana awe ni mjumbe wa Baraza ili kuweza kujua yale ambayo yamezungumzwa katika Baraza kwa upande wake wa Pemba, ili aweze kuziona zile changamoto ambazo zipo.

Kwa hivyo, katika jumla ya wale wajumbe ambao watakuwa ni wajumbe wa Baraza, basi kama itawezekana ningeomba huyu mwakilishi mmoja kutoka Pemba ambaye ni Afisa Mdhamini basi na yeye aweze kupata nafasi ili kujua kama yeye ni msimamizi mkuu wa wizara ile, basi aweze kuingia mule kama ni changamoto ya kuweza kujua nini ambacho kwa Pemba kwa mwaka huu au kwa mkutano huu ambao utakuwa una changamoto zipi

ambazo yeye asiwe mgeni katika wale wajumbe kujua kumefuatwa nini. Kwa hivyo, ningeomba kama itawezekana Mhe. Naibu Spika, basi na yeye apate uwakilishi ili ajuwe nini ambacho kinaendelea katika lile Baraza.

Mhe. Naibu Spika, pia mimi ningeomba kuna jambo jengine kuna kitu kinaitwa nembo ya Zanzibar ambayo ni *brand* ya Zanzibar. Katika hili Baraza letu la Biashara Zanzibar inatumika kila pahala, inatumika mambo mengi sana, inaonekana kama haina udhibiti fulani. Hata hilo Baraza ukisema la Zanzibar linaweza likawa limetungwa Baraza jengine la Zanzibar likawa hata hili la kwetu halijulikani. Nembo yetu wanaitumia watu wana haina udhibiti wa kutosha. Kwa hivyo, ningeomba sana Zanzibar nayo ikawa ina hati miliki yake hii ya *brand* ikajulikana hasa ikitajwa Zanizibar unaijua Zanzibar ni ipi, sio kila mmoja awe anajitajia na kuweka *point* zake akijiwekea baadhi ya malengo yake ya kibiashara kwa kupitia mgongo wa Zanzibar. Hili nalo niliomba niliseme ili liweze kuangaliwa.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, humu sikuona kwamba hili Baraza litakuwa linatumia lugha gani sahihi, ama litakuwa linaendeshwa kwa lugha ya Kiingereza au kwa lugha ya Kiswahili. Sasa ningeomba kama kutakuwa na ufafanuzi au kama kutakuwa na maoni, lugha zote mbili zitumike au itumike lugha ya Kiingereza kwa sababu inawezekana baadhi ya wadau wakawa ni watu ambao lugha ya Kiswahili inaweza kuwa ni changamoto kwao, lakini wakawa mkutano umeanza mpaka umemalizika hawajui hata wamepata nini. Sasa sikujua utaratibu utakaotumika katika hili Baraza, kama itakuwa ni lugha ya Kizungu au ni lugha ya Kiswahili au lugha zote mbili, labda hapo nafikiri waziri atakapokuja aangalie na yeye ni kitu gani ambacho tunaweza tukaangalia.

Vile vile kuona changamoto Mhe. Naibu Spika, kuna changamoto mbili. Kuna changamoto za kusema na kuna changamoto za kusikiliza. Mhe. Naibu Spika, niliomba katika utafiti humu nione kama kutakuwa na uhalali pamoja na changamoto nyengine basi wale wadau na wajumbe wote wa lile Baraza wakati wa kuweka vikao vyao basi baadhi ya vifanyike Pemba, ili wale wajumbe *physical* waione Pemba hali halisi ilivyo ili na wao waweze kutoa mchango wao kama itawezekana kuangalia hali halisi. Kwa hivyo, ningeomba sana kuangalia kabisa.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kuna biashara ambazo kama mjumbe mwenzangu mmoja Mhe. Abdalla Diwani alizungumza, biashara ndogo ndogo ambazo Pemba ni nyingi sana, lakini bado utaratibu wa kuzinyoosha biashara zile bado ni changamoto. Tulikuwa tunazungumza sana kuna biashara hata tukisema hizo za mafuta ya karafuu na vitu gani, ni biashara ambazo ni kubwa, lakini bado changamoto yake haijajikita ikawa kama ni biashara kubwa sana katika ukanda wetu huu kutumika mafuta yetu ya makonyo, mafuta ya karafuu, mafuta ya mchaichai, mafuta ya mkataruki, kuna vitu vingi sana pale.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nataka mara moja ukifika wakati wa maembe uende Pemba. Mhe. Naibu Spika, maembe Pemba yanauzwa kwa ndoo haliuzwi moja moja, ndoo nzima shilingi 1,000/-. Lakini Mhe. Naibu Spika, nataka nikuambie Pemba inaendeshwa kwa chakula ambacho ni *fruit delicious* ni embe inakwenda miezi mitatu haijesha. Pale kuna watoto wanaponea maembe wala hawataki *fruit* nyengine. Yeye asubuhi anakwenda chooni raha mustarehe. Mhe. Naibu Spika, embe kwa ndoo wanauza

shilingi 1,000/- embe za pembeni ambazo kukuambia kweli zinatusaidia sana kwa afya zetu. Sasa ningeomba na hilo Baraza katika vikao vyake watutizamie sana vitu ambavyo havihitaji vitu vikubwa, vinahitaji vitu vidogo vidogo sana, mashine ndogo ndogo sana.

Mhe. Naibu Spika, kule Pemba tunaweza tukawa tumefuta ajira zikawa hakuna ajira za kutosha. Tukapata viwanda vidogo vidogo na *brand* ambayo tutazitumia *packaged* zile, basi Mhe. Naibu Spika, ningeshauri Baraza hili kila linapokaa basi likatupa jicho katika sekta, kwa sababu nataka nikuambie Mhe. Naibu Spika, kwamba Pemba katika ukanda wenye ardhi nzuri, mimi naweza kusema hakuna kisichoota ni Pemba. Ukipanda mgomba mmoja Mhe. Naibu Spika, baada ya mwaka mmoja basi utapata migomba 20 kwa ule mgomba mmoja tu na ndizi kumi kumi kila upande.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Naibu Spika, hivi ni vyakula pamoja na kuangalia kwamba zao kubwa ni karafuu, lakini Mhe. Naibu Spika, nataka nikuambie kwamba muhogo na ndizi Pemba limekuwa ni zalisho. Naweza kukuambia kama ingekuwa kama kuna udhibiti maalum, basi Pemba ikawekwa kama ni kisiwa cha kuzalisha tu ili Zanzibar ilishwe na kwengine ipelekwe, tunaweza tukapeleka kwenye baadhi ya maeneo sana.

Kwa hivyo, utaratibu ningeomba baadhi ya vikao vya kamati vitakavyokaa kuangalia mustakabali basi Mhe. Naibu Spika, waiangalie Pemba ni nini kinaweza kikawa, maana yake mpaka sasa hivi kitu tunachoweza kusafirisha Pemba ni karafuu hakuna kitu chengine. Mheshimiwa Pemba ina nafasi kubwa ya kuweka viwanda bila ya kuathiri hali halisi, maana yake kuna Ukanda wa Vitongoji una upepo wa bahari ambao hakuna nchi nyengine zinazokwenda. Kwa hivyo, ukanda ule ukijengwa viwanda nafikiri hautaathiri watu, kuna nafasi ya kutosha. Ningeomba hili Baraza litizame vizuri sana nafasi hizi kwa upande wa Pemba ili tuweze kujua katika suala hilo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika biashara pamoja na mambo ambayo yanakwenda, lakini bado suala la usafiri Pemba ni gumu, hakuna usafiri ambao unakua *continuously* katika mambo ya kibiashara. Mtu anakwenda Dar es Salaam na kurudi na siku hiyo hiyo anarudi tena, Pemba siku nzima anaimaliza kwenye usafiri na hata akifika kachoka kama aliyepigwa magongo, na akienda kwenye ndege bei mheshimiwa ukauze n'gombe na mwanawe ndio upande ndege.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tukitaka kukuza biashara basi suala la miundombinu ni muhimu sana. Sasa hivi Pemba hatuna boti hata moja ya *speed*, wewe ukitaka utapanda meli hutaki utapanda meli, meli inachukua masaa 6 au 7 na bahari inapokuwa nzito mpaka masaa 10, mpaka ukifika siku ile hata mtu akikupa maji ya kunywa huyataki, siku ile wewe ni kulala ukakandwa tu kwa hali ilivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana ili kuweza kukuza biashara basi Pemba itizamwe katika suala la usafiri, nauli ni bei kubwa ya ndege na ndege zenyewe hazipo, maana yake ndege zenyewe ni chache, lakini meli ndio zinazofanya kazi hatuna *speed* boti. Kwa hivyo, ningeomba pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ilitizame suala hili kwa jamii kwamba kunahitajika boti sasa. Inaonekana wawekezaji kwa suala la boti labda hawako tayari kupeleka maboti Pemba, lakini kama sikosei Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji anaweza akafanya mambo yake kwa vile

ni jukumu lake kuangalia hali halisi ya wananchi wake katika usafirishaji kwenye visiwa vya Unguja na Pemba akatutafutia boti za *speed* zinazoweza kutoka Pemba kuja Unguja.

Kwa hivyo, ili tuweze kujiendesha kiuchumi, ningeomba sana suala la miundombinu ya usafiri Pemba likatizamwa kwa jicho ambalo kukuambia kweli bado usafiri, pamoja na kwamba kuna meli bado suala la usafiri ni gumu sana. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, walichukuwe hili kulitizama kabisa katika mazingira hayo.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie ukanda wa Pemba, ukanda wa Kenya ambao uko Mombasa. Mhe. Naibu Spika, sijui katika kujipanga kwao katika mazingira haya watautizama vipi ukanda ule wa Kaskazini ambao unakamatana na ukanda wa Tanga na ukanda wa Pemba. Pemba na Tanga mheshimiwa hakuna tatizo kubwa katika biashara, tatizo ni vikwazo vinavyokuwepo pale baina ya Tanga na Pemba ndio vinakuwa tatizo, na lazima vitu vinakua ghali Pemba watizame kwa nini wajuwe kwamba kuna tatizo. Kama nyama zamani ilikuwa ikichinjwa Pemba, basi watu walikuwa wakichukua nyama Pemba kuleta Unguja. Nyama ya ng'ombe mheshimiwa, kitoeleo cha nyama ya ng'ombe kilikuwa kinatoka Pemba kinaletwa Unguja. Leo Mhe. Naibu Spika, nyama ya ng'ombe inatoka Unguja inapelekwa Pemba, kwa sababu bado ukiritimba mheshimiwa tukubali tusikubali bado *boarder* zetu za bandari kutoka *Mainland* bado zina usumbufu mkubwa kibiashara. Hili Baraza likakae lizungumze kiundani, kwa sababu wananchi wa Pemba wanakosa huduma na vitu vyake vinakua ghali.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumze kidogo tu samahani kuhusu biashara ndogo ndogo, kama sio kuhamasishwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifungo na Uvuvi na wenyewe na niishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais inahamasisha sana, Pemba sasa hivi nyanya hizi tungule zinauzwa mpaka kwa pishi, visadolini shilingi 2,000/- au 1,000/- zimezalishwa kupita kiasi. Haya matikiti yamezalishwa kupita kiasi. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kupitia Ofisi ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi bado kuna nafasi nzuri ya kushajihisha tukapata ukanda ule. Lakini tatizo tulilonalo mheshimiwa, tuna tatizo la kitoweo cha nyama ya ng'ombe Pemba ni ghali sana kutokana na hali halisi ya ng'ombe wanavyopatikana. Maana yake ng'ombe Pemba hawako tena, wale wa kuchinja kama wale wa wananchi hawako tena Pemba. Ng'ombe anayetoka Tanga mpaka akifika pale kama amechukua ng'ombe wanne au watano basi mmoja anakufa njiani, kwa hivyo hasara ile anamtilia yule yule mlaji. Kwa hivyo, ningeomba kuwe na utaratibu katika hili Baraza litakapowekwa katika masuala ya kilimo na lishe waliangalie sana kuna uhalali wa mifugo ambayo ikitoka Tanga kuja huku basi tuweze kufaidika.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kwamba watu wa Pemba wakipata lishe nzuri ni wazima sana kwa ule upepo wao wa bahari ni wazima kweli kweli. Kwa sababu mtu mmoja mheshimiwa aliyekuwa kazaa watoto 10 anaambiwa hakupata uzazi, ujuwe wako *strong* sana. Kwa hivyo, mheshimiwa nataka nikuhakikishie kwamba tukipata lishe vizuri kutokana na biashara zetu hizi tunaweza kwenda vizuri.

Lakini Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho ambalo nataka nilizungumze kidogo ni suala la kuendeleza. Tatizo tulilonalo ni kwamba kwa kushajihisha ni maneno mengi yanatoka kwenye wizara za biashara tutafanya viwanda vidogo vidogo siku zote. Mhe. Naibu

Spika, hebu hili suala waende wakalikalie kitako Pemba kuna nafasi za kutosha za kufanya viwanda vidogo vidogo, tutapunguza matatizo mengi. Mheshimiwa biashara yoyote haianzi kubwa inaanza ndogo halafu tunakwenda kubwa, tutampunguzia Mhe. Mahmoud Thabit kutaka dawa kama tutakuwa wazima, mgonjwa mpaka akifika kule ni tatizo la lishe pamoja na viwanda na pesa Pemba pesa hakuna. Pemba kuna chakula lakini pesa hakuna.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka nichangie tu ili nione kuna utaratibu wa kutusaidia na katika ajenda zitakazozungumzwa mheshimiwa Pemba iwe na *special*. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Naibu Spika, na pia nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mimi niwashukuru sana kwa utulivu wenu mlionionesha asubuhi hii ya leo. Hadi kufikia hapa naahirisha kikao hadi jioni saa 11:00.

(Saa 7:00 mchana kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

IMEHARIRIWA

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti, (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

(Saa 11.05 Kikao kiliahirishwa mpaka wajumbe watakapotimia quorum)

(Saa 11.16 Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo Kusomwa kwa Mara ya Pili

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na michango kuhusu mswada uliopo mbele yetu anayefuata ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kuchangia mswada ambao uko mbele yetu kwa haraka haraka, niombe tu Mwanasheria Mkuu awe makini kidogo katika kumsaidia Waziri wa Wizara hii, kwa sababu juzi tumepitisha mswada hapa siku hiyo hiyo umetayarishwa na siku hiyo hiyo Mhe. Waziri akausaini. Kwa hivyo, wadau kidogo wamelilalamikia hili na ndio nilipomfuata Mhe. Mwanasheria Mkuu ofisini kwake kutaka ufafanuzi, narudia tena labda alifikiri nataka kumpiga kirungu aa.

Mhe. Mwenyekiti, pia wameelezwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mpinduzi, kwamba mawaziri wajaribu kutokukaa ofisini kila wakati wateremke kwa wananchi kufanya ziara, ili kero zinazogusa wananchi wapate kuzitatua mawaziri.

Baada ya hapo, nianze na ukurasa wa 11 kutakuwa na Katibu Mtendaji 11(4) Katibu Mtendaji atakuwa anawajibika katika majukumu yake kazi atazokueleza. Hoja hii iliyokuwepo hapa Mhe. Mwenyekiti, pana baraza na kamati, Katibu Mtendaji huyu sijui ana mkono wa pweza atapokea maagizo kutoka wapi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba neno muongozo liondolewe.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu 12(2) hapa naomba Mhe. Waziri anisikilize viziri mimi elimu yangu ni ndogo, ndio mpaka leo nasota hapa Unaibu Waziri wala Uwaziri sijapata wala hajakosea Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kutokana na elimu yangu kuwa ndogo. Katika kutekeleza kazi hii zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) kifungu hichi Katibu Mtendaji atakuwa chini ya usimamizi muongozo wa Wizara ya Biashara tukamate wapi. Atachukua maagizo kutoka baraza au kamati ya wizara nafikiri Mhe. Waziri amenifahamu hapo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha moja kifungu hichi cha Katibu Mtendaji atafuata maelekezo na miongozo atakayopewa na Baraza. Kwa kweli, huyu mtambana sana, baraza, kamati pamoja na wizara inamsubiri. Neno hili liondoke maoni yangu.

Mhe. Mwenyekiti, jaduweli nyengine 15(b) Mwenyekiti Mwenza ambaye atachaguliwa na Kamati Tendaji kutoka miongoni mwa wajumbe wa sekta binafsi. Hapa kidogo pananipa mashaka Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu jaduweli inasema atatoka *Chamber of Commerce* au sekta binafsi hapa naomba ufafanuzi.

Nikitoka hapo nije 15(4) Sekta Binafsi hapa kidogo pana mashaka na hapa Mhe. Mwenyekiti, kidogo nitakuwa mkaidi mpaka nipate elimu ya kutosha. Hoja yangu iwekwe wazi muda wa wajumbe watakaotumika kwenye kamati kama miaka miwili au mwaka mmoja, wasi wasi wangu hapa kuna kitu kizuri au si kizuri kinaweza kikaja kikatokeza maana yake mtu anaweza kuja kuudhi akaambiwa kaa upande, au pawe na uwezo fulani ilimradi isije ikatumika siasa zaidi kwa ufupi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kifungu cha 16(g) kuthibitisha bajeti ya mwaka mpango wa kazi katika masuala ya ajira kwa kuwasilisha Wizara ya Biashara Viwanda na Maskoko. Mhe. Mwenyekiti, naomba kupendekeza neno hoja iwe maneno ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko liondoke na lipendekezwe neno waziri anayeshughulikia. Tumeshuhudia hapo nyuma tulikuwa tuna Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii sasa imebaki Wizara ya Afya tu peke yake jamii imekwenda katika uwezeshaji nafikiri kiswahili kinaeleweka. Kwa hivyo, wizara wakati wowote Mhe. Rais anaweza akaondosha lakini waziri anaweza akabaki nafikiri kimeeleweka.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa si mkubwa ulikuwa ni huo mdogo tu sehemu tatu hizo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje anielimishe, ili nipate kufahamu. Kwa hivyo, narudia yale yale elimu yangu mimi ni

ndogo, lakini baada ya maelezo hayo akesha kunifahamisha Mhe. Waziri, nafikiri nitakuwa sina tatizo maana yake tumekuwa tukitunga sheria baadaye utekelezaji unakuwa mzito.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti ndio nikampa tahadhari kidogo Mwanasheria Mkuu hapa, maana yake tulipitisha sheria ya Kamisheni ya Ardhi na Mazingira Mhe. Rais alikwisha kusaini nafikiri Waziri wakati huo Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban, Mwanasheria Mkuu binaadam pengine alisahau matokeo yake ikaja ikapigwa tarehe nyuma ikarudishwa si kitu kizuri. Hivyo, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu hapa aandike hicho kitu, ili afuatilie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba nimalizie hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub ahsante. Mchangiaji anayefuata ni Dkt. Makame Ali Ussi na baadaye Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini ajitayarishe.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji wa mada hii adhimu mada ya Sheria ya Biashara kwa Kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Biashara. Kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza wote waliohusika kwa njia moja au nyengine katika kutayarisha waraka mzuri kama huu, niseme tu mimi hapa kwenye waraka huu nimevutiwa sana na mambo mawili, ambayo nitayaeleza kama ifuatavyo.

Lakini, kwanza kabla sijaendelea naomba niende kwenye ukurasa huu page hii ya kwanza Nam. 108 hapa kuna kifungu Nam. 3 hapa kinasome Jumuiya maana yake ni Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar. Sasa hapa kuna kitu kimekosekana ama kuna kituo kidogo kimeachwa au kuna kundi moja limekosekana kwa sababu inasomeka kwamba wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima. Sasa isomeke wafanyabiashara, wenye viwanda, halafu na wakulima, nadhani itakuwa hiyo ni sahihi zaidi kuliko wafanyabiashara na wakulima itakuwa kama vile haikukamilika sentensi.

Halafu ya pili niingie kwenye ukurasa Nam. 4 hapo hapo kwenye kifungu cha (d) inasomeka kwamba kubadilishana uzoefu juu ya utekelezaji uliokuwepo. Kwa hivyo, hapa Kiswahili kidogo unasema uliokuwepo maana yake uliokuwepo hapo, lakini uliopo hivi sasa nadhani itakuwa sahihi zaidi kwamba utaratibu uliopo sasa hivi na mazingira ya kurekebishwa kwa lengo la kuboresha utendaji.

Baada ya kusema hivyo, sasa niingie kwenye mambo ambayo kwa kweli yamenivutia sana kwenye hii.

Kwanza kabisa hili Baraza ni kubwa sana ambalo kwa kweli litaleta matumaini makubwa kwa wananchi, kwa sababu kwanza Mwenyekiti wake ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar. Kwa kweli, nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kukubali kuwa mwenyekiti wa Baraza hili, kwani ni Baraza muhimu sana ambalo linawagusa sana wananchi, hapa nawasihi wananchi waone kwamba Mhe. Rais anawajali sana. *(Makofi)*

Halafu suala la pili ambalo napenda niliseme nalo limenivutia ni kwamba huu waraka huu, pamoja na mambo mengi yaliyoelezwa humu unagusia sana mambo haya yafuatayo, mambo haya naomba yatiliwe mkazo sana katika uendeshaji wa shughuli hii. Ukiangalia kwa upeo malengo na madhumuni utakuta pale kuna jamii imeguswa yaani *social aspect* imeguswa kwa maana ya kwamba yale makundi ya watu wa aina mbali mbali wenye uwezo tofauti, masikini, matajiri na makundi mengine, kwamba yatazingatiwa sana kwenye shughuli zitakazofanyika na Baraza hili, kwani mambo haya ya jamii ndio yale ambayo kwa kweli yakishughulikiwa ipasavyo tutaweza kuendesha shughuli za biashara kwa ufasihi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu huko sasa hivi ukipita mitaani kila anayejenga anataka aweke mlango wa duka, maduka yanaweza yakawa mengi hata mimi nina mpango huo kwamba nikijenga pengine niweke mlango wa duka. Sasa maduka yatakuwa mengi lakini sio kwamba kila anayeweka duka atajitosheleza ni kwamba yeye kuna bidhaa hataweza kuiuza itabidi aende kwa mwenzake akanunue pengine. Kwa hiyo, huyo huyo mfanyabiashara anauza lakini pia ananunua kwengine, ama atanunua kwa *wholesale* au atanunua kwa *retail* kwa mwenye duka mwengine kwa sababu bidhaa hiyo anayo.

Halafu tena mswada huu umegusia suala la *economy* vile vile, sababu ukenda kwenye *economy* utakuta watu wetu wengine kuna masikini wenye uwezo wa kujitibu, wenye uwezo wa kupeleka watoto wao shule, kuna wengine hata watoto wao kule pengine uwezo unawatenga kwenye uwezo wa kufanya mambo mengi ya kijamii. Kwa hivyo, natoa msisitizo kwamba na hii *economic aspect* nayo ishughulikiwe kwa kina, ili hili Baraza letu liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Vile vile, kuna suala jengine la *culture* hapa lakini halikutajwa hapa isipokuwa ukitizama maelezo yake yaliyomo *culture* imetajwa, kwamba kuna mambo ya yetu ya mila, utamaduni haya pamoja na desturi zetu hizi nazo zina umuhimu sana katika kuendeleza biashara. Hivyo, nazo ningependa sana Baraza letu hili lizingatie sana mambo yetu ya mila na utamaduni katika kuziboresha bisahara na kuziendeleza kwa *taskforce.*

Mhe. Mwenyekiti, pia suala la mifumo ya mawasiliano ni muhimu sana katika kuendesha biashara wanaita *communication asset* inawezekana ukawasiliana kwa barua, kwa magazeti, kwa *posters* a na kadhalika ukaweza ku-*promote* au ukaweza kuhamasisha watu au biashara iendelezwe kwa nguvu zaidi. Kwa kweli, na haya ninayoyasema ni muhimu, kwa sababu kunajitokeza mitindo wakati maalum, wakati wa Ramadhani bidhaa zinapanda bei sana kiasi kwamba utaona kama mfanyabiashara anawakomoa walaji wake ambao ni wateja wake.

Sasa, pia na hili Baraza letu liangalie sana shughuli hii ya biashara kuuza kwa bei ya viwango vya juu sana, kwa sababu litafanya utafiti hili Baraza nadhani litajua hasa bei halisi ambayo inastahiki iuzwe, na itajaribu kuwahamasisha watu wasipindukie bei hiyo ambayo inaweza ikauzwa ikamletea tija mfanyabiashara.

Mhe. Mwenekiti, mwisho niliona hapa kwamba pia imezungumzia suala la *mindset* za watu, kila mtu ana mawazo yake juu ya biashara fulani. Kwa hivyo, kama mawazo ya

wengi yatafanyiwa utafiti na kufanyiwa tathmini yakafanyiwa kazi kwa mujibu wa matokeo yaliyopatikana, basi biashara hii itaendelea vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa ninaomba niingie kwenye ushauri wangu kwa Baraza hili la Biashara, ushauri wangu kwa Baraza la Bisahara nadhani umefika wakati sasa hivi kuangalia zile sifa ambazo anastahiki mfanyabiashara bora kuwa nazo ili waweze kuzisambaza kwa watu. Sifa moja ambayo mfanyabiashara anaweza akawa nayo ni sifa ya ukarimu, kwa sababu mteja ni mfalme anapokuja ukamhudumia kwa ukarimu, basi unamfanya arudi tena siku ya pili. Lakini kama ukimtolea maneno na kumuuzia kwa bei za juu na kumkatisha tamaa basi huyo utakuwa umemkosa na biashara yako kwa mtu yule haitaenda na akipungua mmoja akapungua wa pili na watatu biashara hii itakuja kuanguka mwisho wake. Kwa hivyo, nashauri sana wafanyabiashara kwamba zile tabia za undani wa nafsi ule waziache, ili wafanye biashara kwa mashirikiano na wananchi.

Jambo jengine ambalo nataka kushauri Baraza pamoja na kamati zote zitakazokuwepo ni kwamba lazima *proactive*, yaani tuchangamkie shughuli hizi za biashara ziende vile zinavyotakiwa, kwani ukiwa *proactive* utakuwa mkakamavu, utakuwa mbunifu na utakuwa pia kila penye biashara nje ndani kila jambo linalohitaji kuchukuliwa kibiashara basi utalifanyia kazi na litaleta mafanikio.

Vile vile, katika maamuzi mengi ambayo tunayoyafanya, Mhe. Mwenyekiti nashauri sana tuangalie matokeo yake, kama mambo tunayoyafanya utafiti wetu tunaofanya, matokeo yake yatakuwa yenye manufaa, basi hayo tuendeleze, lakini tukiliona jambo ambalo halitaleta manufaa kwa njia moja au nyengine basi nadhani hilo inabidi tuliachie.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nishauri siku zote Baraza na kamati hizi zifanye shughuli zake kwamba Baraza lifanikiwe katika malengo yake ya kuhamasisha watu, na wale watu nao wahamasike nao wahisi kwamba wanafaidika kutokana na Baraza hili.

Jambo la mwisho ambalo ningependa nisisitize ni kwamba Baraza letu hili, Mhe. Mwenyekiti nashauri sana litafute taaluma za kutosha taaluma ziko nyingi sana za biashara duniani humu. Kwa hivyo, tutafute taaluma za kutosha kutoka mahala popote duniani tuziingize hapa, ili biashara zetu ziende kwa utaalam wa hali ya juu sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo narudia kusema kwamba huu ni waraka mzuri, una lengo kabisa la kuiondoa nchi yetu kutoka umasikini na haya ni mabadiliko makubwa na siku zote tunaambiwa tubadilike. Hivyo, hizi pia ni zile c*oncept* za Mapinduzi, kwamba Mapinduzi Daima tunabadilika kila ambapo panahitajika kubadilika tunabadilika kwa faida ya maendeleo yetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja sitaki niende mbali sana kwa sababu muda umekwenda. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Dkt. Makame Ali Ussi. Sasa ninamwita Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na Mhe. Mohamed Said Mohamed ajitayarishe.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame: Mhe. Mwenyekiti na mimi nakushukuru kunipatia wasaa huu jioni hii kuweza kuchangia mawili matatu kama yalivyowasilishwa kwenye mswada wetu huu na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa kweli tumpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi nzuri sana ya mswada, mswada umeandikika vizuri ukiacha makosa ya uandishi tu na kwenye tafsiri. Kwa ujumla, ukiangalia baadhi ya tafsiri kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili kidogo hauku-*reflect* moja kwa moja, kamati wamejitahidi kusahihisha baadhi ya mambo, lakini naona mengine wameyasahau nitajaribu kuyaonesha moja au mawili. Vile vile, naipongeza sana kamati kwa kazi nzuri sana waliyoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe asubuhi kwamba serikali haifanyi biashara, lakini wajibu wake mkubwa ni kutengeneza mazingira mazuri, ili biashara ifanyike, yaani *conducive* and en*vironment,* ili biashara ifanyike vizuri. Sasa *forum* hii ambayo wanaitengeneza kupitia mswada huu, kwa kweli ni *forum* nzuri sana ya kuwakutanisha wafanyabiashara pamoja na serikali, kuona kwamba hayo mazingira mazuri ambayo serikali imeyaweka kweli yanafanywa, yanatekelezeka na yanasaidia biashara, hayo ndiyo mambo ya msingi.

Kwa hivyo, madhumuni makubwa ya ile *dialogue* iliyowekwa kwenye Mabaraza yale, kwa kweli ni jambo la kupigiwa mfano sana. Nakumbuka vikao tulivyoalikwa siku za nyuma ambapo mwenyewe Mhe. Rais anakuwa Mwenyekiti kunakuwa na uwazi kabisa kama walivyozungumza Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunampongeza sana Mhe. Rais, kwa sababu anawaachilia kila mtu aeleze analotaka kwa uwazi kabisa, aulize anachotaka, tulifika mpaka saa 4 au 5 za usiku, kila mmoja anatoa fikra zake, wanatoa yale madukuduku yao. Maana ile *element* ya kuogopana zamani ilikuwepo kati ya serikali na wafanyabiashara, yaani wafanyabiashara walikuwa wakilalamika kwamba tukipeleka mambo yetu hatujibiwi, hatuambiwi. Sasa, *forum* hii inatoa madukuduku kila mmoja anaeleza yake na anajibiwa kwa ufasaha kabisa. Mhe. Mwenyekiti, napongeza sana wazo hili na hasa haya marekebisho haliyofanywa naamini yataisaidia sana sekta yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nichangie kwenye mswada moja kwa moja na naomba nianzie kwenye jila la mswada wenyewe kabisa. Anasema jina fupi na kuanza kutumika. Sheria hii itajulikana kama "Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara", Mswada wa Kiingereza unasema *"An Act to Establish the Zanzibar National Business Council...*" Nafikiri kwa kutafsiri kama ilivyo neno kwa neno haiji vizuri kama ilivyotafsiriwa kwenye Kiswahili. Hivyo, kwenye Kiswahili imesema "Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara". Nafikiri ingekuwa "Sheria ya Baraza la Biashara la Taifa" kwa sababu huko kwenye taifa kuna mabaraza mengi, kuna Baraza la Sanaa, Baraza la Michezo. Sasa hapa kitu tunachozungumzia biashara kwa hiyo iwe "Baraza la Biashara la Taifa" hayo ndiyo maoni yangu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nije kwenye kifungu cha 11 ndiyo, pale niliposema ukiangalia kifungu cha 11 kwenye mswada wa Kiingereza unasema *from the Recognize University* huyo Katibu Mtendaji awe na Shahada ya Kwanza inayotoka kwenye *Recognize University.* Lakini kwa Kiswahili umesema kutoka Chuo, chuo siyo Chuo

Kikuu wala haikutafsiri ile R*ecognize University* kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika. Sasa nilisema kuna vitu vidogo vidogo hivi lakini vina umuhimu wake kuwepo kutafsiri vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, *observation* yangu nyengine kwenye Kamati za Baraza, hizo zipo kwenye kifungu cha 18 anasema

"18. (1) Kutakuwa na Kamati zitakazoanzishwa na Baraza kama itakavyoona inafaa"

Tunakubali na wamezitaja hapa kwa sasa hivi:

a) Kamati ya Uchumi ya Biashara,
b) Kamati ya Utalii, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi,
c) Kamati ya Mambo ya Ajira."

Mhe. Mwenyekiti, nahisi kwa tulivyo sasa hivi na tunakoelekea kuna haja Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Nishati au Mafuta na Gesi hii Kamati lazima tuitaje sasa hivi iwepo. Kwa kweli, tumeshaingia kwenye mambo ya mafuta na gesi, hatuwezi kungoja na kwenye *forum* hizi mambo haya yatajitokeza kwa wingi sana. Hata hivyo, wasema zitaanzishwa haja itakapotokezea, lakini kwa maoni yangu kamati hii bora ianzishwe sasa hivi iwepo kwa uzito wake.

Mhe. Mwenyekiti, jengine hapo hapo kwenye Kamati ya Kilimo, nimeona Kamati imeongezea kwamba mazingira. Ni sawa mazingira ni *cross cutting issue* linamgusa kila mtu. Lakini hapa nafikiri kuna *serious omission* misitu, lazima misitu tuitaje nayo inauzito wake. Mhe. Mwenyekiti, kwenye Kamati ya Kilimo tumejata Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na sasa hivi tumeongeza mazingira, hivyo, ninashauri na misitu nayo iingizwe inauzito wake hapa kwenye kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, *observation* nyengine niliyonayo iko kwenye Kamati zenyewe sasa, kuhusu suala la uwiyano wa wajumbe katika kamati. Tukifungua kwenye jaduweli la kwanza linasema, naomba kunukuu.

"Akidi ya vikao vya Baraza itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe waliohudhuria kikao na angalau asilimia 40 ya wajumbe watoke katika sekta zote mbili, Sekta ya Umma na Sekta ya binafsi".

Nakubali na nafikiri imewekwa wazi kwamba wajumbe wote kila sekta itatoa wajumbe 12 ni suala zuri sana. Lakini ukenda kwenye Kamati za Baraza nafikiri Mhe. Mwenyekiti, kuna matatizo, nafikiri twende kwenye kamati moja moja tukianza na Kamati ya Uchumi, Biashara, Uwekezaji na Kodi, nimejaribu kuwahesabu haraka haraka wajumbe wa *public sector* wapo sita (6) na wajumbe wa *private sector* wapo watatu (3) tu, uwiyano kidogo haupo.

Mhe. Mwenyekiti, nahisi kidogo unajua serikali inapozungumza kwenye kamati kama hizi watu kidogo wengine lazima wata *feeling theriority complex*, haidhuru wataeleza mawazo yao, sasa wakiwazidi kama hivi *more than 50%* kwa kweli haitopendeza. Kwa

hivyo, nashauri sana tufate ile akidi tuliyoizungumza mwanzo kama serikali wapo sita (6) basi na sekta binafsi wawe sita (6) hivyo hivyo, itapendeza na pengine kwenye kamati watapiga kura, sasa kumzidi mwengine kama hivi haitopendeza.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda kwenye Kamati ya Utalii, kuna wajumbe 10 lakini wanane wanatoka serikalini, wawili tu ndio wanatoka sekta binafsi ambao ni *member* kutoka *ZAT* na *ZATO*, wengine wote wanane (8) wanatoka serikalini. Kwa kweli, hiyo *environment* ya *dialogue* haitopendeza kwa hali hii. Kutokana na hali hiyo, ninashauri sana hapa Mhe. Mwenyekiti tuongeze wajumbe kutoka sekta binafsi kwenye kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, ukija kwenye Kamati ya Kilimo hapa haijambo kidogo kuna wajumbe watano (5) kutoka serikalini na wanne (4) kutoka sekta binafsi. Hapa kidogo kuna kitu kimenikanganya, kwenye *version* ya Kiingereza kwenye hiyo Kamati kifungu cha 9 kinasema, *"Head from Zanzibar the Poultry Association."* Kwa Kiswahili tungesema kiongozi wa *association* ya wafuga kuku, lakini kwenye Kiswahili imeandikwa Mjumbe kutoka Chama cha Wafugaji Zanzibar, sio cha kuku. Kwa hivyo, naielekea hii ya Kiingereza ndiyo iliokosewa labda ingekuwa mjumbe kutoka Chama cha Wafugaji Zanzibar *from the livestock sector* vyote ingesahihishwa hivyo ingekuwa barabara. Ndiyo vile nilivyosema tafsiri kutoka kizungu kwenye kiswahili kwenye sehemu nyengine kidogo haikukaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, ukenda kwenye Kamati ya Ajira nayo ina wajumbe 10 saba (7) wametoka kwenye serikali watatu (3) ndiyo wametoka sekta binafsi. Sasa ndivyo nilivyosema ule mjadala au yale mazungumzo hayatonoga kwa *proportion* kama hii. Hivyo, ninashauri sana Mhe. Waziri huu uwiyano kidogo tujaribu kuuongeza ili mambo yaende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla niseme mswada umeandikika vizuri ukiacha haya mambo madogo madogo tu haya, ambayo naamini waandishi wanaweza wakayarekebisha.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono mswada kwa asilimia 99.99. Nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. Sasa anafuata Mhe. Said Mohamed Said na Mhe. Rashid Makame Shamsi, ajitayarishe.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana, lakini nimshukuru kwa aina ya pekee Mwenyezi Mungu na nimuombe sana wakati nikichangia hotuba yako hii asinipe kiburi, tambo wala jazba, niendelee kuchangia katika hali nzuri tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri sana pamoja na wetendaji wake wote. Nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake kwa kazi nzuri waliyotuletea na marekebisho mengi ambayo wameyafanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwenye madhumuni na sababu ya mswada huu. Niseme mswada huu umekuja kwa wakati wake. Mswada huu ni mzuri tena sana, mwanzo tulikuwa tuna Baraza, lakini mimi sitaki kuita kwamba tulikuwa na Baraza kwa sababu tulikuwa hatuna sheria, tulikuwa na barza ya biashara, lakini sasa tukipitisha mswada huu ndiyo tutakuwa na Baraza la Biashara. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Mwenyekiti, huu sasa Baraza hili litatajika au litasomeka kisheria, mwanzo lilikuwa halipo kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza litafungua uchumi wetu lakini litaweka hali sawa kati ya wafanyabiashara na serikali yao, na hili ndilo jambo jema sana. Serikali kuwa wazi kukubali kukaa na wafanyabiashara mambo mengi tunahisi yatafunguka.

Mhe. Mwenyekiti, leo asubuhi niliuliza swali la nyongeza juu ya wafanyabiashara wadogo wadogo hasa wa magari kule Dubai, nilikwenda *physically* nikaiyona ile hali ambayo inayotokea, yule wakala wetu wa vipimo anapelekewa gari na wafanyabiashara wale kutoka kule kwenye *showroom* kufika kwake ni Dola 100, lakini anaweza yule kwenda kuikwamisha kwa ringi tu liko baya, lirudi tena na ikirudi tena ilipe dola 100.

Tuangalie huyu mfanyabiashara mdogo anaweza ku- *afford* vipi. Pengine pamoja na kuleta hapa faida yake ni laki 5 tu, sasa pesa hizi zote. Lakini pamoja na hayo, serikali yetu bado inapoteza mapato mengi sana, asilimia 70 kuiwacha kule asilimia 30 kuja nayo hapa bado tunakuwa na mapato madogo sana. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali suala hili lichukue kwa umuhimu wake mkubwa sana kuona tunaweza kuongeza mapato juu ya biashara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza wafanyabiashara wana malalamiko mengi sana. Kwanza kuna *double taxation* sasa hivi, bidhaa anayotoka kuchukua mtu Bara mtumiaji wa kawaida analipa *VAT* kule asilimia 18 lakini akiingia nayo Zanzibar analipa *VAT* Zanzibar asilimia 18, kwa mlaji wa kawaida asilimia 36, haileti sifa nzuri. Hivyo, labda Baraza hili litaweka muundo mzuri na serikali inaweza tukaona basi tunafika pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, jambo moja linanipa ukakasi sana, sisi ni mahodari sana wa kuunda Sheria Zanzibar na tuna sheria nyingi sana, lakini utekelezaji wetu uko asilimia 2 katika 100, inatupa wasi wasi. Mhe. Mwenyekiti, hetu tutizame katika miaka hii miwili tuliyokuwepo hapa Barazani, kutoka mwaka 2016 tulikuwa na sheria tulizounda sisi Baraza la Wawakilishi 12. Lakini mwaka 2017 tayari tuna sheria nane (8) sheria 20 sasa hivi tunazo. Tumekuwa wazuri sana wa kufanya sheria mbali mbali lakini utekelezaji wake zero au sifuri. Kwa maana hiyo, naomba sana tujitahidi sana kwenda katika malengo ya sheria ambazo tumeweza kuzitunga. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja kwenye mswada wenyewe hiyo ilikuwa ni dibaji tu. Mhe. Mwenyekiti, nilileta *move motion* yangu *shadow of amendment* jaduweli hili nililipeleka na ninamuomba sana Mhe. Waziri tunapotoa maduweli kama haya tusijibiwe kisiasa, tujibiwe juu ya jaduweli tunavyolileta, kwa sababu anaweza akatoka Mhe. Waziri akatujibu tu kisiasa anavyotaka mwenyewe lakini bila ya kujibu hoja. Kwa kweli, akijibu hoja hizi pengine tayari na sisi tutakuwa tumezikubali tutapunguza kupiga

buti hapa tunapokaa kama Kamati ya Kutunga Sheria. Lakini anapotujibu tu kisiasa anazungumza tu pale haielekei, tujibiwe. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye kifungu cha 4 cha mswada huo. Kifungu hichi cha 4 natoa maelezo nimesema kirekebishwe kwa kuondoa neno *ZNBC,* ambalo ufafanuzi wake umetolewa katika kifungu kinachofuata. Kifungu hichi sasa nilipendekeza kisomeke kama ifuatavyo:

> "Kuzingatia jambo jengine lolote ambalo litapelekea kwa Baraza la Taifa la Biashara kufikia malengo yake". Nilipendekeza hilo."

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 5 kilinasomeka, naomba kunukuu.

> "5.(1) Kutaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Taifa la Biashara kwa ufupi litajulikana kama (*ZNBC*)."

Mhe. Mwenyekiti, nimependekeza kufanyiwa marekebisho hapo "Kuanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Taifa la Biashara, kwa ufupi litajulikana kana (ZNBC). Hayo ndiyo marekebisho yangu niliyoyatia hapa, litajulikana kwa ufupi.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda tena kwenye kifungu cha 7,

> "7.-(1) Baraza litajumuisha na wajumbe wafuatao:-
>
> a) Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndiye Mwenyekiti wa Baraza hili".

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais kukubali kukaa na wafanyabiashara. Hata hivyo, hivi hawa wajumbe ambao watakuwa hapa mawaziri kutoka katika sekta mbali mbali sasa ndiyo inaelekea tutaanza kutimiza dhana nzima za *one stop center*, vitu vyote vinaweza vikamalizika hapa hapa kwa mujibu tunavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 110 kwenye kifungu cha 9(j) kifungu hichi naomba nikinukuu kwenye mswada wenyewe kama hivi:

> "9.(j) kuwa na uhusiano au ushirikiano wa Mabaraza mengine ya Biashara kwa lengo la kutafuta ujuzi na kubadilisha taarifa;"

Mhe. Mwenyekiti, nimekwenda kuibadilisha hii na naomba sasa isomeke kama ilivyo. "Kuwa na uhusiano au ushirikiano wa Mabaraza mengine ya Biashara nje ya Zanzibar, kwa lengo la kutafuta ujuzi na kubadilishana taarifa."

Mhe. Mwenyekiti niende tena kwenye kifungu cha 11

> "11.-(1) Kutakuwa na Katibu Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais."

Mhe. Mwenyekiti, kutakuwa na Katibu Mtendaji, sasa sijui hili ni neno la kisheria au vipi, limeanza kunipa ukakasi sana. Wakati Katibu Mtendaji tayari ameshateuliwa wakati sheria hii bado haijapita sijui kama kunamaneno au funga hii inasihi au itakuwa batili tuanze kufunga tena mawili yanawezekana kustaafu.

Mhe. Mwenyeiti, aliyemfundisha chui kula binadamu, ni binadamu ndiye aliyemfundisha chui kula binadamu. Sasa leo kabla ya sheria haijapita labda Mhe. Mwanasheria Mkuu aje anifahamishe sifahamu, ningeomba niache kitendawili hiki ambacho nashindwa kukitegua katika akili yangu.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye kifungu cha 12 nilifanya marekebisho kifungu cha 12(C)(iv) kwenye mabano yake kinaendelea vile vile. Mhe. Mwenyekiti, nilipendekeza kuwandaa na kuweka kumbukumbu za vikao vya Baraza za kamati zake, kuandaa sasa hiki huku kimesema kuweka kumbukumbu za vikao vya Baraza pamoja na Kamati zake, lakini nikabadilisha na nikapendekeza kuandaa na kuweka kumbukumbu za vikao vya Baraza na Kamati zake.

Mhe. Mwenyekiti, niingie sasa kwenye kifungu cha 20 (C). Mhe. Mwenyekiti, nasema Kamati ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi ina wajibu wa yakatajwa mambo mengine, lakini nikaanza kuweka vitu vyengine nikasema kupendekeza hatua ilikuwa hii ni C (iv) kupendekeza hatua za kutatua matatizo yote katika sekta zote hii, sasa nikapendekeza naseme iwe hivi kama ilivyo kupendekeza hatua za kutatua matatizo yote katika sekta hizi na inaendelea mbele.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kwenye kifungu cha 27(3) kwenye mswada huu vinasomeka vitabu vya hesabu vitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali au mtu mwengine yoyote aliyemuidhinisha na vitakaguliwa angalua mwisho wa mwaka wa fedha. Vile vile, hapa nimetoa mapendekezo mengine nikasema vitabu vya hesabu vitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwengine yoyote aliyemuidhinisha miezi mitatu, baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 119 katika fasili ya 4 kwenye *paper* hii inasema endapo kwa maoni ya Mwenyekiti au Mjumbe yeyote wa Baraza ikiwa kuna jambo linaonekana ni la haraka na la dharura haliwezi kusubiri utaratibu kuja kujadiliwa katika vikao vya Baraza, jambo hilo linaweza kujadiliwa na kutolewa maamuzi katika ngazi ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, hapa niseme tu tumekwenda vizuri sana napo lakini ya nne nimeleta marekebisho kidogo nimesema hesabu zitakaguliwa na Ripoti ya Mkaguzi itawasilishwa katika Baraza sio chini ya miezi sita baada kumalizika kwa mwaka wa fedha. Mhe. Mwenyekiti, sasa hii nimerekebisha hapa, ili aone Mhe. Waziri kama ipo sababu na nia atakayoiona inafaa basi itakuwa vyema sana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niruke kwenye mswada huu kwenye *paper* namba 121 katika jadweli la 3 wametajwa Wajumbe wa Kamati ametajwa Waziri mwenye dhamana ya Biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo, Waziri wa Fedha, Waziri wa Ardhi na wote lakini kumetajwa Mwenyekiti wa Makampuni ya Bakhresa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa napata ukakasi hii sheria hii tunamtungia mtu mmoja au tunatunga kwa mapenzi, kwa nini tusiweke Jumuiya ya Wafanyabiashara na Wakulima Mwenyekiti wake, ambao wote wainakusanywa pamoja tumtaje tu Mwenyekiti wa Makampuni ya Bakhresa. Hivyo, kwa nini hatumtaji Mwenyekiti wa Makampuni ya *VIGO*, Mwenyekiti wa Makampuni mengineyo, kwa nini tumtaje Mwenyekiti wa Makampuni ya Bakhresa, hatuwezi kumtungia mtu sheria hii. Mhe. Mwenyekiti, lakini tukiwa na mapenzi makubwa pengine siku mmoja tukasema tuanza kumuanzia serikali hii angalau kwa mwezi mmoja aiendeshe haya ndio mapenzi, hayo ndiyo mapenzi yakuweza kuweza kutungia sheria kama hiyo. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nimesema nimebadilisha baadhi ya vitu, lakini baadhi ya viti sikubadilisha nimependekeza, na pendekezo hili linaweza kukubalia au kukataliwa. Lakini, tukiwa tunatakaa na tukiwa tunajadili tuweze kujadili kwa kitu kizuri na tusijibiane mipasho.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunivumilia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Omar Seif Abeid ajitayarishe.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Naam ahsante sana Mhe. Mwenyeiti, kwa kunipa nafasi hii alau nichange machache juu ya Mswada huu uhusianao na Baraza hili la Taifa la Biashara.

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, na niwapongeze wajumbe wote ambao kwa kweli wamechangia vizuri katika kufanya mswada huu ukae vizuri zaidi.

Vile vile, nimshukuru na nimpongeze Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuweza kuleta mswada huu ambao ni muhimu sana kwa taifa letu. Wenzangu walitangulia kusema hususan Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwamba mswada kwa kweli umechelewa na Mhe. Mohamed Said Mohamed alisema mwanzo tulikuwa na Barza hivi sasa tutakuwa na Baraza, kwa sababu tokea serikali ijivue katika kuendesha biashara, maana yake pale ndipo ambapo palistahiki sasa kuweza kuunda hasa Baraza la Biashara kisheria kwa hiyo muda umekwenda.

Hata hivyo, mswada huu tukiupitisha basi utakuwa muwaruaini tosha katika suala zima la kuondosha kero za wafanyabiashara wetu sambamba na kuweze kukuza uchumi wa taifa letu, kwa sababu asilimia kubwa sana ya mapato ya serikali yatagemea sana shughuli za wafanyabiashara mbali mbali.

Kwa hiyo, kuwepo kwa majadiliano na *forum* katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, hii itaweza kufanya wafanayabiashara wetu, basi wawe na sehemu ya kuzungumza na hatimaye kero zao kundoka na kuweza kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kuweza kuongeza kipato katika taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika mswada wenyewe nikuwa na michango sio mingi, kwa sababu wenzangu waliopita wameweza kuchangia vizuri tu, isipokuwa nikazie kazie katika baadhi ya mambo ambayo nahisi kuyapa kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, nikija ukurasa aya 108 katika ufafanuzi wa maneno, mara nyingi huwa narejea wanasheria wetu huwa wanasahau, tunanza kutunga miswada hii kwa lugha ya Kiingereza unapo angalia katika lugha ya Kiingereza, basi maneno haya yamepangika vizuri kwa *alphabet order,* lakini tunapogeuza sasa kuja lugha ya Kiswahili huwa tunasahau kuweza kuyapangilia vizuri. Kwa hiyo, ningependa sana maneno hayo ambayo yametolewa ufafanunuzi, basi sasa yapangwe katika mtiririki wa *alphabet order*.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 109 katika kifungu cha 4 (e) kuna neno ambalo katika kamusi yetu ya Kiswahili hapa Zanzibar neno hili halimo neno uboreshaji, ningependa sana tuliondeshe na badala yake sentesi hiyo isomeke hivi

"kutathmini na kupendeza mfumo bora zaidi wa sera za kimazingira inaendelea,
na tuweze kuondosha neno uboreshaji"

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kifungu cha 5, mara nyingi mimi ninakuwa sijui nachang'anyikiwa tunapoleta ufupisho tunatizama lile neno la Kiingereza au tunatizama neno la kiswahili, kwa sababu huu mswada kwa hapa unasomeka kwa kiswahili, yaani Baraza la Taifa la Biashara na iwepo Zanzibar hapo ndio itakuwa imekamilika, Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar, hivyo naomba ikae Zanzibar hapo. Kwa mfano, hata hii *ZNBC* maana yake ipo Z, Z ina *represent* Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hili neno la kiswahili Zanzibar hapa haipo na tunapotoa ufupisho sasa tunatazama ile ya kiingereza au tunatizama hii ya kiswahili naona kama tunajichanganya, kwa hiyo kama tunatumia kiswahili basi isomeke BTBZ hiyo ndio itakuwa inaleta ufupisho lakini tuna *refer* ya kiingereza, basi sawa lakini hiyo ya kiswahili neno Zanzibar liwepo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoa hapa nakuja katika kifungu cha 7. Mhe. Mwenyekiti, kuna muundo wa Baraza lenyewe. Baraza litajumuishwa na wajumbe wafuatao kuna vifungu cha kwanza (a), (b) na (c). Sasa kifungu (c) kina wajumbe 12 ikimeainisha wajumbe 12 kutoka Sekta Binafsi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa kwamba hivi sasa wenzetu kinamama wamechangamka sana katika biashara hakuna biashara ambayo hawafanyi, kama ni biashara ya kwenda nje kinamama wanafanya, kama biashara ndogo ndogo viwanda wanafanya. Kwa maana hiyo, naomba sana katika wajumbe 12 hawa basi angalau 4 basi wawe ni wanawake na iwekwe wazi hasa, kwa sababu mara nyingi tunaona kwamba mfumo dume unatawala katika vyombo mbali mbali. Kwa hiyvo, tusipongiza hapa kabisa tukaweka kinga tutakuja kuta mfumo dume unatawala katika hiki chombo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika ukurusa vile vile 112 kifungu cha 15 katika Kamati Tendaji. Hapa pia wimbo wangu ni huo huo Kamati Tendaji inajumuisha wajumbe 10. Naomba isemwe katika Wajumbe 10 basi angalau 3 wawe wanawake, ili tuweze kuleta

uwiyano wa kijinsia katika vyombo ambavyo vinatoa maamuzi, na hususan tukiangalia kwamba katika biashara basi wenzetu wanawake na wao wana mchango mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurusa wa 114 katika kifungu cha 4 ambacho kinasema bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha 3 cha kifungu hiki Bodi inaweza kuanzisha kamati nyengine yoyote inaendele. Hapa Mhe. Hamza Hassan Juma alisema na mimi bora nisisitize, hii bodi katika mswada huu ndio kwanza hapa inaonekana neno bodi, kwa hiyo hatujui bodi hii imetokea wapi. Hivyo, namuomba Mhe. Wazari wakati atakapokuja kufanya majumuisho aweze kutoa ufafanuzi kamili juu ya bodi hii, na kama ipo basi kwenye maneno ya ufafanuzi basi itolewe ufafanuzi kwamba hii ni bodi fulani, ili tuweze kuifahamu vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije sasa katika ukarasa wa 117 kifungu cha 14 fasili ya 3. Mhe. Mwenyekiti, kumeachwa maneno hapa ambayo napendekeza yaingizwe katika baina ya neno kufanyika na itakapo hitajika palikuwa na maneno isomeke wakati wowote itakapohijika, kwa mujibu wa *version* ya kiingereza ilisema *anytime your deem necessary* kwa hiyo hicho kitu kimekosekana naomba kiingizwe hapa wakati wowote itapohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika ukurusa wa 121 katika jadweli ya 3. Katika jadweli hii *statement* ambayo ni namba 1 ambayo inaelezea muundo wa wajumbe wa kamati utakuwa kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia *version* ya kiingereza inasema *the types and composition of committee shall be the follow* kwa tafsiri isiyo rasmi maana yake aina na miundo wa Kamati utakuwa kama ifuatavyo, kwa tafsiri isiyo rasmi lakini itakuwa ni nzuri zaidi kuliko iliopo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamesema sana juu ya muundo wa kamati hizi. Kwa upande wangu ninasisitiza kwamba kamati hizi zinahitaji kuangaliwa upya kama tunataka kuwe na *forum* nzuri kati Sekta Binafsi na Sekta ya Umma hizi kamati hazina uwiyano wa wajumbe wake hazina uwiyano kabisa. Kwa hiyo, yanapofanyika maamuzi ambayo yatabidi yapigiwe kura, basi mara zote Sekta Binafsi watashindwa, wakati Sekta Binafsi wao ndio wenye muhimili wa biashara. Sasa huwezi ukawa na *forum* ya wajumbe hii kwa mfano Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini alisema, vile vile Mhe. Abdalla Maulid Diwani alisema huwezi ukawa na majadiliano katika kamati unakuta wafanyabiashara au watu wa Sekta Binafsi 3 lakini Sekta ya Umma wako 10. *(Makofi)*

Nadhani hapa pakiwa na kura maana yake hawa unawaonea. Kwa kweli, hapo maana yake tunasahau nini lengo la kuunda Baraza lengo ni kwamba Sekta Binafsi iweze kukaa na Sekta ya Umma, katika kuweza kujadili mambo yao na hatimaye tuweze kukuza uchumi. Kwa hivyo, kamati zote hizi naomba kupendekeza zifumuliwe upya, ili tuweze kuwaingiza vile vile idadi ya wajumbe ambayo itakuwa na uwiyano kutoka Sekta Binafsi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hapa vile vile kuna masahihisho kutoka tafsiri ya kiingereza kuja tafsiri ya kiswahili. Wenzetu kamati niwapongeza sana ambayo imeweza kufanya

marekebishao na mapendekezo wao waliliona neno *Minister*, kwa sababu ilisema katika baadhi ya hizi kamati kuna Waziri wa Fedha, Waziri wa Ardhi wenzetu wameliona hili wakaweza kupendekeza kwamba waziri mwenye dhamana ya ardhi, waziri mwenye dhamana ya fedha, hiyo ndivyo inavyotakiwa isomeke na hata kwenye *version* ya kiingereza iko hivyo *the minister have responsible*.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala zima la makatibu hili linataka kuweka sawa. Kwa mfano, katika kamati hii ya mwanzo Katibu Mkuu kutoka Wizara aya Biashara, inatakiwa isomeke kwamba ni Katibu Mkuu kutoka Wizara yenye dhamana ya Biashara na Katibu Mkuu kutoka Wizara yenye dhamana ya fedha kwa sababu hizi wizara kama alivyotangulia kusema Mhe. Jaku Hashim Ayoub zinabadilika. Kwa mfano, hivi sasa hatuna Wizara ya Fedha tuna Wizara ya Fedha na Mipango, kwa hiyo utakaposema Wizara ya Fedha pia itakuwa ni makosa, na unaposema kutoka Wizara ya Biashara maana yake vile vile tunarudi kule kule.

Kwa hiyo, Katibu Mkuu kutoka wizara yenye dhamana ya biashara, Katibu Mkuu wizara yenye dhamana ya fedha na tunapokuja Kamati ya Utalii tunakuta na hayo hayo Katibu Mkuu mwenye dhamana ya ardhi, Katibu Mkuu mwenye dhamana ya utalii. Na tunapokuja katika Kamati ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi Katibu Mkuu mwenye dhamana ya kilimo, na tunapokuja katika Kamati ya Masuala na hapo napenda iwekwe wazi kidogo wajumbe wa Kamati ya Masuali, sio masuali ni masuala yanayohusiana na ajira.

Vile vile, kuna hiyo Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi basi isomeke kwamba Katibu Mkuu wa wizara yenye dhamana ya kazi. Na Katibu Mkuu Wizara ya Utumishi wa Umma isomeke Katibu Mkuu wizara yenye dhamana ya utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya michango hiyo michache basi na mimi nichukue fursa hii kuunga mkono mswada huu asilimia mia kwa mia. Lakini yale mapendekezo ambayo ninayatoa yakiwa ni masuala ambayo yatasaidia basi yaweze kuzingatiwa, ili mswada wetu huu ukae vizuri zaidi kwa maslahi ya taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa ninamwita Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Hidaya Ali Makame ajitayarishe.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nachukua fursa hii adhimu kukushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuchangia kidogo tu katika mswada huu mzuri ambao umeletwa mbele yetu.

Mchango wangu leo ni wa kusaidia tu, yaani ushauri wa baadhi ya mambo. Kwa kweli, mswada ni mzuri unahitaji kufanyiwa kazi mle ambapo mimi nilikuwa nataka kupita kidogo Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kamueleza kwa kina na mimi nimemuona, Mhe. Rashid Makame Shamsi kamuona na kamzungumzia ambazo ndio sehemu zilizogusa hasa maudhui na mantiki ya mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu, Waheshimiwa Wajumbe wote waliomo katika Baraza hili, wananchi, wafanyabiashara pamoja na wanaotusikiliza wanaoliangalia Baraza lako hili, kwamba baada ya mswada huu wa sheria kukamilika ukawa sheria mambo mengi

ambayo yalikuwa ni vikwazo kwa wafanyabiashara yanaweza yakatatuka. Hilo ni jambo ambalo ndio matumaini ya Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na vilio na bado mpaka leo vipo vya wafanyabiashara wetu kuhusiana na malipo ya kodi, pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na serikali za kulitatua tatizo hili la kulipa mara mbili. Lakini kilichonifurahisha zaidi katika mswada huu ambao upo hapa ni kile kilichopo katika *page* hii ya 109 kifungu cha (e) ambacho kinasema kutathmini na kupendekeza uboreshaji wa sera za kimazingira ambazo zitawavutia wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kuficha nchi yoyote ulimwenguni inahitaji wawekezaji. Mhe. Simai Mohammed Said aliyazungumza kwa kina suala la uwekezaji, na suala hili bila ya kuwawekea mazingira mazuri, wawekezaji watatukimbia watakwenda nchi nyengine. Sasa, ili tuweze kuwadhibiti wawekezaji ni kuwawekea mazingira bora. Tuwawekee mazingira bora yatakayowavutia wawekezaji wawe na hamu ya kuja kuekeza, ili nchi yetu ipate faida kutokana na uwekezaji huo. Lakini vyenginevyo tutatangaza uwekezaji na wawekezaji watakuja, na pale watakapoona kwamba tumeshindwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji, basi wawekezaji watatukimbia na hatimaye tutakuja kukosa hata kile kidogo tulichokuwa tunakitegemea kukipata. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani. Kwa, sababu wawekezaji anapokuja huwa haridhiki kuja kuona leo anapanda ofisi hii anapanda ngazi, kesho anapanda ngazi ofisi nyengine, keshokutwa anapanda ngazi anaambiwa nenda *ZIPA,* akitoka *ZIPA* nenda ardhi, akitoka ardhi fedha, akitoka fedha wapi sijui lile mwekezaji huwa halimjengii picha nzuri anaona kwa nini niwekeze Zanzibar, kwa nini nijisumbue, kwa nini nisiende kwenye nchi nyengine wakati mimi nina fedha yangu nikenda nikaekeza. Mhe. Mwenyekiti, leo wenzetu Wanyarwanda wanapiga hatua kubwa kutokana na uwekezaji, na sisi Zanzibar tunayo mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji, kwa sababu ni nchi ya kisiwa tofauti na wenzetu waliopo kati kati ya Bara. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nainasihi bodi baada ya kumaliza mswada huu ukawa sheria na ikaanza kufanya kazi, basi iyatizame mambo haya na iweze kutatua changamoto zinazowakabili wawekezaji. Sambamba na hilo naomba kutoa wito, kwamba tusisubiri mpaka hiyo bodi, Marehemu Mzee Karume alisema linalowezekana leo lifanywe leo. Nampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwa sababu nimo kidogo kidogo katika mambo haya naona baadhi ya usumbufu tunaoupata na yeye mwenyewe anajaribu kusukuma mbele, ili kuwavutia wawekezaji wasogee. Kwa hivyo, naomba na zile taasisi nyengine ambazo zinahusika na mambo haya, zibadilike zifate utaratibu kwa mujibu wa sheria tuliowawekea waweze kufanya wawekezaji wakawa na imani ya kuekeza katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine zuri ambalo nimeliona katika mswada huu ni pale inapozungumziwa kamati. Tukizungumzia hizi Kamati kama ya Biashara, Kamati za Uchumi kuhusu mambo ya bandari. Leo ulimwenguni bandari inakuwa ndio kichocheo kikubwa cha kukuza biashara. Kutokana na hali hiyo, pia ni budi kwa upande wa bandari wakatoa huduma bora. Vile vile, naomba kupendekeza kitu kimoja ambacho nakiona na nitoe wito kwa wafanyabiashara wetu kwamba kuitumia *EPZ* (*Export Processing Zone*) pale Maruhubi tunayo.

Kwa kweli, sidhani kama wafanyabiashara wetu wengi wana uelewa wa kuitumia ile *EPZ*. Lakini pia kwa upande wa serikali walitakiwa kuboresha yale mazingira ya pale *EPZ*, kwa sababu eneo lile leo kama utaliwekea kontena kwa ajili ya wafanyabiashara watoe mizigo yao wakaiweke pale, ili watakapopata soko wakalipe kodi ndio watoe mizigo yao, basi eneo lile ni dogo mno na wala halitoshelezi hata robo ya dhamira ya kuwa na *EPZ*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano, wenzetu ukienda kama pale Mombasa wanayo *Export Processing Zone* zaidi ya nne ambazo ni kubwa mara nne au mara tano hatujafikia huko. Lakini ni vyema tukaitanua na tukatoa elimu tukawashajihisha wafanyabiashara wetu wakaweza kuitumia ile *EPZ* pale Maruhubi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nimefurahishwa kutajwa kilimo, leo kilimo ni biashara na kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yoyote ulimwenguni. Lakini ni jambo la kusikitisha kwamba leo wakulima wetu hatuna hata benki moja ya wakulima hapa, hatuna hata benki moja ya wafanyabiashara, ambapo anajua mfanyabiashara mimi kama ni mfanyabiashara niende kwenye benki yangu ya biashara nikatafute mkopo ambao utaniendeleza mimi mfanyabiashara. *(Makofi)*

Kwa kweli wafanyabiashara njia yao ya kukuza biashara ni kuwa na Benki ya Biashara inayosomeka benki ya biashara kwa maana benki ya wafanyabiasha. Naishauri bodi wakati itakapoundwa kuweza kushawishi taasisi za fedha, kufungua benki, kwa ajili ya wafanyabiashara iweze kutoa mikopo ya riba nafuu, ili wafanyabiashara wetu wakubwa na wadogo waweze ku-*afford* mikopo ambayo inatolewa na benki hizo.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika kwa upande wa kilimo wenzetu Bara kule wanayo Benki ile ya Maendeleo na Ushirika Vijijini *CRDB*, lakini sijui kwa nini leo. Kwa mfano, mtu anawezekana akawa na shamba la shilingi milioni mia tano lakini benki hawalikubali hata kutoa dhamana ya mkopo wa milioni 20, kwa nini? Badala yake benki inang'ang'ania kuchukua nyumba, ukishindwa wachukue nyumba wakauze au wakapige mnada nyumba jambo ambalo si sahihi. Naiomba sana bodi hii pamoja na serikali iangalie mambo haya kwa mujibu wa mustakabal wa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kabisa kwa mambo yaliyoelezwa humu katika dhamira ya huu mswada tulionao leo, unaweza kubadilisha mambo mengi sana ambayo yataleta maslahi kwa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar kutokana na imani aliyonayo ndio maana akaliona kwamba hili lina umuhimu wa aina yake sasa kulianzisha.

Kwa upande wangu mimi naunga mkono mswada huu na nawaomba wenzangu tuunge mkono, tuupitishe mswada na tuwakabidhi majukumu bodi ya kuweza kusimamia yale ambayo yameletwa kwa mujibu wa sheria waweze kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya natamka kwamba mimi naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Omar Seif Abeid. Sasa ninamwita Mhe. Hidaya Ali Makame na baadaye Mhe. Amina Iddi Mabrouk ajitayarishe.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia machache juu ya Mswada huu wa Sheria ya kuanzishwa Baraza la Taifa la Biashara na kuweka pamoja na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu wakati muafaka, na wakati ambao ulimwengu umepamba moto na umechakarika zaidi kuhusiana na masuala haya ya kibiashara.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja nianze na mchango wangu kwa kwenda kifungu Nam.7 ukurasa wa 109 Baraza litajumuisha na wajumbe wafuatao.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna vipengele (a), (b) na (c) lakini katika kipengele (c) kuna wajumbe 12 kutoka sekta binafsi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wajumbe hawa watakaoteuliwa ni 12, lakini haikusema jinsia hapa isikuwa nanapenda sana ikazingatia *gender*, kwa sababu mawaziri wataingia kutokana na wadhifa wao wa uwaziri, lakini hata tukiangalia huko kwenye uwaziri wanawake ni wachache zaidi. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri hapa ikazingatia pia *gender*.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu Nam.15 tunalikuta suala hili hili la uzingatiaji wa *gender* katika kifungu (b) hapo. Vile vile, namuomba sana Mhe. Waziri nalo suala hili likaangaliwa kwa uzingatiwaji wa *gender*.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama *special* kwa ajili ya kuangalia hizi *gender* na nimeusoma mswada huu na nikaona kwamba kuna haja Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri akatuangalia wanawake, kwa sababu wanawake sasa hivi kwa kweli hatuhitaji kukaa kitako, isipokuwa wanawake tumeamua kujitolea katika kufanya kazi. *(Mkofi)*

Kwa hiyo, kwa vile tumejitolea na kwa kuwa tunaweza na tumeonesha nia, kwa sababu biashara tunafanya nyingi tu kama utazingatia na kama utaangalia huko nje wafanyabiashara wengi wao sasa hivi msururu mkubwa basi na wanawake tuko nyuma hatujakaa kitako na wala hatujajiacha. Hivyo, katika Mabaraza yote haya ambayo yameorodheshwa katika sheria hii, basi namuomba sana Mhe. Waziri akatutizama kwa vile yeye mwenyewe ni mwanamke, basi na sisi tukapata kuingia zaidi ili tukawa wengi tukazidi kusaidiana kazi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nakwenda kwenye ukurasa wa 117 katika kifungu Nam.24 ambacho kinasema, naomba kunukuu.

> "kutakuwa na Jukwaa la Biashara la Baraza ambalo litakuwa na muundo ufuatao..."

Mhe. Mwenyekiti, katika huu muundo umeundwa una vifungu saba hapa, lakini katika kifungu (d) wajumbe kutoka jumuiya ya wafanyabiashara. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba wafanyabiashara sasa hivi wamegawika katika sekta mbali mbali, lakini hapa jumuiya hii hatujajua ni jumuiya ipi ambayo itaingia hapa katika hili Baraza.
Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho angalau atufafanulie hawa wajumbe ambao wataingia hapa ndio wepi, hawa jumuiya ya wafanyabiashara kwa vile ndio tunajua hizi jumuiya zipo nyingi na wafanyabiashara pia wapo wengi. Ingawa na chini huku katika kifungu (f) kimefafanua pia kwamba kutakuwa na wafanyabiashara wengine kama Baraza litakavyoamua. Sasa, hilo Baraza litakapoamua basi liwaangalie na wafanyabiashara wadogo wadogo, kwa sababu na wao wana haki zao lakini pia nao wana mahitaji ambayo yakutaka kusonga mbele kimaendeleo, pia kukuza zile biashara zao, ili siku zote wasiwe wafanyabiashara wadogo wadogo na wao ipo siku watokee kuwa wafanyabiashara wakubwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia hapo hapo katika kifungu Nam.24 katika kifungu Nam.3 kuna Jukwaa la Baraza litafanyika kwa mwaka mara moja. Lakini pia akaendelea kusema kwamba litafanyika kwa siku ambapo labda itabidi litafanyika tena hilo Baraza. Lakini endapo haikubidi Baraza hili litafanyika kwa mwaka mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri sijui waliliangalia vipi suala hili kwa sababu kama tunavyojua biashara ni biashara, yaani biashara ni kitu cha kubahatisha huwezi kufanya kama siku zote ukawa na uhakika kwamba siku zote nitaingiza. Changamoto zinatokea siku zote na migogoro na kila kitu, lakini pia kuna faida ndani yake.

Kwa hiyo, naomba kupendekeza kwamba hili Baraza lisiwe mara moja kwa mwaka, endapo kuwa itatokea changamoto hata kama kasema kwamba ndio litafanyika baadhi wakati kama itatokea hiyo dharura, dharura inatokea muda wowote. Je, endapo kama itatokea dharura kwa mwaka mara tano au sita. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti naomba hapa kwa maoni yangu kwamba hili Baraza angalau lifanyike misimu miwili ndani ya mwaka, iwe mwisho wa mwaka labda na kati kati ya mwaka.

Kwa kweli, kuna mengi ambayo yataibuka pale watapokutana, lakini pia kuna maoni mbali mbali yatajitokeza endapo kuwa hawa watu wote watakuwa wamekusanyika pale, yaani wadau kutoka katika majukwaa tofauti watakusanyika pale kutoa maoni na michango yao. Pia kukutanisha zile changamoto zao na faida na hasara kuna mengi yatakayoibuka, lakini kuna mengi ambayo watakuwa tayari wao kama wao wameshayaona, ili kuyafanyia marekebisho au matengenezo.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nimalizie kuhusu suala la uwiyano. Mswada huu wote mzima ni mzuri, uko sawa na unakwenda na wakati. Lakini namuomba sana Mhe. Waziri

uwiyano wa wajumbe kati ya wajumbe kutoka sekta binafsi na wajumbe kutoka sekta ya umma basi uwe unalingana, utakapolingana huu uwiyano ukawa sawa hakuna atakayemburuza mwenziwe, watu wote watatendeana haki na watu wote watakwenda sawa katika misingi yao ambayo watakuwa wameiweka wenyewe na kuifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia niseme kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu aupitishe kwa salama na amani, ili wafanyabiashara wetu wote wafanye kazi kwa mashirikiano na kuitendea mema nchi yetu ya Zanzibar na kuijalizia mapato mengi, ili wananchi tufaidike na tuendelee kuishi kwa amani na utulivu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hidaya Ali Makame. Sasa namwita Mhe. Amina Iddi Mabrouk na baadaye Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) atatufungia mjadala wetu.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kunijaalia kusimama hapa mbele ya Baraza lako hili tukufu. Vile vile, nichukue nafasi hii adhimu kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mswada huu muhimu sana kwa taifa letu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na watendaji wake wote kwa kuleta mswada huu muhimu, ambao utasaidia sana kuimarisha maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi sana, kwa sababu mengi yameshazungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe waliopita na kama Kanuni zetu zinavyosema tuepushe sana kurejea rejea.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba katika nchi yoyote basi hakuna maendeleo yatakayopatikana ya kiuchumi na kijamii bila ya mashirikiano kati ya serikali na sekta binafsi. Hata hivyo, sote ni mashuhuda kwamba wafanyabiashara wetu wanavyopiga kelele katika kulalamika kwamba kodi zimekuwa nyingi na pia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa pili wa serikali niipongeze sana serikali kwa namna inavyojitahidi kukusanya kodi kwa wawekezaji, lakini pia kwa wafanyabiashara. Hii yote kwa kuwa wana nia nzuri lakini pia wana nia ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

Hata hivyo, serikali nayo inasikitika sana na kulalamika kwamba wawekezaji na wafanyabiashara wanakwepa kodi sana. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti naamini kuletwa kwa sheria hii, itasaidia sana kuweza kuwaunganisha kati ya wafanyabiashara na wawekezaji lakini pia na serikali, ili iweze kutatua matatizo ambayo yanawakabili.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo ninaamini kwamba sekta binafsi ina malengo ya kuleta maendeleo ya nchi yetu na watu wake, lakini pia na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo pia ina nia kubwa ya kuongeza pato la nchi yetu. Hivyo basi, naamini na

haya ninayoyasema yanatoka ndani ya moyo wangu kwamba mswada huu kama utafanyiwa kazi ipasavyo, basi matatizo haya yataweza kupungua kwa asilimia kubwa au kumalizika kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo niingie katika ukurasa wa 116. Naipongeze sana serikali kwa kuona kwamba Wakuu wa Mikoa wote husika watakuwa Wenyeviti wa Baraza la Mikoa, naamini kwamba serikali inatambua kuwa katika mikoa yetu husika hasa ndio uchumi wa nchi yetu unakopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilikuwa nina pendekezo dogo tu, kwamba kwa kuwa Wakuu wa Mikoa ndio watakuwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Mikoa, basi ni vizuri wakuu hao wawe Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa. Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kama mswada huu unavyoeleza kuwa uchumi wa nchi hii, unakuwepo chini kwenye mikoa yetu na kule kwenye mikoa yetu kama ulivyoeleza mswada huu kwamba Wakuu wa Mikoa ndio watakaokuwa Wenyeviti wa Mabaraza haya ya Mikoa. Hivyo, ni busara na ni vyema Wakuu wa Mikoa hawa basi waingizwe wawe wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa, ambalo Mwenyekiti wake atakuwa Mhe. Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyozungumza mwanzo kwamba sitokuwa na mengi, kwa sababu mengi yameshazungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe waliopita. Kwa hiyo, niseme kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Amina Iddi Mabrouk. Sasa namwita Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) ambaye atakuwa ni mchangiaji wa mwisho katika meza yangu.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi lakini kwanza napenda nimpongeze Mhe. Rais wa Zanziba na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufikia wakati wa kwamba sasa Zanzibar kuwe na Baraza la Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, awamu nyingi zimepita katika nchi yetu na awamu zilizopita zilikuwa zikiendeshwa na *Chamber of Commerce,* haya yalikuwa yapo kwa ajili ya kuendesha shughuli za biashara. Lakini lazima ifahamike kwamba katika nchi yoyote kuna wafanyabiashara, wauza maduka na wajasiriamali. Haya mambo tofauti haya huwezi kuwa mjasiriamali ukawa mfanyabiashara, wewe utakuwa mjasiriamali na huwezi ukawa muuza duka halafu ukawa mfanyabiashara. Lakini sasa Zanzibar imefikia hatua ya kuwa na wafanyabiashara, kwa sababu Zanzibar ilikuwa na wafanyabiashara wachache mno ambao kwa mujibu wa taratibu za wafanyabiashara walikuwa hawawezi kutangazwa rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, unapomuona Rais wa nchi anayekuja Zanzibar na *delegation* ya watu mia au watu 30 au 40 wale ni wafanyabiashara. Hivi karibuni hapa tulimuona Mfalme wa Morocco alikuja na watu wengi mno na magari na kila kitu, wale ni wafanyabiashara, wengine wakaingia kwenye Serengeti, wengine wakaenda katika mbuga za wanyama na hata yeye mwenyewe akawekeza hapa Zanzibar, maana yake ni kwamba nchi lazima iwe na Baraza la Wafanyabiashara.

Sasa Baraza la Wafanyabiashara kwa kawaida duniani linaongozwa na mwenyewe Rais wa nchi au Mfalme wa nchi ndiye anakuwa Mwenyekiti wa lile Baraza, halafu baadaye ndio huko chini kunakuwa na hizo *Chamber of Commerce*. Kwa hiyo, tunapofikia hatua ya kuwa na wafanyabiashara ambao watasimamiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hili ni jambo la kujivunia na kuona kwamba sasa tumefikia pahala pa kuwa na matunda ya Mapinduzi yanakuja kidogo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, matunda ya Mapinduzi si embe na mafenesi, isipokuwa matunda ya Mapinduzi ni maendeleo yanayowasogeza Wazanzibari kwenye hatua mbali mbali za maisha bora. Sasa kwa harakati hizi ambazo anazichukua Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi za kutaka kuona kwamba Zanzibar sasa ina Baraza la Wafanyabiashara, na kweli umefika wakati muwafaka. Kwa kweli, kuna makampuni ya mwani hapa Zanzibar yanawekeza Lindi, Mtwara, Kilwa na Mafia, mimi mwenyewe binafsi nayajua yapo hapa Zanzibar, lakini yamewekeza huko, maana yake sasa tumekuwa na wafanyabiashara.

Vile vile, hapa unaondoka mwani wa zaidi ya US$ 400,000 kwa mwezi, yaani kunakuwa na utaratibu wa ku-*export* na ku-*import,* hapo ndio unapata wafanyabiashara. Sasa kama tutakuwa na wauza maduka halafu tukasema kwamba sisi tunataka tuwe na wafanyabiashara hicho kitu haiwezekani, lazima nchi iwe ina-*export* na ku-*import* hapo ndio utapata wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mfano uliotolewa wa mfanyabiashara mmoja ambaye sitaki kumtaja jina huu ni mfano tu wa mfanyabiashara, lakini wako wafanyabiashara ambao tayari wana-*import* na wana-*export* tayari wanajulikana hapa wapo wa siku nyingi na wanatusaidia. Kwa mfano, Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali ni mfanyabiashara wa siku nyingi na yeye ambaye ana-*import* na tayari katika ku-*import* kwake tunaofaidika ni sisi, tunakopa vespa hapa, watu wengi Unguja hii wanakopa vespa kupitia kwake, maana yake ana-*import* katika nchi, halafu kama ana-*export* yeye hatujui, pengine labda katika mfumo wa biashara na yeye ana-*export,* lakini huo ndio mfumo wa biashara. *(Makofi)*

Kimsingi nchi hii sasa inapiga hatua za maendeleo, na kwa kuwa inapiga hatua za maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na Wazanzibari kwamba sisi tutalinda Mapinduzi yetu ya Zanzibar kwa gharama yoyote, kwa sababu nchi yetu sasa inaelekea kwenye maendeleo na wala hatuko tayari kusikia mtu anarudisha lugha za ajabu ajabu sijui kesho, mwezi ujao, siku tatu, siku mbili, hizi lugha sio lugha za kujenga nchi yetu hizi ni lugha za kubomoa na lazima Wazanzibari wawe makini kwamba tunataka kujenga nchi yetu katika mifumo na awamu mbali mbali. Hiyo ndio haja ya Wazanzibari kwenda hatua kwa hatua katika Mapinduzi yao yaliyofanyika mwaka 1964 tarehe 12 Januari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lazima ifahamike wazi kwamba nchi yetu ya Zanzibar sasa hivi imekuwa ina changamoto nyingi, lakini imekuwa na uwezo mkubwa wa kuhimili mitafaruki na mambo mbali mbali ya biashara. Tunalo Shirika la *ZSTC* Dubai ni Shirika la Zanzibar, tunayo ofisi inayoratibu meli zinazosajiliwa na Zanzibar Dubai, hiyo ndio

biashara. Tunataka Baraza la Biashara sasa Zanzibar, na ndio maana tukasema tutampa nguvu sote Mhe. Rais afanikishe jambo hili, kwa maana ya kwamba Zanzibar ipige hatua ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani sasa hivi ni wakati muwafaka wa kusema kwamba mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Vile vile, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote tuunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ili kuisogeza Zanzibar kwenye maendeleo yanayotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum).

Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) amekuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho. Sasa naoma nimwite Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwa ajili ya kujibu hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kurudi tena kwa salama sasa hivi kumalizia kazi yetu ya kupitisha huu mswada.

Lakini kwanza nianze kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Wajumbe wa Kamati yetu hiyo kwa kuukubali mswada wetu, lakini pia kwa marekebisho mazuri waliyoyafanya ambayo yameongeza nguvu huu mswada wetu. Naomba nimshukuru sana Mwenyekiti na nimhakikishie tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wajumbe waliochangia katika mswada huu kwa ujumla ni wajumbe 17 wakiwemo:

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Simai Mohammed Said
3. Mhe. Hamad Shehe Mattar
4. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakili
5. Mhe. Hamza Hassan Juma
6. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
7. Mhe. Suleiman Sarahani Said
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
9. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
10 Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
11. Mhe. Mohammed Said Mohammed
12. Mhe. Rashid Makame Shamsi
13. Mhe. Omar Seif Abeid
14. Mhe. Hidaya Ali Makame
15. Mhe. Bahati Khamis Kombo amechangia kwa maandishi
16. Mhe. Amina Iddi Mabrouk na

17. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba michango yote iliyokuwa imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe ni mizuri na imeongeza kiwango kikubwa sana cha huu mswada wetu. Pia imenipa matumaini makubwa kwamba Baraza letu hili la Biashara la Zanzibar litakuwa ni chombo muhimu na madhubuti na chenye ufanisi, kwa sababu Waheshimiwa Wawakilishi wameukubali na wafanyabiashara wanaosikiliza sasa hivi wataukubali na wananchi wetu wataufurahia, kwa sababu umejaa matumaini kwa ajili ya kuendeleza na kupeleka mbele sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, michango kama nilivyosema pale mwanzo ya Waheshimiwa Wajumbe nimeipokea, kwa sababu imeongeza ubora wa mswada wa sheria hii. Vile vile, michango hii ina weledi mkubwa, michango ile imetoa rai mbali mbali za utekelezaji na imetoa mapendekezo ambayo tukiyatekeleza yataweza kufanikisha Baraza letu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi, kwamba nimepokea michango yao na maoni yao na marekebisho ambayo wameyapendekeza na marekebisho ya kamati yote nayachukua na tuko tayari kuyatekeleza. Kwa kweli, tunataka Baraza hili liwe Baraza ambalo ni zuri na ambalo litakuwa linafanya kile ambacho serikali inataka kifanye.

Mhe. Mwenyekiti, labda niseme kwamba nichukue nafasi hii kutoa pongezi za dhati kabisa na ningeomba ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi tukakubaliana na mimi kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein. Kwa kweli amelisimamia Baraza tangu linaanzishwa, akaliendeleza mpaka huu mswada tuliokuwa nao hivi leo umetokana na maelekezo na juhudi na marajio yake makubwa, kwamba Baraza hili ndio litakalokuwa suluhishi kubwa na litakalokuwa chombo kikubwa cha kuwaweka pamoja wafanyabiashara na serikali.

Hivyo, ni jambo ambalo linatakiwa na ni muhimu kwa maendeleo yetu. Naomba kabisa mkubaliane na mimi tumpe pongezi nyingi sana na tukubaliane kuwa Mhe. Dkt Ali Mohd Shein ni Rais wa kisasa anaependa maendeleo na anataka kwamba Zanzibar irudie katika wakati ule nilipokuwa nyuma kwamba Zanzibar kuwa ni Kituo cha Biashara basi Zanzibar ichukuwe nafasi hiyo tuwe na Kituo cha Kibiashara cha Kimataifa na kuweza kutoa huduma katika ukanda wetu wote na dunia nzima. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kama nilivyosema kwamba Waheshimiwa Wajumbe, ambao wengi walikuwa wanapendekeza ni marekebisho katika vifungu vyetu na nimeviunga mkono. Lakini kuna mambo ambayo madogo madogo wameulizwa na Waheshimiwa Wajumbe naomba kuyajibu kwa jumla.

Kwanza, Mhe. Ali Suleiman Ali nafikiri alizungumza kwamba Rais kama Mwenyekiti akiwa na udhuru wowote atawakilishwa vipi. Naomba nimuhakikishie Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba Rais anapokuwa hayupo kiutaratibu Rais huwa anachaguwa mtu wa kumuwakilisha kiongozi wa kumuwakilisha na hii ndivyo itakavyokuwa. Kwa hivyo, usiwe na wasi wasi hii shughuli itakwenda kama vile ilivyokuwa imepangwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine ukiangalia orodha huu wa Wajumbe hasa ile Kamati ya Kilimo ilipendekezwa kwamba Mjumbe wa Jumuiya ya Wavuvi, lakini Mhe. Mwenyekiti, nikuhakikishie hakuna mpaka sasa hivi Zanzibar Jumuiya ya Wavuvi. Lakini wavuvi watawakilishwa vile vile na jumuiya nyengine ambayo imeangalia mambo yote yanayohusu sekta hii ikiwemo ufugaji na kadhalikaa. Kwa hiyo, watawakilishwa mle na maoni yao yatafikishwa kunakotakiwa.

Vile vile Mhe. Simai Mohamed Said katika mambo aliyoyazungumza ambayo niyasema kwa ufupi baadaye aligusi kwamba katika hili Baraza tuwe na Mjumbe wa *Diaspora*. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo zuri lakini kwa sasa hivi mfumo huu wa kuwatia watu wa *Diaspora* naona kwamba hautoweza kuleta tija. Lakini mapendekezo yetu kwamba kutakuwa na nafasi ya kualikwa Wajumbe kama hawa. Kwa hiyo, Mjumbe wa *Diaspora* ataalikwa katika mkutano ule wa jukwaa na ataweza kuchangia kama wanavyokuwa wanachangia wengine.

Pia, alizungumzia kwamba Wajumbe ambao wanatambulikana kutoka Bara nao wawe na nafasi katika Baraza. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kumuhakikishia Mhe. Simai Mohamed Said kwa kusema kwamba Wajumbe hawa nao wataalikwa katika jukwaa, kwa sababu jukwaa ni pana zaidi na watakuwa na uwezo wa kuzungumza kwa ubana zaidi na kutoa mapendekezo yao na yakaweza kufanyiwa kazi.

Pendekezo jengine Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa kuhusu mtendaji wa Baraza au Mjumbe wa vyombo vilioko Bara kama vile vya *East Afrika* na nakadhalika. Hili jambo linakubalika na tutafanya hivyo, ili kumuwezesha na yeye awe amejiunga anajua yanatokea upande ule mwengine, kwa sababu biashara Mhe. Mwenyekiti haina bahari, biashara haina mipaka. Biashara ni pande zote sisi na Tanzania Bara, sisi na Afrika Mashariki sisi na kanda nyengine ikiwemo *SADC* na ile *tripartite*. Kwa hiyo, sehemu zote hizi tutahakikisha kwamba Katibu Mtendaji wetu na yeye pia ataweza kujumuika na kuweza kuchangia na kuweza kupata taarifa, ili imuwezeshe kufanya kazi vizuri zaidi. Jengine ambalo lilikuwa limependezwa ni kuhusu hili Baraza liweze kutatua kero, na hiyo ndio moja ya madhumuni ya Baraza hili kwamba ni eneo ambalo wanakaa wafanyabishara wa sekta binafsi pamoja na serikali. Kwa hivyo, kero zote ambazo zinakuwa kama vikwazo kwa biashara zao ama zinakosesha nafasi kwa zile biashara zao kwenda mbele au pengine kero ambazo ziko nje ya uwezo wa serikali au uwezo wao.

Lakini kwa pamoja tunaweza kukaa na tukafikia njia tukaweza kuondasha kero hizo. Kwa hiyo, ni moja ya madhumuni ya hili Baraza, ni imani yangu kwamba Baraza hili litaweza kufanya hivyo, na kuweza kutatua kero zote au muhimu ama nyingi ambazo zinawasumbua wafanyabiashara na wenye viwanda na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Simai Mohamed Said alizungumzia suala la haya mambo yaliyotokea hivi karibuni, kwamba kuna wananchi wenye nyumba wanatoa vyumba kuwapa wageni na hili jambo limetokea hivi karibuni huko Tanzania nadhani na Zanzibar, lakini ni jambo ambalo linafanywa nchi zote ukiwa Marekani unaweza kukaa kuna nyumba za watu tunaita *pay guest* unakaa unalipa Afrika ya Kusini wanafanya hivyo hivyo, Nairobi wanafanya hivyo hivyo, yaani nchi zote zilizoendelea wanafanya hivyo.

Nakubaliana na Mhe. Simai Mohamed Said kwamba labda tuangalie wizara zinazohusika waangalie utaratibu wa kuifanya iwe rasmi, na watu vile vile waweze kujulikana na kulipwa kile ambacho kinatakiwa kilipwe kama mapato serikalini. Kwa kweli, hiyo kazi inafanyika sasa hivi Bara wanafanya sasa hivi, lakini sisi Zanzibar tusiwachie waende hivi hivi kiholela tuwe na utaratibu mzuri wa kuwasimia.

Katika jambo mambalo lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi Mhe. Mwenyekiti, kwamba Baraza hili litumie wataalamu hasa wa Vyuo Vikuu, ambao ndio walobobea katika hizi fani wana uzoefu wa kutosha na wanaelewa nini hasa biashara inavyokwenda, na wataweza kutoa mapendekezo ambayo yataweza kuongeza uwezo na kuongeza ufanisi wa wafanyabiashara wetu. Suala hili nakubaliana nalo na naliunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil alizungumzia kwa ujumla tu, mambo ambayo nadhani ni muhimu niyazungumze kwa sababu yatatoa ufafanuzi mara nyingi Waheshimiwa Wawakilishi huwa wanazungumza masuala haya. Alizungumzia suala zima la kuwa na usawa katika biashara baina ya wafanyabiashara ya nje na wafanyabiashara wa ndani, yaani wale wawekezaji wa nje na wakekezaji wa ndani. Lakini pia alizungumzia usawa kwamba katika kufanya biashara paweko mahala ambapo pataweza kama kitengo cha usuluhishi.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua katika biashara kunakuwa kutokuelewana, kuibia au labda kudhulumiana. Sasa baada ya kwenda Mahakamani chombo hichi alivyopendekeza yeye kama Baraza liweze kutoa suluhishi katika kesi kama hizo.

Mhe. Mwenyekiti, ni wazo zuri unapozungumzia kuwa na usawa hata katika Sheria ya Biashara hata katika Sheria ya Kufanya Biashara Halali ya mwaka 1995 tumezungumzia kwamba biashara ziwe za usawa na ziwe halali. Kwa hali hiyo, kulikuwa na vyombo vinatakiwa viongozwe hapa Zanzibar, lakini bado vyombo hivyo havijaongezwa.

Lakini naomba nimuhakikishie Mhe. Mjumbe, kwamba Sheria hii ya *Fair Competition*, sheria inayotaka wafanyabiashara waweze kushindana kwa uhalali wasitumie njia kwa sababu wao wana *monopoly* au hao ni wafanyabiashara wakubwa wakaweka bei tu bila kuangalia maslahi ya wananchi pamoja na taifa wakapanga tu bei. Hivyo ni vyema, lazima vitu vyote hivi vitizamwe na kuwepo na chombo ambacho tunakaa kama na kiongozi na kuwaambia kwamba hapa hujafanya haki urudi katika msingi wa haki na hatua kuchukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nihakikishie kwamba sasa hivi wizara yetu tumo katika mkakati, kwa sababu serikali imeshatupa rasmi idara hii ya kuangalia ushindani wa biashara na vile vile kumlinda mlaji tunaelekea huko, kwamba huko mbele biashara ya Zanzibar lazima ifuate utaratibu uliokuwa wa wazi na wa haki. Kwa hiyo, jambo niliona nilisemee kwa sababu hata mara nyengine wanauliza masuala ya Tume ya Bei.

Masuala ya Tume ya Bei, kwamba watu wanapandisha bei wanavyotaka wenyewe. Hichi chombo ambacho kinatakiwa na *tribunal* na *bureau* na Mahakama yake ya kuweza kutoa maamuzi nitasimamia. Hicho chombo kitatupa nguvu zaidi Baraza la Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa sekta binafsi na kwamba hatujafanya *review* za sekta binafsi, lazima niseme kwamba sheria za *PPP* tumeshaipitisha Wizara ya Fedha kupitia Tume ya Mipango wanasimamia sheria hii. Lakini bado kuna sheria mbili kuna Sera ya Sekta Binafsi, ambayo sasa hivi imo katika mchakato wa kufanya lakini pia na Sheria ya Sekta Binafsi pia imo katika mchakato kumalizwa. Haya mambo yote yakimalizika yanatoa nguvu zaidi hili Baraza la Biashara, ili liwe na meno zaidi liwe na uwezo wa kutoa maamuzi ambayo yatatekelezeka kwa urahisi na yatakuwa ya kudumu na yatakuwa mazuri kwa uhai na maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nije katika mchango wa Mhe. Mohammed Said Mohammed katika michango yake alizungumza mambo mengi. Lakini nizungumze hili ambalo lilizungumzwa linalohusu uteuzi wa Katibu mtendaji. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais amemteuwa Katibu Mtendaji hakufanya makosa na wala hakubahatisha, kwa sababu kama mnavyojua nilisema pale mwanzo kwamba Baraza la Biashara lilipaonzishwa lilianzishwa kwa utaratibu wa Hati ya Kisheria, na hii ni miongoni mwa *instrument* zinazotumiwa katika sheria.

Kwa hivyo, ni miaka yote ile Baraza la Biashara lilikuwa linafanyaka kazi kwa mujibu wa Hati za Kisheria na lilikuwa liko sawa sawa, na mtendaji huyu kateuliwa kwa sababu bado sheria ile inafanya kazi ameteuliwa kwa mujibu na kwa uwezo aliokuwa nao Mhe. Rais. Hivyo, hakuna kosa lolote lililofanyika na kwa kweli huo ndio utaratibu ambao tunaofata wa utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba nijibu hoja ambazo zililzozungumzwa kwa upande wa kwamba biashara ya Zanzibar tuko nyuma. Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani kwamba biashara ya Zanzibar tuko nyuma tulikuwa juu sana tukateremka kwa kiasi tukawa chini sana. Lakini sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tunakwenda vizuri. Kwa nini nikasema hivyo, kwa sababu katika taarifa ya *World Bank* iliyozungumza *Doing Business* sisi tulikuwa chini kabisa, lakini tumejipangia kwamba katika miaka mitatu tuliyonayo mpaka 2020, basi kiwango cha kufanya biashara na kufanya mambo yote yanayohusu biashara na viwanda, basi viwango viwe vya juu zaidi.

Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti suala lilichukuliwa mfano mmoja wa leseni. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mwenyekiti upatikanaji wa leseni ni kikwazo kimoja cha biashara kinachofanya biashara za Zanzibar zionekane kwamba ziko chini, kwa sababu mtu kapata leseni inabidi atembee vyombo vya kiserikali vilivyokuwa vingi sana, mfano mmoja anataka kufungua mtu *restaurant* au hoteli ama *guest house*.

Lakini inabidi apate vibali katika vyombo mbali mbali ikiwemo kwa Sheha ikiwemo Halmashauri, ikiwemo Kamisheni ya Utalii ikiwemo *ZRB* ikiwemo *TRA* na kwengine na mifano hii ni mingi Mhe. Mwenyekiti, mingi sana. Lakini, tumejiandaa kwa kweli sasa hivi tunataka kwenda katika utaratibu wa kutoa leseni katika utaratibu wa *electronic*, yaani unapata risiti zako kupitia mtandano. Vile vile, tunataka tuwe na *one stop centre*,

yaani eneo moja ambalo mtu baada ya kuzungushwa mote humo atembee basi wende eneo moja.

Sasa hivi Baraza letu limeshaanza kutoa muelekeo, kuweka vigezo pamoja na kufanya utaratibu wa leseni ziwe rahisi kupatikana na zisiwe usumbufu na wala zisiwe ghali sana kwamba watu wanakuwa hawawezi kuzipata. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama wasimamiaji wa sekta hii ya biashara tumejiandaa vizuri. Niseme kwamba unapokuwa na suala la biashara kuna vyombo vinatakiwa viwepo kulikamilisha Baraza hili la Biashara na pia tukikalisha Kitengo kile chetu cha Kumlida Mlaji au Mtumiaji tutakuwa tumo katika kukamilisha vyombo vyote vinavyosimamia biashara hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa upande wa Mhe. Bahati Khamis Kombo amenileta kwa maandishi. Mhe. Mjumbe, kasema yeye ananiunga mkono asilimia 99 lakini asilimia moja alikuwa anataka kujua haya mapato ya *TBS* katika mambo ya *PVAC* linatoa faida gani kwa taifa. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba mapato haya mpaka sasa hivi tumeshakusanya zaidi ya bilioni mbili na fedha hizi zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, kwa hakika kabisa fedha hizi ndizo zinazochangia kuongezea pale ambapo tunatakiwa tuongeze.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mapendekezo yote ya kurekebisha vifungu nimeyakubali kuna pendekezo moja ambalo liliguswa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mohamed Said Mohamed pamoja na wengine wengi ambao wamezungumza, nalo hili kuhusu kipengele tulichosema kwamba katika wale Wajumbe wa Baraza kwamba amependekezwa mfanyabiashara maarufu kutoka Kampuni ya Bakhresa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme kwamba hili jambo lilikuwa limeshatolewa maamuzi na lilikuwa limeshakubaliwa kwamba hichi kifungu kiwekwe sawa kirekebishwe kisomeke kama hivi ifuatavyo:-

> "Mfanyabiashara maarufu atakaechaguliwa na Jukwaa la Wafanyabiashara". *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme hivi kwa sababu tulipokuwa tunazungumza wananchi wanasikia na sipendi wananchi wasikiwe kwamba vile Nd. Bakhresa tumempa sisi fedha, yaani tumemfanyia upendeleo. Hii pendekezo halikutoka serikalini, isipokuwa lilitoka katika kikao cha Jukwaa la Biashara lililopita, na ndio maana mkaliona katika mapendekezo yaliyokuja katika mswada huu tulioleta, walikaa wafanyabiashara wenyewe huko nyuma na wakasema nani ambaye atatuwakilisha katika Baraza sisi wafanyabiashara wa Zanzibar, ambaye ana uwezo mkubwa anaaminika, amejitolea Mzanzibari kindakindaki na mfanyabiashara anayejulikana nje na ndani. *(Makofi)*

Kwa kweli, tunao wafanyabiashara hapa wazuri kabisa, lakini tuseme ukweli. Wafanyabiashara weneyewe wamemchagua Nd. Bakhresa. Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nitoe mfano mmoja kwa mradi wake mmoja tu sisi tunaoshangalia vitega uchumi tunachukuwa miradi ya Bakhresa kama ndio *right point* ya hadidu rejea. Sasa kama

anakuja mfanyabiashara mkubwa anamuangalia anauliza nani mkubwa yupo, mradi gani ambao ni mzuri tunaweza kufanya anapelekwa kuangalia miradi ya Bakhresa akiangalia *satellite* na sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niseme Waheshimiwa Wawakilishi hili jambo si la Zanzibar peke yake, isipokuwa nchi zinazoendelea zote zinawatambua na kuwaheshimu na kuwapa nafasi wafanyabiashara ambao ni wa mfano, kama mnavyosikia Mr. Tata wa India anakaa kunako mabaraza tunajua sote sisi gari za Tata yule muwekezaji wa Tata anakaa kwenye mabaraza. Ukiangalia *Nissan* akina *Honda*, akina *Hyunda*i, akina Huwawei, Marekani kina Lock Fela wanakaa kwenye mabaraza.

Kwa hiyo, mimi hataka nitoe elimu hii kwamba si kosa Nd. Bakhresa kuwa kwenye kamati hii Mzanzibari kindakindaki mchango wake ni mkubwa na wa mfano tena ni wa mfano sasa tunatakiwa sisi wote tukubalia na tumseme kwa vizuri tusimseme kwa vibaya tukamrudisha nyuma. Mhe. Mwenyekiti, niliona niseme hayo kwa sababu sitaki tena baadaye wakalichukuwa hili huko nje ikawa akaonekana Bakhresa kama muhalifu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambao nilikuwa nataka niliseme la mwisho kulikuwa kuna pendekezo kwamba kuna neno limetumika Bodi lile neno ni la makosa Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa iwe Kamati Tendaji sio bodi. Kwa hiyo, nadhani hapo napo inabidi tufanye marekebisho.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme yale ambayo yalikuwa yanamsumbua Mhe. Jaku Hashim Ayoub asije akanipigia mabuti. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe katika vipengele alivyoviseme yeye zaidi hivi vya uteuzi. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa wote ambao walizungumzia suala hili. Lazima tuone huu mswada ulivyokwenda upande mmoja kuna serikali, yaani dola na kwa upande wa pili sekta binafsi, sekta binafsi wanakutana pamoja. Lakini sekta binafsi lazima waje viongozi wao hawezi mtu mmoja mmoja akasema yeye aje kwenye mabaraza na viongozi hawa wanachaguliwa na wajumbe wao, na wajumbe wao lazima wawe wajumbe wa jumuiya na hapa naomba nijibu vile vile hoja kwamba wanawake wawemo katika hili Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niambiwe kuna mwanamke gani hapa Zanzibar Mwenyekiti katika jumuiya hii, *Chamber* of *Commerce* Mwenyekiti wake Tafik Turky na vyombo vyote hivi vya biashara, bado wanawake tuko nyuma hatuajweza kuingia katika kuongoza vyombo hivi. Lakini hilo kwa upande wa wanawake si tatizo, kwa sababu Mhe. Rais amepewa nafasi humu humu katika mswada kuteuwa Wajumbe waingie katika vyombo hivi. Kwa hiyo, Mhe. Rais kwa kifungu hichi anao uwezo wa kuteuwa mwanamke akawemo katika vyombo hivi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu hasa akinamama wa UWAWAZA wenzangu tuwe na subra, kwa sababu Mhe. Rais hajatuangusha ni kiongozi wa mfano katika sehemu nyingi ametuteuwa, na nina imani kubwa atatuteuwa katika vyombo hivi na sisi kuwemo katika uwamuzi na kuwemo katika kutoa mapendekezo ambayo yatakuwa ya muafaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, vile vile suala la kwamba wafanyabiashara hawa, kuna Jumuiya nyengine. Jumuiya iliyokua kubwa ni *Zanzibar Chamber of Commerce Industry and Agriculture*, yaani chombo cha wafanyabiashara wenye viwanda na kilimo. Lakini kuna Jumuiya nyengine ambazo sio wanachama wa Jumuiya hii, sasa tunasema wale ambao sio wanachama wa Jumuiya hii na wao pia wapate nao kushiriki katika suala zima la biashara kwenye Baraza la Biashara na pia kwenye Jukwaa.

Kwa hivyo, ndio maana tukapendekeza humu *Chief Secretary*, yaani Katibu Kiongozi kwanza yeye ndiye Mwenyekiti wa Kamati Tendaji, lakini awe na Mwenyekiti Mwenza lazima atoke katika sekta binafsi, lakini sekta binafsi wachaguliwe ndani ya jopo lao lile achaguliwe mtu mmoja awe ndiye mwenza na huo ndio utaratibu, sio jambo ambalo limekosewa. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe asiwe na wasi wasi, kwa sababu hawa wote wanachaguliwa na vyombo ambavyo viko rasmi na ni vyombo vinavyokubalika.

Mhe. Mwenyekiti, labda niseme kwamba yale yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe waliyauliza nimeyaunga mkono kama nilivyosema pale mwanzo. Ningesema kwamba tulipata nafasi hapa leo kuzungumzia mambo mengi yanayohusu viwanda na yanayohusu biashara. Kwa hivyo, niseme tu kwamba kuna miswada mingi inakuja mbele yetu, wizara yetu tumejiandaa vizuri.

Vile vile, liliulizwa swali kwamba huyu Katibu Mtendaji atapokea maagizo ya nani, anaweza kubabaika. Mhe. Mwenyekiti, huyu Katibu Mtendaji bado ni mtendaji wa serikali, yuko ndani ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, lakini bado chombo hiki kiko chini ya Ofisi ya Rais. Lakini kuna mambo ya *administration* na kuna miongozo mbali mbali, kuna masuala ya fedha na masuala ya bajeti. Lazima kuwe na chombo cha kuweza kumsaidia aweze kutekeleza yale mambo ambayo yanatakiwa atekeleze, ndio maana akawa chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Lakini kazi alizonazo anafanyakazi kutokana na vikao maalum, Kikao cha Kamati Tendaji na Kikao cha Mabaraza. Hivyo ndio vikao maalum anatakiwa avifanyie kazi.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuna swali liliulizwa je, sasa hawa watakaokaa katika hii Kamati Tendaji watafanyakazi vipi na maamuzi yao yatakuwa vipi, halafu akataka waongezwe, kwamba serikali ni wengi kwenye kamati hizi lakini wafanyabiashara ni kidogo. Nafikiri ni kamati moja tu ambayo imeonekana kwamba uwiano unakuwa mzuri kidogo. Lazima tukumbuke waheshimiwa kuhusu huu utaratibu mzima unavyokwenda.

Baraza linakaa na linapokea zile kero zote na mambo yote ambayo yanatakiwa yaamuliwe, Baraza linakaa na kuzungumza pande zote mbili zinazungumza. Baada ya pale kamati zinatakiwa zizungumzie sasa urekebishaji au suluhu au kutaka kupata maelekezo au kutoa ufumbuzi wa yale mambo ambayo yameonekana yana matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, sio burasa kuongeza wafanyabiashara binafsi, kwa nini, kwa sababu anayetoa ufumbuzi anayetoa maamuzi na utekelezaji ni serikali, kwa hivyo serikali ni lazima wawe wengi katika kikao kile, ili wanapozungumza ule utekelezaji uwe mzuri na wa haraka. Lakini ukiwaweka watu binafsi, watu wa sekta binafsi wameshazungumza vikao vya juu, pale kazi yao ni mapendekezo ya utekelezaji ambayo yanatoka pale

yanakwenda katika utaratibu ambao wamejiwekea, kwamba yaende serikalini kwa utekelezaji. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme la mwisho kwamba jamani tumetoka mbali, wakati huu tuliokuwa nao, huu mswada umekuja kwa wakati mzuri, kwa nini nasema hivyo. Kwa kweli, tukumbuke na tusikilizeni matamshi ya wenzetu nchi zilizoendelea. Sasa hivi nchi zote duniani zinazungumzia masuala kwamba kila mtu anajiangalia yeye mwenyewe. Hata suala la biashara hawazungumzii tena biashara ya dunia, au biashara kwamba mmoja apate na mwengine apate, wanazungumzia biashara kwamba mmoja tu apate na aendelee kumkandamiza mwengine.

Kwa hivyo, sasa hivi hili Baraza kwa muundo huu umekuja kwa wakati mzuri kabisa, wakati Tanzania tunajiendeleza kiviwanda na kibiashara. Lakini pia tukumbuke kuna mabadiliko makubwa, mabadiliko katika Jumuiya ya Afrika imetia mkazo katika kuwa na biashara ndani ya Bara letu la Afrika, ambalo lina mali ghafi nyingi, lina uwezo mkubwa na lina soko kubwa. Sasa hivi Afrika tunawakaribia Wachina, Wachina sasa hivi wameshapindukia bilioni mbili, Waafrika tunakaribia bilioni moja na zaidi, labda bilioni tatu au nne huko, hilo ni soko kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, lazima nimuunge mkono Mhe. Said Soud Said (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum), kwamba Zanzibar tujipange tukaze soksi, tufanye yale mambo muhimu, kwa ajili ya maendeleo yetu na Baraza la Biashara ndio ambalo litatusukuma. Kwa hiyo, wakati mwengine tunaambiwa serikali tuna *bureaucracy*, serikali inaonekana inakuwa na *bureaucracy*. Lakini ndani ya Baraza itatupa nafasi sisi na wenzetu wafanyabiashara kuambizana kwamba hapa, hii tuliyokuwanayo ni ndogo tuongeze zaidi, tufanye nini, tutoke twende wapi na tutafute nani awe rafiki yetu, tutafute mali ghafi ya aina gani, soko la aina gani na kwa utaratibu gani.

Mhe. Mwenyekiti, hili Baraza Waheshimiwa Wajumbe, ndicho chombo cha maendeleo na ndio kitakachotupeleka kule tunakotaka kwenda. Niseme tu kwamba wakati ni muafaka na niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi muwe pamoja na sisi kutuongoza katika hili Baraza kwa ushauri uliokuwa mzuri na makini, na kuweza kwenda mbele kule ambako tunataka twende.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaoafiki hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mkono. Wasiokubali hoja ya Mhe. Waziri. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwe na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kabla hatujaendelea kuna tangazo. Baada ya kuahirisha kikao hiki Waheshimiwa Wajumbe wabaki ukumbini kuna mambo muhimu tunataka kujulishwa. Mhe. Waziri karibu utoe taarifa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara ya 2017

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu cha 1 Jina fupi na Kuanza Kutumika pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 2 Matumizi

Kifungu cha 3 Ufafanuzi pamoja na Marekebisho yake

Kifungu cha 4 Malengo ya Baraza pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar

Kifungu cha 5 Uanzishwaji wa Baraza pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 6 Muhuri wa Baraza pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 7 Muundo wa Baraza

Mhe. Simai Mohamme Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilitoa ushauri kwamba katika wajumbe hawa watakaotoka katika sekta binafsi waweze kufahamu dira ya chama ambayo pia ni *manufacture* ya Chama cha Mapinduzi, nikashauri wafanyiwe semina. Sasa Mhe. Waziri wakati anatoa maelezo yake sikumsikia, ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa najibu hoja nilisema kwamba mashauri yote nayakubali yakiwa mazuri ambayo yanataka mafanikio. Hili pia nimelikubali. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohamme Said: Ahsante, Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu cha 7 Muundo wa Baraza pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 8	Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 9	Kazi za Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 10	Mikutano na Jukwaa la Majadiliano la Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 11	Uteuzi wa Katibu Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 12	Majukumu ya Katibu Mtendaji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na mapendekezo au maoni yangu ambayo nilipokuwa nikichangia kifungu 12(2) nilisema, naomba nikinukuu Mhe. Mwenyekiti, ili Mhe. Waziri anifahamu.

"Katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1), Katibu Mtendaji atakua chini ya usimamizi na miongozo na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko"

Hapa nilisema kuna Baraza na kuna kamati, mtu mmoja huyu atachukua maelekezo mangapi, huku ni kuja kusokotwa. Niliomba neno miongozo liondoke.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nilijibu swali hili, lakini pengine Mhe. Mjumbe alikuwa hayupo, lakini nitarejea tena kwa sababu ya umuhimu. Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba chombo hiki kwanza chombo cha serikali hakiwezi kikawa kinaning'inia bila ya kuwepo mahali na hiki chombo ni cha biashara kimewekwa kwa *administration* chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Vile vile, majukumu yake kwa sababu ni chombo cha kusimamia kitu maalum, majukumu yake yamepangwa kwa mujibu wa sheria, nayo ni kuandaa vikao na utaratibu wote kamati kutuwakilisha pengine nje ya nchi, kwa sababu kuna vikao kama hivi nchi za nje pia ni moja kama ilivyoelekezwa humu. Lakini sasa kuna masuala ya *Administration* Mhe. Mwenyekiti, kuna masuala ya bajeti, kuna masuala mengine ya utendaji kazi na kadhalika.

Kwa kweli kama nilivyosema kwa sababu chombo cha biashara ndio manufaa kwa chini ya Wizara ya Biashara na Viwanda. Kwa hivyo, miongozo atapokea kote, kwa ile miongozo inayohusu mambo ya mabaraza na utaratibu mzima wa mabaraza kama ilivyoelezwa hapa, pale anatakiwa ashughulikie na *Chief Secretary* ambaye ndio Mwenyekiti wa Kamati Tendaji na Mwenyekiti wake Rais.

Mhe. Mwenyekiti, lakini humu humu ukiangalia katika hii sheria imetupa mamlaka kama mimi waziri nasimamia sheria ya biashara. Pia kutoa muongozo ili chombo hiki kisiwe kina ning'inia lakini kiweze kwenda vizuri kama kinavyotakiwa kiende vizuri kwa ufanisi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kimejirudia karibu mara tatu au mara nne, naomba aangalie Mhe. Waziri. Ukitizama kifungu cha 12(1) kimetaja majukumu ya Katibu Mtendaji, na kile kifungu cha 12(2) kimekuja tena kueleza kuwa majukumu ya Katibu Mtendaji yatatekelezwa chini ya usimamizi wa miongozo ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, kama hapo hapatoshi kifungu cha 12(3) kimerejea utekelezaji wa majukumu, huko ni kusokotwa, mtu mmoja huyo atachukua maelekezo mangapi. Tunatakiwa watunga sheria tuwe makini, tusijekumpa mtu majukumu baadae utekelezaji ukawa haupo. Mtu mmoja atafanya mambo mangapi, atachukua maelekezo kwa huyu, akija kwa huyu utakuwa ni mseto, huo ni mchanganyiko Mhe. Mwenyekiti. Nia yetu ni nzuri ya kutengeneza, lakini huo ni mkorogo, hawezi kuchukua mtu maelekezo kwa watu watatu.

Mhe. Mwenyekiti, kimejirejea aangalie Mhe. Waziri. Kifungu cha 12(1), 12(2) na 12(3) maana ndio ile ile. Kwa ufupi, kama ni wali unaweza ukabadilisha mapishi ukapika mseto, ukapika pilau na ukapika biriani, lakini ndio ule ule wali.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Jaku atizame hicho kifungu anachokisema yeye cha 12(1), orodha hii ya kazi ambazo mimi ningemsaidia kufanya.

1. Kwanza kutekeleza kazi za kila siku za Baraza,
2. Kuweka kumbukumbu za vikao vya Baraza pamoja na kamati zake,
3. Kutayarisha hoja zinazotakiwa kujadili katika vikao vya Baraza,
4. Utekelezaji wa maazimio ya Baraza,
5. Kuungana na mabaraza ya mikoa,
6. Kutayarisha bajeti kwa kila mwaka ya kazi za Baraza na kuiwasilisha kwa Kamati Tendaji kwa ajili ya kuthibitishwa na kuidhinishwa, sasa kwanza nitowe mfano huo.

Mhe. Mwenyekiti, taratibu za kibajeti lazima zipitie katika wizara ili ndio ziweze kuleta bajeti yake. Kwa hivyo, hapa anaunganishwa na wizara. Pili kuandaa mpango mkakati wa kibiashara wa Baraza. Mwisho kutayarisha ripoti ya utekelezaji na kadhalika.

Lakini huku Mhe. Mwenyekiti, ameambiwa kwamba usimamizi na miongozo ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, na kama nilivyosema Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko miongozo inahusu masuala ya bajeti, masuala ya *Administration* na masuala wakati mwengine ya kusaidia katika baadhi mambo ya mafunzo na kadhalika, ambayo humu hayakutajwa.

Kwa hivyo, sio jambo la kigeni ama linatatiza, ni jambo ambalo husaidia hiki chombo kifanye kazi vizuri na kuna vyombo vyengine, sio tu Zanzibar kuna nchi nyengine, hata Bara viko vyombo kama hivi ambavyo vinasimamiwa, ingawa vinakuwa juu katika *level* ya juu, lakini vinasimamiwa na wizara husika. Wizara husika ya chombo hiki ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, naona bora tuendelee tusije tukafika pahali mbali.

Kifungu cha 12 Majukumu ya Katibu Mtendaji pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 13 Wafanyakazi wa Baraza pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Uanzishwaji na Muundo wa Kamati ya Baraza

Kifungu cha 14 Uanzishwaji wa Kamati Tendaji

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia muundo na uanzishwaji wa Baraza. Nilizungumza vizuri kwamba uwiano hapa uko vizuri sana, lakini katika uundaji wa zile Kamati za Baraza. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia maana halisi kwamba biashara yoyote iko katika sekta binafsi, serikalini hakuna biashara.

Kwa hivyo, ndio nikasema angalau basi na huku ule uwiano uwepo, ili hata katika vikao vyao ikifika *time* ya kuamua kwa kura na wao watu wa sekta binafsi wawe na nguvu za kuzungumza. Lakini kwa muundo huu ulivyo, inamaana siku zote wataburuzwa watu wa sekta binafsi. Ndio nikapendekeza hapa angalau baadhi ya wajumbe waongezeke katika jadweli kwenye muundo wa kamati.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeomba katika hizi angalau badala ya kumi kwa tatu, angalau basi iwe kumi kwa saba angalau inapotokea maamuzi ya kupiga kura uwepo ule uwiano, sikupata jibu lake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani, muundo umo katika kifungu namba 15 bado hatujafika, kifungu cha muundo hatujakifikia bado, tuko katika kifungu namba 14 Uanzishwaji wa Kamati Tendaji.

Kifungu cha 14 Uanzishwaji wa Kamati Tendaji

Kifungu cha 15 Muundo wa Kamati Tendaji

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri maelezo nimeshayatoa, naomba jibu langu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nahisi bado hatujafika katika kifungu hicho, kwa sababu yeye kwa nilivyomfahamu anazungumzia kamati zile ndogo ndogo, labda iwe mimi sijafahamu anifafanulie vizuri. Kwa sababu hapa tunazungumzia *Executive Committee* ambayo ni Kamati Tendaji inayoongozwa na *Chief Secretary*. Kamati anazozungumza yeye ambazo tuwe na uwiano ni zile ambazo kamati za *sector* ambazo zinaongozwa na Mawaziri, sasa ningeliomba nifafanue zaidi nadhani mimi hapa sina zaidi. Ahsante

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani hebu lete ufafanuzi.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa tuendelee ninasubiri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wakati nilipochangia kifungu hichi 15(b) inasema Mwenyekiti Mwenza atatoka sekta binafsi kifungu cha jaduweli ya pili akasema, Makamo Mwenyekiti na Mwenyekiti hayupo ataendesha vikao na kama hayupo atatoka jumuiya ya wafanyakazi wenye viwanda na wakulima. Je, Makamo atatoka sekta binafsi ambayo haijatafsiriwa na kutoka *Chamber*.

Jambo jengine, nilichangia hapo hapo kutoka 15(4) ambacho kinatoa uwezo wa kubadilisha wajumbe kutoka sekta binafsi kama kamati inavyoeleza. Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kwa nini kamati tendaji haina muda wa kumaliza wajumbe kutoka sekta binafsi kuwekwa muda vizuri, nilikuwa nataka muda wa hao wajumbe wawekewe muda.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu la kwanza la Mhe. Jaku Hashim Ayoub vile vile nimeshalijibu hili lakini ndio alikuwa hayupo. Kwa hivyo, nilisema kwamba katika hili la (b) Mwenyekiti ni *Chief Secretary* ni Katibu Kiongozi kule kunakuwa na mwenza ambae anatoka sekta binafsi, lakini hatukupendekeza kwamba *Chief Secretary* achague katika sekta binafsi ni wenyewe waliopo katika sekta binafsi watachagua nani mwenyekiti wao.

Kwa kweli, humu hatukuwafunga kwamba hatujui kama watakuwa pengine atakuwa kiongozi wa *Chamber* ya biashara au atakuwepo na akina *ZAT* na wengine wengine. Kwa hiyo, wao wenyewe waliomo mle watakaa wenyewe watasema nani mwenza na hiyo ndio *practice* inayofanywa katika vyombo vyote vya biashara, wanajichagua wenyewe wanasema sisi kwa kipindi hichi sisi Mwenyekiti wetu Mwenza huyu. Sasa kama Mwenyekiti Mwenza hayupo wenyewe watatafuta njia ya kutafuta kwa siku ile yule mwengine kama *Chief Secretary* hayupo, wataendelea na kikao huo ndio utaratibu ambao unafanywa katika vyombo vya kibiashara kama hivi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, aliuliza kuhusu muda kwa wajumbe wa sekta binafsi, tunaelewa sisi wote sekta binafsi katika vyombo vyao hivi wana muda hawakai wale siku zote kila baada ya miaka mitatu wenyewe wana mikutano yao wana chaguzi zao. Kwa hivyo, nafikiri si sahihi kuwawekea muda kwa sababu ule muda wao ukishakwisha watabadilika waingie wengine. Hivyo, hatukutaka kuingia zaidi katika kuchagua na kuwabana wajumbe, kwa sababu wao wenyewe wana taratibu zao za kuchaguana na sisi tunachagua yule ambae ni kiongozi ndio anayekuwa katika vikao kama hivi. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, itakuwa kitu cha ajabu kweli kweli kuwa kitu hakina muda na itakuwa vichekesho hata kwa wananchi watatuona watu wa ajabu kweli kweli sisi ndani ya Baraza, muda lazima uwepo hata ukenda kununua chakula utaambiwa kuna muda wake wa ku-e*xpire* hichi kitakuwa kichekesho. Mhe. Mwenyekiti, hili sikubaliani nalo muda lazima uwepo uwe wazi kwa nini tufiche na tupo hapa kwa niaba ya wananchi anitajie muda, ili tuendelee, haiwezekani hicho kitu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimrudishe tena Mhe. Jaku Hashim Ayoub mimi nategemea yeye mjumbe wa *Chamber of Commence*, chaguzi ngapi wameshafanya kubadilisha viongozi Kiongozi wa *Chamber* aliyekuwepo sasa hivi Mwenyekiti sio yule aliyekuweko Abdalla Abassi sasa hivi yuko Toufiq S. Turky na ana miaka yake waliyomchagua wenyewe mitatu sijui minne sijui mingapi sisi hata hatuna habari na hiyo miaka yao.

Kwa hivyo, yeye kwa sababu kachaguliwa kuje pale kama Mjumbe wa *Chamber* hakuja kama Toufiq S. Turky au hakuja kama mtu mwengine ambaye ni kiongozi, isipokuwa anakuja pale kuwakilisha *Chamber* kama *Chamber* yenyewe ikimtoa akiwa si kiongozi hawezi kuingia huku, kwa hivyo tunamuwekea muda wa nini na wakati sisi sio tunaowachagua. *(Makofi)*

Ningemuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama yeye hajui pengine si mwanachama wa *Chamber*, lakini kama ni mwanachama wa *Chamber* au *Chamber* zozote zilizokuwepo hapo ukenda huko *ZATO*, ukenda *ZAT* ukenda wapi wote wale viongozi wana muda, hakuna jumuiya ambayo haipigi chaguzi wakachaguana kwa muda wao wanaojiwekea.

Kwa hivyo nadhani niseme hivyo si sawa kusema tuwawekee sisi pengine baada ya miaka mitatu ile sisi tumeshampa miaka mitatu lakini isije tena kiongozi wa *Chamber* tutafanyaje sasa, sio kila kiongozi wa *Chamber* sisi tunataka viongozi wa *Chamber*. Hivyo, tuiache kama hivi ilivyo na mimi nasema tuiache hivi hivi kwa sababu ina maslahi kwetu na ina maslahi kwa wenyewe wafanya biashara kwenye Jumuiya zao. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla sijakuruhusu Mhe. Jaku Hashim Ayoub watendaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko naomba waingie ndani kumsaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, *limit time* lazima iwepo mimi nimuombe yote nimemkubalia, *limit time* lazima iwepo ni jambo dogo tu hili.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa, Waheshimiwa Wajumbe, itabidi tupige kura wale ambao kuwa wanakubaliana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wanyanyue mikono, wanaokubaliana na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Biashara, Vwanda na Masoko wameshinda, hivyo hoja hii imekubalika. Tunaendelea.

Kifungu cha 15	Muundo wa Kamati Tendaji pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 16	Kazi za Kamati Tendaji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, 16(g) Kuthibitisha bajeti ya mwaka ya mpango kazi masuala ya ajira na kuwasilisha Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa taarifa kuwasilisha katika Baraza, ninachoomba mimi hoja ya maneno ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iondoke na ipendekezwe Wizara anayoshughulikia Wizara ya Biashara tumeshuhudia Mhe. Rais wakati wowote anaweza kuvunja wizara akaongeza kitu au akapunguza kitu.

Mhe. Mwenyekiti, nikatoa mfano kuwa tulikuwa tuna Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imebakia afya, ustawi wa jamii imekwenda kwa Mhe. Maudline Cyrus Castico, Maji Umeme Nisharti na Mazingira imekwenda Wizara ya Ardhi, Maji, Mazingira na Nisharti. Kwa hili nafikiri likikataliwa sijui itakuwaje lakini liko wazi tena halitaki tochi.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nimuite Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kutengua Kanuni ya Muda.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda uliombele yetu hautoshi kukamilisha shughuli iliyo mbele yetu na kwa kuwa inatubidi kumaliza shughuli hii leo hii. Kwa hivyo, naomba Baraza lako Tukufu tuweke Kanuni ya Muda kando, ili tumalize shughuli zilizo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwa hichi mimi sina pingamizi na pendekezo la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa sababu ni kubadilisha tu kusema wizara inashughulikia masuala ya biashara, viwanda sawa sawa haina shida.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, huu ndio uzoefu wa waziri wa siku nyingi ahsante sana tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu	16	Kazi za Kamati Tendaji Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu	17	Mkutano wa Kamati Tendaji

Sehemu ya Nne

Uanzishaji wa Kamati za Baraza

Kifungu 18

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia na kama tunavyotambua kwamba *sprit* ya mswada huu ni kuweka ukaribu baina ya sekta binafsi pamoja na sekta umma, ili kutatua dhamira kuu.

Tukiangalia kamati ambazo zimetajwa kama zilivyoelezwa katika sheria hii nilizungumza suala la uwanja wa Mao Tse-Tung, kwamba kufuatana na tangazo la Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, ambaye anayesimamia masuala ya kazi, Juni tarehe 30 kwamba vibarua pale sasa hivi wanalipwa shilingi elfu 10, fundi pamoja na kibarua kwa kutwa wanapofanya kazi huku ukizingatia kwamba wanatakiwa walipwe shilingi elfu 25 na elfu 30.

Sasa, katika *spirit* ambayo tunakwenda nayo na huku tukiangalia hitilafu kama hii na hapa tukitambua kwamba mradi huu unafadhiliwa na marafiki zetu ambao ni wakubwa wa Jamhuri ya Muungano pamoja na sisi kwa upande wa Zanzibar ambao ni Wachina.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata maelezo kwamba hapa tunapitisha mswada huu kwa lengo la kuweka ukaribu baina ya sekta binafsi na sekta ya umma, lakini kwa tangazo la serikali pamoja na kauli ya Mhe. Balozi Seif Ali Iddi ambaye ni Makamo wa Pili wa Rais, ametaka watu wote waweze kulipa kima ambacho ni kipya. Kwa hivyo, naomba tuelezwe hapa leo Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nafikiria yupo pamoja na Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, ambaye anasimamia Uwanja wa Mao Tse- Tung tupate maelezo kidogo juu ya hili. Ahsante

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa tunajenga Baraza tunalitengeneza liwe bora zaidi, sasa haya masuala kwamba kuna matatizo ya ajira sijui kulipana. Nafikiri, Baraza likishakuwa tayari haya yatazungumza ni moja ya ajenda ambayo inatakiwa izungumzwe huko, lakini hapa sio mahali pake.

Kwa kweli, hata hao Wachina wanaojenga Mao Tse-Tung stadium wale sio *investors* wale ni wajenzi, sio *investors* ni wageni. Kwa hiyo, hata hiyo sifa ha-*qualified* na ninaweza nikenda mbele zaidi kwa uzoefu wangu kwamba unapokuwa wanajenga kuna mikataba maalum baina ya serikali ile inayotoa misaada kujenga lile jengo. Kwa maana hiyo, haya yote hapa sio pahali pake ningemuomba Mhe. Simai Mohammed Said twende kwenye Baraza hili likishaundwa haraka haraka haya yatazungumzwa kwa vizuri tu kwa murua maneno ya siku hizi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohammed Said, nadhani tunakubaliana hivyo sio pahali pake hapa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Tuendelee Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa majibu yake ya utulivu na ufafanuzi na mifano mbali mbali. Katika kifungu hichi cha 18 nilikuwa nina hoja ambayo ilikuwa kwenye kifungu cha kidogo cha 4 kinachosema Bila ya kuathiri Masharti ya kidogo cha 3 cha kifungu hichi, bodi inaweza kuanzisha kamati.

Sasa, nilihoji kuhusu bodi na kwa sababu bodi hii haikutajwa kwenye ufafanuzi hapa kidogo nilikuwa nahitaji maelezo, kwa sababu Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko inaonesha kalisahau au pengine sikusikia.

Vile vile, katika kifungu kidogo cha 5 Wajumbe wa Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha 3 cha kifungu hichi watakuwa kama walivyoainishwa katika chini ya Jaduweli la pili la sheria hii. Lakini ukija ukiangalia kwenye jaduweli lenyewe kifungu hichi kina *reflect* kwenye jaduweli la tatu. Sasa unajua hapa tunatunga sheria sasa inawezekana pengine kwenye marekebisho ilifanywa kama haijafanywa, lakini ukiangalia hata hilo jaduweli lenyewe linasema chini ya kifungu cha 18(5). Lakini huku kwenye kifungu chenyewe cha sheria kifungu kidogo cha 5 kinasema chini ya jaduweli la pili la sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi. Lakini yale mengine aliyoelezea na tunamshukuru sana kwa kufanya marekebisho katika lile eneo la Wajumbe wa Kamati na yale merekebisho aliyofanya hasa ndio yaliyokuwa yanatakiwa, kwamba itoke ridhaa kwenye jopo la mabaraza la biashara kuweza kumteua mtu ambaye ataingia katika ile nafasi kuliko kutaja jina la kampuni moja kwa moja kwa sababu kidogo ingelileta taswira mbaya kwa jamii. Pamoja na hayo namshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza niwaambie jambo moja kwamba wakati mwengine Mhe. Waziri anapojibu walioiuliza huwa hawapo, lakini pia vile vile hiki kifungu Nam. 5 kimo katika marekebisho ya Kamati imetajwa na mengine yametolewa ufafanuzi. Hata hivyo, nampa fursa Mhe. Waziri atoe majibu ambayo yamebakia.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, pale nilisema kwamba neno Bodi libadilishwe kuwa Baraza, lakini pia hii *Schedule* ya pili isomeke *Schedule* ya tatu na marekebisho yamo humu lakini sijui kama wenzetu wameyasoma yote lakini mambo mengi humu yamerekebishwa na yamo katika *attachment.*

Kifungu	18	Kamati za Baraza pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu	19	Kumualika Mtu pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu	20	Kazi za Kamati pamoja na Marekebisho yake.

Sehemu ya Tano

Masharti Yanayohusiana na Mabaraza ya Mikoa

Kifungu 21

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake na ufafanuzi kwa Waheshimiwa Wajumbe. Lakini, Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nachangia nilishauri kwamba kwa kuwa Wakuu wa Mikoa watakuwa Wenyeviti wa Mabaraza husika ya Mikoa yao, na kwa kuwa

shughuli zenyewe za uchumi ziko kule hasa kwenye Mikoa, basi nilishauri Wakuu wa Mikoa wawe Wajumbe wa Baraza kuu la Taifa, lakini naona Mhe. Waziri dada angu hajajibu hajasema chochote. Kwa hivyo, naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Wakuu wa Mikoa kuwa katika Baraza haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mawaziri wamo katika Baraza lile na wanawakilisha Mikoa, kwa sababu mambo yote yanayotoka chini yanakuja serikalini kupitia mawaziri yanaletwa katika vikao vile. Kwa hivyo, hatukupendekeza Wakuu wa Mikoa kuwemo. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake, lakini naona hajasema lolote kwamba watakuwa wanaalikwa au *total* watakuwa hawamo hawaingii, kwa sababu wao ndio wanaosikiliza hasa kule katika mikoa yao.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ukisoma Wajumbe wa kunako jukwaa humu mna nafasi kubwa kwenye mkutano wa jukwaa ya viongozi wengi ambao wanashiriki. Kwa hivyo, baada ya Baraza kuzungumza na kutiwa kwenye kamati na utekelezaji unavyotaka kutoka wanaweza wote hawa na ndio ilivyo wanahudhuria kwenye jukwaa ambalo linakuwa kubwa zaidi, na linakuwa na uwezo zaidi na upanda zaidi wa mazungumzo zile *issue* ambazo zimepita kwenye Baraza.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, narudia pale pale kwamba katika Mabaraza ya Mikoa shughuli za kiuchumi ziko katika Mikoa yetu, na hawa Wakuu wa Mikoa ni Mwenyeviti wa Mikoa yao, sasa basi angalau Mhe. Waziri wangekuwepo japo Wakuu wa Mikoa wawili wakaweza kuwakilisha.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, labda nitoe ufafanuzi tu kwa Mhe. Amina Iddi Mabrouk tararibu za serikali zinakwenda kwa taratibu zilizowekwa, Wakuu wa Mikoa wanawakilishwa na wizara zilizohusika, ni kweli mambo mengi yanafanyika kule chini, ndio maana tukaweka Baraza la Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Sehemu ya Sita Uanzishwaji wa Jukwaa la Biashara ni kifungu cha 1(6) kinasema Wajumbe wa Baraza la Mikoa huku wanahudhuria katika Mkutano ule mzima na mazungumzo yote wanayajua na wanashiriki, lakini kunako Baraza ambako ni idadi maalum na zaidi waliokuwemo mle ni Mawaziri na Makatibu Wakuu hawezi kuingia Mkuu wa Mkoa mle kwa sababu utaratibu haufanywi hivyo kiserikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Amina Iddi Mabrouk asome kifungu cha 21(1)(2) atakuta Mkuu wa Mkoa wa Mkoa husika atakuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mkoa. Kwa hivyo, ile hoja yake ambayo amekuwa ameijenga kwa Wakuu wa Mikoa kwenye Mabaraza ya Mikoa na wao wanaingia kwa kifungu cha 21(2).

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemuelewa sana Mhe. Waziri lakini pia nimemuelewa zaidi Mhe. Mwanasheria Mkuu na nimesoma kwa umakini sana

na nimeona kwamba Wakuu wa Mikoa wote watakuwa Wenyeviti wa Mabaraza Mikoa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Kifungu 21 Muungo wa Baraza la Mkoa na Marekebisho yake
Kifungu 22 Kazi za Baraza la Mkoa na Marekebisho yake
Kifungu 23 Wajibu wa Baraza la Mkoa na Marekebisho yake

Sehemu ya Sita

Uwanzishwaji wa Jukwa la Biashara

Kifungu 24 Kuanzishwa kwa Jukwa la Biashara na Marekebisho yake

Sehemu ya Saba

Masharti ya Fedha

Kifungu 25 Vyanzo vya Fedha na Marekebisho yake
Kifungu 26 Makadirio ya Mwaka na Marekebisho yake
Kifungu 27 Hesabu za Ukaguzi na Marekebisho yake

Sehemu ya Nane

Masharti Mengineyo

Kifungu 28 Kanuni
Kifungu 29 Kufuta na Kubakiza Pamoja na Marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na Marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri Biashara, Viwanda na Masoko wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara la Mwaka 2017

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kunzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo mengineyo yanayohusiana na hayo usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naafiki

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji tena wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hapo ndio mwisho wa shughuli yetu ya leo, lakini pia iwashukuru sana kwa kufanya kazi nzito hii ambayo ilikuwepo kwa ajili ya taifa letu. Pia msisahau kwamba Tangazo lililotoka kwamba baada ya kuakhirishwa Kikao hichi Wajumbe tuendelee kubaki. Naakhirisha Kikao hichi hadi kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:48 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 29/9/2017 saa 3:00 za asubuhi)